**Ndani** Pata makala na chambuzi za uchumi zilizoandikwa na waandishi mahiri

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00085 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumamosi Oktoba 12-14, 2024 |

# Samia jabali la uchumi

Uk. 6





## TASAF inavyoinua hali ya maisha ya Watanzania wenye hali duni

Uk. 12-13

## Sekta ya bima na ukuaji wa uchumi, uimarishaji afya nchini Tanzania

Uk. 10-11

rifaly

Habarika kidijitali! Soma gazeti la Uelekeo ndani ya Rifaly!



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com





# Mikakati ya Samia kuondoa hali ngumu ya maisha

**Na John Ngunge**

KATIKA siku za hivi karibuni, kumekuwa na maneno mengi kutoka kwa watu wa rika na aina tofauti za kimaisha, wakilalamikia ukali wa maisha.

Kwa madai yao, ukali au ugumu wa maisha unatokana na Watanzania wengi kukosa fedha za kukidhi manunuzi ya mahitaji muhimu hasa ya kijamii kama vile ya chakula, ujenzi wa nyumba za kuishi, tiba, usafiri na kadha wa kadha.

### WANASIASA KUFANYA MTAJI

Kuna wanaotumia mitandao ya kijamii kujadili hapa na pale, madai ambayo baadaye yamedakwa na baadhi ya viongozi wa asasi zisizo za kiraia na kisha vyama vya siasa vya upinzani na kuyafanya kuwa mtaji wao wa kisiasa!

Wanasiasa wamebeba madai hayo na kuanza 'kulia' nayo mitaani katika maandamano yao huku wakitumia pia mambo ambayo yalikuwa yakijitokeza kutokana na matatizo ya hali ya hewa kama vile kupanda kwa bei ya sukari miezi michache iliyopita, tatizo ambalo serikali ilikuwa ikilishughulikia vyema kabisa.

### LAWAMA BILA UTAFITI

Tukashuhudia serikali ikinyooshewa kidole kwa madai kwamba inahusika na hali hiyo, shutuma ambazo zinatajwa kiholela bila kufanyiwa kwanza uchunguzi wala utafiti. Lakini wanaotoa shutuma kwa serikali, hawaelezi pia mikakati mbalimbali mizuri ambayo serikali inapambana kuifanikisha ili kunyanyua hali za maisha ya wananchi, tena kuanzia shuleni.

Kuonesha lawama bila uchunguzi kwa mfano, walioilaumu serikali kwenye kupanda kwa bei ya sukari mwanzoni mwa mwaka huu hawakuzingatia kwamba hali ile ilitokana na mvua nyingi za El-Nino zilizoathiri uzalishaji wa miwa, hali iliyosababisha viwanda vya ndani kusitisha uzalishaji kwa muda na hivyo kusababisha upungufu mkubwa wa upatikanaji wa sukari sokoni.

Pili, licha ya serikali kutoa vibali vya kuagiza sukari kutoka nje, baadhi ya wazalishaji walishindwa kuagiza kiwango cha kutosha, hali iliyochangia kuendelea kwa uhaba wa sukari sokoni na kusababisha bei kupanda zaidi. Aidha, gharama za usafiri na changamoto za usambazaji pia ziliongeza mzigo wa bei kwa watumiaji.

Serikali ikaendelea kuchukua hatua kwa kuruhusu uingizaji wa sukari zaidi kutoka nje hadi pale hali ilipotulia.

Hapo serikali ilikuwa inahusika vipi na kupanda kwa bei ya sukari hadi wale wapenda maandamano kubebea bango bei ya sukari?

Tukirudi kwenye lawama dhidi ya serikali kuhusu maisha magumu, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) katika maandamano waliyofanya maeneo mbalimbali nchini walikuwa wakiitaka serikali ipeleke bungeni mpango wa kukwamua wananchi na hali ngumu ya maisha.

Chini ya mpango huo walitaka bei ya bidhaa muhimu ishushwe (ikiwemo sukari) au kuweka ruzuku katika baadhi ya bidhaa.

Lakini wakawa hawawaambii wananchikwamba serikali imeshashusha tozo kibao na kuweka ruzuku kwenye bidhaa muhimu kama petroli, ikaweka ruzuku kwenye mbolea na kuondoa tozo kibao kwenye sekta ya kilimo kama makala hii inavyoendelea kujadili kwa kina.

Wakawa pia wamejitoa ufahamu kwamba mahitaji ya nchi ni mengi, kuweka ruzuku kwenye kila bidhaa na kuondoa tozo unavuruga bajeti na hivyo kuna mambo hayatakwenda kwa sababu nakisi ya bajeti itakuwa kubwa na nchi inapolazimika kukopa ili kufidia nakisi ya bajeti, hao hao jamaa wanapiga tena kelele na kuhoji kwa nini nchi inakopa!

Ndio maana nimeona tukumbushane kwamba mambo hayo wakati mwingine hayahitaji hasira bali utulivu wa mawazo na nguvu ya hoja.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kuwa bila kuathiri sheria za nchi, kila mtu yuko huru kutoa maoni yoyote na kutoa nje mawazo yake.

Wanazuoni pia kwa upande wao wanaosema bila utafiti mtu hana haki ya kuzungumza (no research, no right to speak). Kwa tafsiri ya kawaida ya mtaani ni kwamba usipokuwa na hoja zilizoenda shule, mazungumzo yako yanakosa ushawishi.

Katika akaunti ya mtandao wa kijamii wa X, Richard Mabala anapigilia msumari msemo huo kwa kuongeza, 'no investigation, no right to judge.' Kwa tafsiri yangu isiyo rasmi ni kwamba bila uchunguzi, hakuna haki kuhukumu.

### HATUA ZA SERIKALI

Sasa ni hivi! Tangu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan aingie madarakani Machi 2021, taarifa zinaonesha kuwa serikali anayoiongoza imechukua hatua za muda mfupi na muda mrefu katika kupambana na ukali wa maisha kwa wananchi.

Wengi hawakuziba masikio yao pamba pale Rais Dk. Samia alipoamua kuchukua hatua za muda mfupi kutoa ruzuku ya shilingi bilioni 100 kwenye mafuta hadi pale hali ya bei ya mafuta duniani itakaporejea katika hali ya kawaida. Tamko lake alilitoa Juni 2022 akiwa mkoani Kagera.

Pia tulisikia Septemba 2022, Rais Dk. Samia akiidhinisha shilingi bilioni 150 kutumika kwa ajili ya ruzuku ya mbolea katika msimu wa 2022/23 ili kuwezesha upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa wingi na kwa gharama nafuu.

Ruzuku hiyo ililenga kuongeza uzalishaji wa chakula nchini na hivyo kuwa na usalama wa chakula na kukidhi upatikanaji wa malighafi za viwanda vya ndani.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alilieleza Bunge jijini Dodoma, Septemba 23, 2022 kwamba katika kipindi cha mwaka 2021/22, tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula imeonesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula umefikia tani milioni 17.4, ambapo kati yake uzalishaji wa mazao ya nafaka ni tani milioni 9.4 na mazao yasiyo ya nafaka ni tani milioni 7.9.

"Mahitaji yote ya chakula yanayojumuisha nafaka na yasiyo ya nafaka kwa mwaka 2022/23 ni zaidi ya tani milioni 15 ambapo tani milioni 9.5 ni za mazao ya nafaka na tani milioni 5.5 ni mazao yasiyo ya nafaka.

"Kwa kulinganisha uzalishaji na mahitaji, nchi yetu ina kiwango cha utoshelevu wa chakula wa asilimia 115.

Alisema ili kuhakikisha hali ya chakula nchini inaendelea kuimarika, Serikali imeuwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kuhifadhi tani 147,142 na kuendelea kununua mazao ya chakula kwa ajili ya kuhifadhi.

Aidha kupitia kwa aliyekuwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (Sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira), Februari mwaka jana, alitoa vibali vya kuingiza nchini tani 90,000 za mchele ili kuwezesha wananchi wanunua zao hilo kwa bei inayohimilika.

Pia aliondoa baadhi ya kodi ili zao hilo liweze kuongezeka kwenye soko.

Wakati ulipotokea uhaba mkubwa wa sukari nchini mapema mwaka huu, Serikali ilitoa vibali vya kuagiza sukari kutoka nje ili kuondoa changamoto hiyo.

Tumeshuhudia pia Agosti mwaka huu, Rais Dk. Samia akizindua kiwanda cha Sukari cha Mkulazi kilichopo Kata ya Mbigiri, wilayani Kilosa, ambacho kina uwezo wa kuzalisha tani 50,000 za sukari kwa mwaka huku mipango ikiendelea kusukwa kujenga kiwanda kingine cha sukari cha Mkulazi one.

### TAARIFA YA HALI YA UCHUMI

Aidha katika rejea ya taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2021 inatuonesha kuwa Serikali ya Awamu ya Sita iliendeleza juhudi za kuboresha maendeleo ya watu kwa lengo la kuinua viwango vya maisha.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, maendeleo ya watu ni kipimo muhimu cha maendeleo na ustawi wa nchi kwa ujumla na huboreshwa kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma muhimu ikiwemo maji, elimu na afya.

Aidha, taarifa inasema maendeleo ya watu huathiriwa na masuala mbalimbali ikijumuisha wastani wa idadi ya watu kwa kaya, uwiano wa utegemezi na rushwa.

### UJENZI WA UCHUMI JUMUISHI

Serikali ya Dk. Samia inaendelea kuweka msukumo katika kujenga uchumi jumuishi wa viwanda wenye lengo la kuongeza fursa za ajira na kupunguza umaskini.

Inaendelea uk. 3

# Mikakati ya Samia kuondoa hali ngumu ya maisha

Inatoka uk. 2

Kuhusu hali ya umaskini na maendeleo ya watu, Serikali kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka

Mitano (2021/22 - 2025/26) - FYDP III, iliendelea kutekeleza sera na mikakati mbalimbali inayolenga kuongeza kasi ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mpango huo unalenga kupunguza uwiano wa idadi ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini wa chakula kutoka asilimia 8.0 mwaka 2018 hadi asilimia 5.8 mwaka 2025/26.

Taarifa hiyo inaonesha uwiano huo kwa upande wa vijijini unatarajiwa kupungua kutoka asilimia 9.7 mwaka 2018 hadi asilimia 8.0 mwaka 2025/26 na upande wa mijini kutoka asilimia 4.4 mwaka 2018 hadi asilimia 3.1 mwaka 2025/26.

Aidha inasema umaskini wa chakula kwa ujumla ulipungua kwa asilimia 1.7 na kufikia asilimia 8.0 mwaka 2021 kutoka asilimia 9.7 mwaka 2012.

Inasema kupungua kwa viwango vya umaskini kulitokana na jitihada mbalimbali za Serikali ikiwemo kuendelea kuziwezesha kaya maskini kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini – TASAF pamoja na kuimarika kwa sekta ya kilimo inayotegemewa na wananchi wengi wa kipato cha chini.

### HATUA ZAIDI

Pia, hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, aliyowasilisha bungeni wakati akielekeza hali ya uchumi kwa mwaka 2024/25 kuhusu na mpango wa maendeleo wa Taifa, inabainisha hatua mbalimbali zilizochukuliwa na serikali kuhusu suala hilo.

Kwa mfano, Profesa Mkumbo anasema utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti na kuanza kuimarika kwa upatikanaji wa mazao ya chakula katika masoko ya ndani na ya nchi jirani, kumepunguza mfumuko wa bei pamoja na mambo mengine.

Anabainisha kuwa kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea kilipungua na kufikia asilimia 1.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 2.6 mwaka 2022.

### VITA YA URUSI NA UKRAINE

Anasema ongezeko dogo la kasi ya ukuaji wa uchumi wa mataifa yaliyoendelea la asilimia 1.6 mwaka 2023 hadi matarajio ya asilimia 1.7 mwaka 2024 na asilimia 1.8 mwaka 2025 linachangiwa na madhara ya vita inayoendelea kati ya Urusi na Ukraine.

Madhara hayo kwa kiasi kikubwa anasema yameyumbisha siyo tu uchumi wa nchi za Ulaya bali hata uchumi wa dunia nzima.

Vita hiyo imechangia kuongezeka kwa gharama za maisha kulikosababishwa na mfumuko wa bei za nishati barani Ulaya na bei za vyakula katika soko la dunia.

Akifanya marejeo ya taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili mwaka huu, inaonesha kuwa kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa upande wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kilikuwa cha wastani wa asilimia 3.8 mwaka jana ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.9 mwaka juzi.

Anasema kupungua kwa ukuaji kulitokana na kuongezeka kwa mfumuko wa bei, kuongezeka kwa gharama za ukopaji katika masoko ya fedha ya kimataifa, kupungua kwa misaada na mikopo nafuu ya kibajeti, athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na athari za vita hiyo inayoendelea.

Aidha, anasema ukuaji wa uchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ulikuwa wa wastani wa asilimia 4.4 mwaka jana ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.2 mwaka juzi.

### MFUMUKO WA BEI

Sasa kwa hapa nyumbani, Profesa Mkumbo anasema, mfumuko wa bei ulifikia asilimia 3.1 katika kipindi kilichoishia mwezi Aprili mwaka huu, ikilinganishwa na asilimia 4.3 katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Anasema mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka jana, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.3 mwaka juzi.

"Kiwango hiki ni cha chini ikilinganishwa na nchi wanachama wa EAC na kipo ndani ya malengo ya kati ya asilimia 3.0 hadi 7.0 na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kikanda (EAC na SADC)," anasema.

Mwaka 2021, Serikali iliendelea kuboresha hali za maisha ya watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri kupitia programu mbalimbali ikiwemo Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini.

Mpango huo unatekelezwa kupitia maeneo matatu ambayo ni pamoja na kuhawilisha fedha kwa kaya maskini ili ziweze kukidhi matumizi ya kaya; kutoa ajira za muda kwa kaya za walengwa ili kuongeza kipato; na kuhamasisha uundaji wa vikundi vya kuweka akiba, kukopeshana na kuwekeza kwenye miradi ya uzalishaji mali kupitia vikundi hivyo.

### SERIKALI IMEJITAHIDI

Hayo, pamoja na mambo mengine mengi yanathibitisha kazi kubwa ambayo serikali imechukua katika kuwaondolea wananchi ukali wa maisha kwa muda mfupi na kwa muda mrefu. Kwa lugha nyingine, Rais Samia ameweka mikakati madhubuti ya kupunguza umaskini nchini kwa kuimarisha na kuboresha sekta muhimu za miundombinu na kilimo lakini pia sekta ambazo sikuzizungumzia kwa kina sana kama utalii, madini, nishati na viwanda bila kusahau kuvutia uwekezaji na kuboresha mazingira ya biashara. Pia sikuzungumzia mpango wa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwa vikundi vya wanawake, vijana na walemavu na halmashauri zetu mbazo lengo lake ni kupambana na umaskini.

Mkakati wa Rais Samia unajikita katika falsafa ya "R4" inayolenga mageuzi, ufanisi na kuimarisha taasisi za umma ili kuongeza ajira, kuongeza mapato ya taifa, na kuboresha hali ya maisha. Wananchi ni waelewa, huweza kuchambua chuya kwenye mchele.

Katika muktadha huo, Rais pia anaendelea kuboresha elimu ya ufundi ili vijana waweze kupata ujuzi unaohitajika katika soko la ajira.

Serikali inapanga kujenga vyuo vya ufundi katika kila wilaya na kuimarisha elimu ya ufundi badala ya kusisitiza tu elimu ya kitaaluma na hata mtaala mpya wa elimu unajelekeza kwenye elimu ya amali na ujasiriamali.

Rais pia anaboresha sana ushirikiano wa kimataifa.

Tanzania inaendelea kushirikiana na nchi kama China, Korea Kusini na nyiginezo ili kufadhili miradi mbalimbali na kuleta mitaji nchini na ujuzi, mambo ambayo yataimarisha uchumi na kupunguza gharama za biashara.

Pia, nchi inapokea mikopo yenye masharti nafuu ili kuimarisha miradi hii itakayosaidia kubadilisha maisha ya Watanzania ikiwemo kutengeneza ajira.

### WANANCHI KUPAMBANA NA UMASKINI

Wananchi wanapaswa pia kuchukua hatua kadhaa kupambana na umaskini na maisha magumu. Hapa nitataja njia kadhaa ambazo zinaweza kusaidia:

Mosi, ni kujielimisha na kuongeza ujuzi: Elimu ni moja ya silaha kubwa dhidi ya umaskini. Wananchi wanapaswa kuwekeza katika elimu, mafunzo ya ufundi stadi na kujifunza ujuzi mpya kama vile teknolojia, biashara, au kilimo cha kisasa ili kuimarisha kipato chao.

Mbili, ujasiriamali: Badala ya kutegemea ajira za serikali au sekta binafsi pekee, wananchi wanaweza kuanzisha biashara ndogondogo kama ufugaji, kilimo, ushonaji, biashara za rejareja, au huduma za mtandao. Ujasiriamali unatoa fursa ya kujitegemea kiuchumi.

Tatu, kushirikiana katika vikundi vya kijamii: Kuanzisha vikundi vya ushirika, vikoba, au SACCOS (Savings and Credit Cooperatives) kunaweza kusaidia watu kuwekeza pamoja, kupata mikopo ya bei nafuu, na kufanya miradi ya maendeleo.

Nne, kilimo cha kisasa na biashara ya chakula:

Wananchi wanapaswa kutumia mbinu za kilimo bora kama vile umwagiliaji, matumizi ya mbegu bora, na mbolea za kisasa ili kuongeza mavuno na kupata kipato zaidi. Pia, wanaweza kuwekeza katika usindikaji wa mazao na kuyauza kwa faida.

Tano, kubadilika kiakili na kuwa na ubunifu: Wananchi wanapaswa kuwa na mawazo ya kubadilika na kubuni njia mpya za kujikimu kimaisha. Wanaweza kutafuta njia mbadala za kupata kipato, kama vile kazi za mtandaoni au kufanya kazi katika sekta ambazo hazihitaji uwekezaji mkubwa.

Sita, kuweka akiba na uwekezaji: Ni muhimu kwa wananchi kujifunza kuweka akiba kidogo wanayopata na kuwekeza katika miradi midogo midogo inayoweza kuzaa matunda baadaye.

Saba, ushirikiano wa kijamii na misaada ya kimaendeleo: Jamii inaweza kushirikiana kwa kusaidiana na kutekeleza miradi ya kijamii kama vile ujenzi wa miundombinu ya kijamii na biashara ndogondogo ambazo zitasaidia watu wengi kupata kazi na kipato.

Nane, uzazi wa mpango: Baadhi ya nchi zilizoendelea kama Singapore, Korea Kusini, na nyinginezo ambazo miaka ya 1960 wakati tunapata uhuru tulikuwa na maendeleo karibu sawa, uzazi wa mpango pia umezisaidia sana kuzinanyua kiuchumi. Kuna nadharia zinaonesha kwamba bila kuwa na uzazi wa mpango, wategemezi watakuwa wanaongezeka kila kukicha kwenye familia, kila siku vitanda mahospitalini havitatosha hata mwongeze vipi na hata madawati na madarasa kila mwaka yataonekana hayatoshi!

Kwa hiyo kupambana na umaskini ni jitihada ya pamoja ambayo inahitaji uhamasishaji wa kila mtu binafsi, familia na jamii kwa ujumla.

Serikali inaweza kusaidia kwa kuweka mazingira wezeshi, lakini wananchi wanapaswa kuchukua hatua binafsi na za kijamii kuimarisha hali zao za kiuchumi. Hata vyama vya siasa vinavyolalamikia ugumu wa maisha, vinapaswa kuwaambia wananchi mambo ya kufanya wao wenyewe ili kujiletea maendeleo na namna ya kufikia hayo maendeleo.



# Usafiri wa anga unavyoimarishwa nchini na umuhimu wake

## ● Matumaini ya ATCL 'kutoboa' katika ukanda huu ni makubwa

**Na Hamid Yassin**

JULAI 30, mwaka 2021, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dk. Samia Suluhu Hassan, ilipokea ndege yake ya kwanza aina ya Bombadier Dash 8-Q400.

Ndege hiyo ilikuwa ya tisa kufika nchini kati ya ndege zilizonunuliwa na Serikali kwa ajili ya kuimarisha sekta ya usafirishaji nchini.

Ndege nyingine nane zilifika nchini wakati wa Serikali ya Awamu yan Tano. Agosti 20 2024, yaani mwezi uliopita, Serikali ya Awamu ya Sita ilipokea ndege nyingine mpya aina ya Boeing B8787- Dreamliner ikiwa ni ndege ya 7 kununuliwa ndani ya awamu hii ya sita kati ya 15 zilizonunuliwa tangu mwaka 2016.

Ndege hii iliyopokelewa kule Zanzibar na Rais wa visiwa hivyo, Dk. Hussein Ali Mwinyi ina uwezo wa kubeba abiria 262, ina viti 22 vya daraja la biashara na viti 240 daraja la kawaida.

Pia ina uwezo wa kubeba mizigo kati ya tani 15 hadi 20 kulingana na ujazo wa abiria na mizigo. Tumeambiwa bado ndege nyingine zinakuja!

Wakati huu Serikali ya awamu ya 6 ikiendeleza jitihada na kazi kubwa ya kuliimarisha Shirika letu la Ndege na sekta nzima ya anga, wengi wanaohoji kwa nini Serikali iendelee kununua ndege?

Je, ununuzi huu wa ndege una faida gani kwa Taifa hasakiuchumi na maendeleo ya watu?

Mtiririko huu wa Awamu ya Sita kuendelea kuliimarisha shirika la ndege kwa kuendelea na ununuzi wa ndege ulioanza toka kipindi cha Awamu ya Tano kwa kufufua Shirika la Ndege la Taifa (ATCL) kutoka kuwa na ndege 1 mpaka sasa kuwa na ndege zake 15 umekuwa na maswali na mijadala mingi sana mitaani hasa kwenye makundi mbalimbali ya Watanzania. Baadhi yao wanahoji kila mmoja kwa upande wake kuhusu maamuzi haya ya Serikali kuendelea kununua ndege na faida yake kwa nchi na maendeleo?

Upande mmoja ukikubaliana na kupongeza maamuzi ya Serikali kununua ndege hizi kama kichocheo kikubwa cha uchumi wa Taifa huku upande wa pili ukikosoa maamuzi hayo ya Serikali.

Hawa wa pili wanahoji kama kweli ndege ni hitaji muhimu la Mtanzania kwa sasa au kuna mahitajio mengine muhimu zaidi?

Je, ndege inamsaidiaje Mtanzania wa kawaida wa Katavi ndani ndani huko tena wa kipato cha chini asiye na uhakika hata wa mlo mmoja? Ni Watanzania wangapi wanao uwezo wa kukidhi na kutumia usafiri wa ndege?

Sasa mjadala huu unatupeleka kujadili kwa undani sababu za msingi za kiuchumi za nchi yetu kuimarisha Shirika la ndege na kuendelea kununua ndege.

### KWA NINI TANZANIA IIMARISHE USAFIRI WA ANGA

Tafakuri hii ni pana sana na tunaweza kuianza kwa kuangalia kidogo falsafa ya Baba wa uchumi wa ulimwengu, Adam Smith.

Mtaalamu na mbobezi huyu mkubwa wa uchumi wa Uingereza Adam Smith, anayechukuliwa kama baba wa mifumo yote ya kiuchumi na nadharia zake zote za ulimwenguni aliwahi kusema kwamba uchumi imara ni ule 'Cycle Economic engaged Routine' yaani uchumi ulioko kwenye mzunguko na unaoishi na kutegemea maeneo mengi.

Unapotaka kujenga uchumi imara na vita yenyewe ya kusukuma uchumi uende mbele ni lazima uwe na nyenzo nyingi za kukufikisha na kukupeleka mbele.

Nyakati hizi ambazo Tanzania inahaha kutekeleza azma yake ya kujenga Taifa imara la uchumi wa kati, inahitaji sana ndege kwa sababu zifuatazo:-

### KUUNGANISHA DUNIA

> **Ndege nyingine nane zilifika nchini wakati wa Serikali ya Awamu yan Tano. Agosti 20 2024, yaani mwezi uliopita, Serikali ya Awamu ya Sita ilipokea ndege nyingine mpya aina ya Boeing B8787-Dreamliner ikiwa ni ndege ya 7 kununuliwa ndani ya awamu hii ya sita kati ya 15 zilizonunuliwa tangu mwaka 2016.**

Usafiri wa ndege unawawezesha watu kutoka mataifa na mabara mbalimbali kuwasiliana kwa urahisi. Hii inaboresha mahusiano ya kidiplomasia, biashara, na utamaduni, na pia kurahisisha safari za kibinafsi kama vile kutembelea familia na marafiki.

Katika masuala ya diplomasia na ushirikiano wa kimataifa, usafiri wa anga unachangia sana katika kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kati ya nchi mbalimbali. Pia unawezesha mikutano ya kimataifa na matukio mengine muhimu kufanyika kwa urahisi kwa kurahisisha usafiri wa viongozi na washiriki wa kimataifa.

Ununuzi wa ndege na uboreshaji wa sekta nzima ya anga unalichangamsha Taifa, kuharakisha shughuli za watu na uchumi.


Taifa ambalo halina usafiri wa anga imara haliwezi kuendelea na mara zote shughuli za watu na uchumi zitakwenda taratibu sana na kulala.

Leo kupitia ndege hizi mfanyabiashara wa Dar anaweza kusafiri kwenda Mwanza na kurudi ndani ya siku moja kuliko kupoteza muda wa siku nzima kusafiri kwa gari. Unaweza

Inaendelea uk. 5




Bombadier Dash 8-Q400



**Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa na viongozi wengine wakati akikata utepe kuzindua ndege mpya ya mizigo Boeing 767-300F ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) kwenye hafla fupi iliyofanyika katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam Juni 3, 2023.**

# Usafiri wa anga unavyoimarishwa nchini na umuhimu wake

Inatoka uk. 4

kutoka Dar ukaenda Kigoma kikazi na jioni yake ukarudi. Mzigo unaweza kutoka Dar asubuhi na ndani ya saa ukafika Dodoma, Tanga au Mtwara.

Katika ujenzi wa uchumi na dunia hii ya utandawazi muda ni kila kitu. Bila usafiri imara wa ndege nchi inadumaa na hakuna jambo linaweza kwenda katika nchi. Ni kupitia usafiri huu wa ndege ambao ni wa haraka na unaobeba watu wengi unaolifanya Taifa kuwa 'bize' na shughuli za kiuchumi na za watu wake kiurahisi zaidi na salama.

Kimsingi, usafiri wa anga ni njia ya haraka zaidi ya kusafiri umbali mrefu. Mashirika ya ndege yanasaidia kusafirisha abiria kwa muda mfupi, ambayo ni muhimu hasa kwa safari za kibiashara na za dharura.

### KUKUZA UTALII

Tanzania inatajwa kuwa nchi mojawapo iliyobarikiwa kila aina ya vivutio vya utalii hapa duniani. Tanzania inatajwa kuwa namba mbili duniani kwa wingi wa vivutio vya utalii baada ya Brazil.

Nchi hii imebarikiwa kila aina ya kivutio cha kumvutia Mtalii kuja kuanzia mbuga, bahari, mito, maziwa, mabonde, visiwa, hifadhi, milima, mapango ya kale, makumbusho ya kale na vingine kedekede.

Kwa namna nchi hii ilivyobarikiwa na vivutio vingi vya utalii, njia pekee ya kukuza utalii wake na kushawishi Watalii wengi kuja ni kupitia ndege. Kwa lugha nyingine ushawishi wa utalii unaanzia kwenye uhakika na urahisi wa usafiri.

Mfano, ukiwa na ndege zako mwenyewe ni rahisi kumtoa mtalii moja kwa moja kutoka New York, Marekani au Brussels, Ubelgiji kuja hapa kwa ndege zako bila kutumia za nchi nyingine ambazo nazo zina vivutio pia.

Ni hivi, mfano Mtalii anayetoka Marekani na anataka kuja kutalii Tanzania lakini akabebwa kwa ndege ya Kenya (KQ) kwa vyovyote vile Kenya itamshawishi atalii pale pale kwa kumuonesha Turkana, Milima Meru ama Mombasa na moja kwa moja nchi yetu itamkosa yule mtalii, mapato yake na hata kama atakuwa na marafiki wa kutalii wote wataishia Kenya!

Kwa hiyo ukiwa na ndege zako mwenyewe utaweza kuwaleta watalii na zaidi kutangaza utalii wako kwa ndege zako kupitia mpaka TV zilizo ndani ya ndege hizo na hakuna mtalii 'atakayechoropoka' kwenda kwingine.

Hata ukiangalia mataifa ya Afrika kama Morocco, Afrika Kusini, Misri, Mauritius, Kenya na Sychelles ambayo hupokea watalii wengi zaidi licha ya kwamba tumewapita kwa vivutio vingi, hutumia zaidi ndege zake kuboresha utalii na kushawishi Watalii wengi zaidi. Kile kile kipindi tulichokuwa hatuna ndege za kutosha kilichangia sana kutufikisha hapa na sasa ndio tunaendelea 'kujitafuta'. Huwezi kujitafuta kama mahala pa kuanzia kwa maana ya kutokuwa na ndege.

Kwa hiyo ununuzi huu wa ndege utatusaidia sana nchi yetu kuboresha utalii kwa kupokea watalii wengi kwa kutumia ndege zetu.



**Rais Dk. Samia akiwa amekaa kwenye chumba cha marubani ya ndege mpya ya mizigo Boeing 767-300F ya ATCL baada ya kuizindua katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.**

### KUKUZA UCHUMI, MASOKO

Sekta ya usafiri wa anga husaidia katika kukuza uchumi wa nchi kwa kurahisisha biashara za kimataifa na usafirishaji wa bidhaa ikiwa ni pamoja na kuiunganisha nchi na masoko ya ndani na ya nje, na hivyo kuwezesha ukuaji wa biashara na uwekezaji wa kigeni.

Ndege zinaendelea kutuwezesha kufungua masoko ya bidhaa za ndani zinazoharibika haraka kwenye masoko ya kimataifa.

Tanzania kwa sasa ni mzalishaji mkubwa wa bidhaa laini na zinazoharibika haraka kama matunda (yakiwemo maparachichi), mbogamboga, maua, nyama na samaki na zinategemea sana kuuza bidhaa hizi nje ya nchi.

Mwaka 2019 tuliuza bidhaa hizi kwa zaidi ya Dola za Marekani milioni 700 na mpaka 2025 kutokana na uzalishaji mkubwa wa bidhaa hizi tunatarajia kuuza bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 2.

Bidhaa hizi zinazoharibika haraka, njia sahihi ya kuhakikisha biashara hii inakuwa himilivu na endelevu ni kuwa ndege zako mwenyewe, hususani ndege za mizigo.

Leo hii Tanzania kupitia ndege hizi imeshaanza kusafirisha nyama, mbogamboga na maua kwenda nje ya nchi na azma yetu ya kuuza bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 2 ifikapo mwakani 2025 huenda ikatimia.

### KUKUZA SEKTA NYINGINE

Sekta ya anga inasaidia sana kukuza sekta nyingine nyingi za kiuchumi na kujenga unyumbulifu wa uchumi wa nchi, yaani 'Diversification of economy' unaotegemea sekta nyingi.

Ukinunua ndege tayari umekuza sekta ya biashara, uwekezaji, utalii, ajira na kujenga uchumi imara unaotegemea katika sekta nyingi (Diversified economy) kwa hiyo badala ya kutegemea sekta moja kama kilimo, ndege zinakuhakikishia ukuaji wa sekta nyingine kwa haraka na ukubwa hivyo kujenga uchumi imara wa nchi usiojifunga katika sekta moja na badala yake hata sekta fulani ikiyumba bado sekta nyingine zinaimarisha uchumi wako. Hakuna mwekezaji anayeweza kuja kwako kutalii kama hauko imara kwenye sekta ya anga. Mwekezaji kabla ya kuchagua nchi kuwekeza anaangalia urahisi wa usafiri ili kurahisisha shughuli zake.

Sasa kwa Taifa kama letu ambalo lina fursa nyingi sana za uwekezaji, biashara, kwenye madini, ardhi, gesi na mengine, njia pekee ya kuinua sekta hizi ni kuimarisha sekta nzima ya usafiri wa anga ili kuwavutia

Inaendelea uk. 6

# Samia jabali la uchumi




**Na Mwandishi Wetu**

TANGU Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani mwezi Machi 2021, Tanzania imepitia kipindi kizuri cha ukuaji wa uchumi kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali na mabadiliko ya sera za kiuchumi, kijamii, na kiutawala. Ikuimbukwe kwamba wakati akiingia madarakani, Tanzania na dunia kwa ujumla ilikuwa inapitia hatua ngumu ya kiuchumi kufuatia janga la ugonjwa korona (Uviko -19) lililoikumba dunia na kufuatiwa na vuita vya Urusi na Ukraie ambavyo pia viliteteresha uchumi wa dunia na kusababisha vitu kama ptroli kupanda, baadhi ya vyakula kama ngano na pembejeo za kilimo.

### MIRADI YA KIMKAKATI NA MIUNDOMBINU

Rais Samia ameendeleza miradi mikubwa ya miundombinu iliyokuwa imeanza awali, lakini pia ameanzisha miradi mipya muhimu. Baadhi ya miradi hiyo ni:

Mosi ni mradi wa Reli ya Kisasa (SGR): Ujenzi wa reli ya SGR unaendelea na unatarajiwa kuimarisha usafirishaji wa mizigo na abiria kutoka bandari ya Dar es Salaam hadi mikoa ya ndani na hata nchi jirani kama Rwanda, Burundi, na DRC. Kwa sasa usafiri huo umefika katikati mwa Tanzania, Dodoma. Hii itaongeza kasi ya ukuaji wa biashara na uzalishaji viwandani.

Pili, mradi wa Bwawa la Umeme la Julius Nyerere (JNHPP): Mradi huu una lengo la kuzalisha megawati 2,115 za umeme, hatua inayotarajiwa kupunguza uhaba wa nishati na kuongeza uwezo wa viwanda. Tayari vinu kadhaa vimeshaanza kuzalisha umeme na kumaliza tatizo la mgao wa umeme.

Tatu, Barabara, madaraja na Viwanja vya Ndege: Serikali imeendelea na upanuzi wa barabara za lami, viwanja vya ndege, madaraja na bandari ili kuboresha miundombinu ya usafirishaji na kurahisisha biashara. Daraja la Magufuli linalounganisha Kigongo na Busisi mkoani Mwanza.

### KILIMO NA MPANGO WA BBT

Serikali ya Rais Samia imeanzisha mpango wa BBT (Building a Better Tomorrow) ambao unalenga kuwasaidia vijana kuingia kwenye sekta ya kilimo kwa kuwapa mafunzo, pembejeo, ardhi, na mikopo ya bei nafuu.

Mpango huu unalenga kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, kuimarisha usalama wa chakula, na kupunguza ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana.

Serikali pia imewekeza katika kuendeleza sikimu kibao za umwagiliaji na na kuongeza maradufu teknolojia bora za kilimo, kuongeza uzalishaji wa mazao muhimu kama vile kahawa, chai, pamba, korosho, na mazao ya chakula kama mpunga na mahindi.

### MABORESHO KATIKA AFYA

Rais Samia ameongeza juhudi katika kuboresha huduma za afya, kwa kujenga na kuboresha vituo vya afya, zahanati, na hospitali na hii lengo likiwa ni kuboresha afya za Watanzania ili kujikita katika uzalishaji na pia kupunguza gharama za kufuata huduma za matibabu mbali na wakati mwingine nje ya nchi. Kwa sasa huduma lukuki ambazo watanzania walitumia mamilioni ya pesa kuzifuata nje ya nchi zinapatikana nchini. Baadhi ya mambo yaliyofanyika katika eneo hili ni kama yafuatayo:

Kwanza, Serikali imeongeza bajeti ya dawa na vifaa tiba, kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi, hasa vijijini.

Pili, Rais Samia ameongeza idadi ya watumishi wa afya, ikiwa ni pamoja na madaktari, wauguzi, na wataalamu wa afya, jambo linalosaidia kupunguza uhaba wa wataalamu wa afya nchini.

Tatu, Ujenzi wa hospitali mpya za wilaya na za rufaa umeendelea, pamoja na vituo vya afya zaidi ya 300 vilivyojengwa tangu 2021.

Nne, vifaa tiba vya kisasa na mitambo imeendelea kununuliwa na kusambazwa hadi kwenye vituo vya afya.

### VIWANDA NA UWEKEZAJI

Rais Samia ameendelea kuhimiza uwekezaji katika sekta ya viwanda, kwa lengo la kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda ifikapo 2025. Serikali imeanzisha sera zinazovutia wawekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza katika sekta ya viwanda, hasa kwenye uzalishaji wa bidhaa za kilimo, nguo, na madini.

Serikali pia imeanzisha mkakati wa kuendeleza uchumi wa buluu (blue economy) kwa kuwekeza kwenye uvuvi, uchimbaji wa mafuta na gesi baharini, na utalii wa baharini.

### MABORESHO YA SERA ZA KIUCHUMI

Rais Samia amechukua hatua za kuimarisha mazingira ya biashara kwa kupunguza urasimu na kuongeza uwazi katika utoaji wa leseni za biashara. Serikali pia imekuwa ikifanya juhudi kubwa kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kushirikiana na sekta binafsi, na kuanzisha sera mpya za ushuru zinazolenga kuwasaidia wafanyabiashara wadogo na wa kati.

### UTALII

Utalii umeendelea kuwa sekta muhimu kwa uchumi wa Tanzania. Rais Samia alifanya juhudi kubwa kuvutia watalii kupitia filamu ya "The Royal Tour," ambayo iliitangaza Tanzania duniani kote kama kivutio cha utalii. Hii imechangia ongezeko la wageni na mapato yanayotokana na utalii, hasa baada ya kupungua kwa idadi ya watalii kipindi cha janga la Uviko-19.

### DIPLOMASIA YA UCHUMI

Rais Samia ameboresha mahusiano ya kimataifa, hasa kupitia diplomasia ya uchumi, ambayo imekuwa na matokeo chanya kwa kuvutia misaada, mikopo ya bei nafuu, na uwekezaji kutoka mataifa mbalimbali. Mahusiano mazuri na nchi kama Marekani, Uingereza, China, na nchi jirani yameimarisha biashara ya kimataifa na kuleta ushirikiano wa kiuchumi.

Kwa ujumla, serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imeonesha juhudi kubwa za kukuza uchumi kupitia uwekezaji katika miundombinu, kilimo, viwanda, na huduma za kijamii kama afya na elimu, huku ikihimiza maendeleo ya vijana na kuimarisha sera za biashara na uwekezaji.

### MAJIBU YA MALALAMIKO

Pamoja na hayo, kumekuwa na watu wakidai kwamba deni la taifa linaongezeka, kwamba maisha ni magumu, kwa nini tunaendelea kununua ndege, mara Rais anasafiri sana na mengine mfano wa hayo. Katika gazeti hili baadhi ya malalamiko hayo yamejibiwa na kimsingi kama utasoma makala hizo utajua umuhimu wake na kwamba hata maisha kwa sasa kwa ujumla si magumu kama wapinzani wa serikali wanavyotaka ieleweke.







Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alikagua gwaride la heshima baada ya kuwasili katika viwanja vya mapokezi ya viongozi vilivyopo kwenye majengo ya Union Buildings, Ikulu Afrika Kusini.

# Safari za nje za Rais Dk. Samia na faida lukuki

## ● Ukijifungia, maendeleo ya ndani yanadidimia pia


**Na Hamisi Kibari**

KATIKA dunia ya sasa, nchi zinashindana kibiashara na uzalishaji, lakini pia zinashirikiana katika mambo mbalimbali kama biashara, kupambana na ugaidi, mabadiliko ya tabianchi na kadhalika na kadhalika.

Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, alipata kusema kwamba huwezi kukaa ndani, ukajifungia bila kushirikiana na mtu nje halafu ukategemea maendeleo, badala yake hata maendeleo yako ya ndani na matarajio hayatatimia!

Makamba aliyasema hayo katika mkutano na waandishi wa habari kuelezea mafanikio ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini Korea Kusini aliyoifanya mwishoni mwa Mei, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Makamba, Tanzania inaheshimika sana huko nje kutokana na kuwa na misimamo katika masuala ya kimataifa, kutoa kauli za maendeleo yetu ya ndani na kuwa tayari kwa ushirikiano na wengine.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiwa katika mazungumzo ya faragha na mwenyeji wake, Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa.

Anasema ziara za Rais Dk. Samia nje, licha ya kwamba zinaenda na sera zetu za masuala ya nje kwa maana ya kushirikiana na mataifa ya nje katika kulinda uhuru wetu na kutafuta maendeleo zaidi, lakini pia zinaifungua Tanzania kwenye diplomasia ya uchumi.

Anasema sera mpya ya Tanzania ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001 inasema kwamba Tanzania itahusika kuchangamka kimataifa ili kutimiza malengo yetu ya kimaendeleo.

"Kuna dhana kwamba safari za nje hazina uhusiano na maendeleo yetu ya ndani. Si kweli. Safari hizi zina uhusiano mkubwa. Na nyinyi (waandishi wa habari) ni mashahidi.

Tulijaribu kujifungia milango na matokeo tunayajua, kwenye uwekezaji, kwenyebiashara na kwenye sifa na heshima ya Tanzania," anasema.

**KUVUTIA WAWEKEZAJI**

Safari za Rais zimeongeza juhudi za kuvutia uwekezaji kutoka nje, hasa kwa kuboreshamazingira ya biashara na ushirikiano wa kiuchumi.

Inaendelea uk. 8

# Safari za nje za Rais Dk. Samia na faida lukuki

Inatoka uk. 7

Kwa mfano, safari zake kwenda nchi za Ulaya, Mashariki ya Kati, na Marekani zimefanikisha mikataba na ahadi za uwekezaji katika sekta kama nishati, miundombinu, na kilimo. Baadhi ya mifano ya uwekezaji iliyotokana na safari hizi ni pamoja na:

**Mkataba wa Bandari ya Dar es Salaam (Dubai):**
Baada ya ziara ya Rais Samia katika nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Tanzania ilisaini mkataba na kampuni ya DP World kutoka Dubai kwa ajili ya kuboresha na kuendeleza Bandari ya Dar es Salaam. Uwekezaji huu unatarajiwa na tayari umeanza kuboresha miundombinu na ufanisi wa bandari hiyo, hivyo kuimarisha biashara ya kimataifa.

**Mikataba na sekta ya nishati (Ufaransa):**
Ziara ya Rais Samia nchini Ufaransa ilisababisha makubaliano katika sekta ya nishati, hususan nishati mbadala. Kampuni za Kifaransa zimeonesha nia ya kuwekeza katika miradi ya umeme wa jua na upepo nchini Tanzania.

**Miradi ya elimu na afya (Uingereza):**
Baada ya ziara ya Rais Samia nchini Uingereza, kumekuwa na ongezeko la ushirikiano katika sekta za afya na elimu, ambapo baadhi ya taasisi za Uingereza zimeahidi kuwekeza katika kuboresha huduma za afya na kutoa ufadhili wa masomo kwa Watanzania.

**Uwekezaji katika sekta ya kilimo (Uturuki):**
Ziara ya Rais Samia nchini Uturuki ilisababisha makubaliano kati ya Tanzania na Uturuki juu ya uwekezaji katika sekta ya kilimo. Serikali ya Uturuki imeahidi kuwekeza katika kuongeza thamani ya mazao ya kilimo kama kahawa, chai, korosho, na pamba. Pia, wameonesha nia ya kusaidia katika ujenzi wa viwanda vya usindikaji wa mazao.

**Mikataba ya madini na maliasili (Canada):**
Baada ya ziara yake nchini Canada, Tanzania imepata makubaliano mapya na kampuni za uchimbaji madini za Canada. Kampuni hizo zinawekeza katika uchimbaji wa madini adimu kama vile grafiti na cobalt, ambayo yanahitajika sana kwa ajili ya kutengeneza betri za magari ya umeme.

**Uwekezaji wa viwanda (Oman):**
Ziara ya Rais Samia nchini Oman imefungua milango kwa uwekezaji katika sekta ya viwanda.
Oman imeonesha nia ya kuwekeza katika viwanda vya kuchakata samaki na mazao ya baharini katika ukanda wa Pwani ya Tanzania, hasa Zanzibar. Hii itasaidia kuongeza ajira na uzalishaji wa ndani.

**Sekta ya teknolojia na mawasiliano (India):**
Ziara ya Rais Samia nchini India imesaidia kuvutia uwekezaji katika sekta ya teknolojia.
Kampuni za India zimeonesha nia ya kuwekeza katika kuanzisha vituo vya TEHAMA na kuboresha miundombinu ya mawasiliano nchini. Hii itawezesha ukuaji wa uchumi wa kidijitali na kuongeza fursa za ajira kwa vijana.

> "Ziara ya Rais Samia nchini India imesaidia kuvutia uwekezaji katika sekta ya teknolojia.

**MIKOPO NA MISAADA**
Rais Samia ameweza kushawishi mashirika ya kimataifa kama Benki ya Dunia na IMF kutoa mikopo yenye masharti nafuu pamoja na misaada ya maendeleo. Mbali na masharika hayo pia ameshawishi nchi marafiki kutapatia misaada au mikopo yenye masharti nafuu sana.
Kwa mfano, safari ya Rais Korea Kusini ambayo nitaitolea zaidi mifano katika makala haya, Tanzania ilipata mkopo wa Dola bilioni 2.5 (takriban shilingi trilioni 6.25) utakaolipwa kwa miaka 40 na riba yake ni asilimia 0.01. Ni mkopo utakaotolewa kwa muda wa miaka mitano na utaanza kulipwa baada ya miaka 25.
Tanzania imekuwa pia ikipata misaada inayoelekezwa katika miradi ya kijamii kama vile uboreshaji wa sekta ya afya na elimu, na ujenzi wa miundombinu muhimu.



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan, akiagana na Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi baada ya mapokezi katika Ikulu ya India Oktoba 9, 2023.**

**UIMARISHAJI WA DIPLOMASIA**
Rais Samia amerejesha ushirikiano wa kidiplomasia ulioimarishwa na mataifa mengine, jambo linalosaidia kuongeza ushawishi wa Tanzania katika masuala ya kikanda na kimataifa. Hii imejenga nafasi ya Tanzania kuwa na sauti kubwa kwenye masuala muhimu kama mabadiliko ya tabianchi na usalama wa kikanda.
Ni katika muktadha huu, Rais Sama alipokwenda China kuanzia Septemba 2 hadi 6, 2024 akiwa miongoni mwa wakuu wa nchi na serikali 53 walioshiriki kwenye Mkutano wa Tisa wa Wakuu wa Baraza la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC) ndiye aliyepewa nafasi kuzungumza akiwakilisha Ukanda wa Afrika Mashariki.

**KUIMARISHA SEKTA YA UTALII**
Kupitia kampeni kama "Royal Tour," Rais Samia ameongeza juhudi za kuitangaza Tanzania kama kituo cha utalii duniani. Hii imesaidia kuongeza idadi ya watalii, hali ambayo inachangia mapato makubwa kwa uchumi wa taifa.
Katika ziara yake Marekani, Rais Samia alifanikiwa kuvutia wawekezaji katika sekta ya utalii kupitia mpango wa kutangaza Tanzania kama kivutio kikuu cha utalii duniani.
Filamu ya The Royal Tour iliyoongozwa na Rais Samia ilisaidia kuongeza umaarufu wa vivutio vya Tanzania kama vile Serengeti na Zanzibar.
Baada ya filamu ya The Royal Tour na kuitangaza nje ya nchi, idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, mwaka 2022 Tanzania ilipokea zaidi ya watalii milioni 1.5, ikilinganishwa na watalii milioni 0.6 mwaka 2020, kipindi ambacho kilikuwa na athari pia janga la UVIKO-19.
Mwaka wa 2022, mapato ya utalii yalifikia zaidi ya dola bilioni 2.6, ongezeko kubwa kutoka dola bilioni 1.3 mwaka 2021. Ongezeko hili linahusishwa moja kwa moja na juhudi za Rais Samia katika kuutangaza utalii kupitia The Royal Tour.
Vivutio vya utalii kama Serengeti, Ngorongoro, Zanzibar, na Gombe ambako kuna sokwe vimepata umaarufu zaidi na watalii wameonyesha nia kubwa ya kutembelea maeneo haya. Hii imeonekana kwenye ongezeko la wageni katika hifadhi na mbuga za wanyama.
Haya yote, mbali na kuongeza uwekezaji, yamekuza ajira ajira katika sekta ya utalii. Watu wengi wamepata kazi kwenye hoteli, kama waongoza watalii na katika maeneo ya vivutio vya utalii.

**MFANO WA ZIARA YA INDIA**
Rais Samia ameshafanya ziara kadhaa nje ya nchi na kila moja imezaa au inatarajia kuzaa manufaa lukuki. Na haya manufaa si ya kutafuta kwa tochi bali yako wazi tu kama ambavyo nimegusia hapo juu. Hata hivyo, katika makala haya tutatoa mfano wa

Inaendelea uk. 9



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk.Samia Suluhu Hassan, akiwa kwenye picha ya pamoja na Rais wa Marekani, Joe Biden baada ya kuwasili katika Ikulu ya Marekani Washington D.C. Desemba 14, 2022. Kulia ni Jill Biden, mke wa Rais.**

# Safari za nje za Rais Dk. Samia na faida lukuki

Inatoka uk. 8

ziara mbili; ya India na ya Korea Kusini.

Aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba anasema kwamba ziara ya Rais Samia nchini India iliwanufaisha sana wakulima wa mbaazi.

January anafafanua kwamba India ni taifa ambao linatumia mbaazi kwa wingi na hivyo, ingawa nao wanalima zao hilo lakini ili kutosheleza mahitaji wanalazimika kuagiza pia nje.

Hata hivyo, anasema wanunuzi hao wakubwa wa mbaazi na wenye bei nzuri huwa wanatoa kiwango maalumu cha kila nchi kuingiza mbaazi nchini humo ambapo Tanzania ilikuwa imepangiwa kuingiza mzigo wa mbaazi usiozidi tani 50,000.

Anasema Rais Samia alipofanya ziara nchini India alifanikiwa kumshawishi kiongozi wa nchi hiyo, Waziri Mkuu Narendra Modi, tena nchi hiyo ikielekea kwenye uchaguzi hadi akaruhusu mbaazi za Tanzania tani laki mbili hadi tatu kuuzwa India.

Anasema hatua hiyo imesababisha wakulima wa mbaazi hususani kutoka mikoa ya Kusini kupata fedha zaidi na kuongeza mashamba zaidi ya zao hilo.

"Hii maana yake ni nini? Ni kwamba mazungumzo ya Rais na viongozi wenzake au na wakuu wa taasisi huko nje, yanakuwa na ushawishi mkubwa kwa ajili ya manufaa kwa Watanzania... Ninayo mifano mingi ya faida ya safari za Rais nje kwa Watanzania wengi lakini leo ninawapa huo mmoja," anasema.

### MANUFAA ZIARA YA KOREA

Aliyekuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji anasema ziara ya Rais Samia Korea Kusini imekuwa sababu ya kuanzisha majadiliano ya ushirikiano wa kiuchumi (Economic Partnerdhip Agreement - EPA) baina ya Tanzania na Korea. Ziara hiyo ya siku sita ilianza Mei 30, mwaka huu.

Dk. Kijaji ambaye kwa sasa ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) anasema majadiliano hayo yanatarajiwa kuwa na manufaa mengi kwa Tanzania, moja wapo ikiwa ni kuboresha bidhaa zinazozalishwa nchini kufikia viwango vya kimataifa.

Anasema moja ya mambo ambayo Watanzania watunufaika na ushirikiano huo ni kuboresha bidhaa zitakazokuwa zinazalishwa nchini kufikia viwango vya kimataifa kama ilivyo kwa nchi hiyo na hivyo kuviuza mahala popote duniani.

Faida nyingine anasema kwamba kuna bidhaa zimekuwa zikizalishwa nchini lakini inakuwa ni vigumu kueleza uasili wake kuwa ni za Tanzania kwa asilimia ngapi, hivyo kwa ushirikiano huo tatizo hilo linakwenda kutatuliwa.

Amesema faida nyingine inayotarajiwa kupatikana kutokana na ushirikiano huo ni suala la uendelevu wa biashara (continuity), akifafanua kwamba huwa inatokea Tanzania inapeleka bidhaa nje, tuseme tumbaku lakini ikishapeleka mara moja inashindwa kuwa na uendelevu licha ya bidhaa kuhitajika sokoni. Sasa Waziri Kijaji anasema kwa ushirikiano huo, tatizo hilo pia litapatiwa ufumbuzi kutokana na uwekezaji utakaofanyika.

Anasema ana uhakika kwamba kutokana na ushirikiano huo, kile kilichofanyika nchini ndani ya miaka 50 au zaidi kitaongezeka takribani mara tano mpaka 10 ndani ya miaka isiyozidi 10 tu.

### BASHARA YA TANZANIA NA KOREA KUONGEZEKA MARADUFU

Kutokana na ziara aliyoifanya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan nchini Korea Kusini, uwekazaji kutoka nchini humo na biashara kati ya Tanzania na Korea vinatarajiwa kuongezeka maradufu katika kipindi kifupi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo ambaye pia alikuwepo kwenye ziara hiyo anasema kwamba uwekezaji unaokaribishwa kwa sehemu kubwa utajielekeza katika kilimo na madini, hususani madini ya kimkakati.

Anafafanua kwamba mbali na kusaidia katika utafiti, uwekezaji kutoka Korea utajikita katika kuzalisha bidhaa za kilimo na madini hapahapa Tanzania na si kusafirisha nje mali ghafi.

Anasema Tanzania ni kati ya nchi chache zenye madini mengi ya kimkakati lakini wawekezaji waliokarinishwa nchini kutoka Korea Kusini watatusaidia kujua kiasi cha madini hayo kilichopo na pia ubora wake.

"Kwa miaka 50, tuliwakaribisha wakavuna madini na kuuza nje, sasa tunataka waje kuvuna na ku-process (kuchakata kwa kuyabadili kuwa bidhaa) hapahapa. Hiyo pia ni njia moja wapo ya kulinda ajira za Watanzania (badala ya kuzipeleka nje unapouza madini ghafi)," anasema.

Anasema umri wa Korea Kusini ni sawa na Tanzania na kwamba walianza maendeleo yao kwa kufanya mapinduzi katika kilimo, kisha wakafanya mapinduzi ya viwanda na sasa wako kwenye mapinduzi ya teknolojia.

Anasema Wakorea wamefika hatua ya sasa ambayo wametuacha mbali kimaendeleo kwa bidii zao wenyewe na uwekezaji kutoka Marekani. Anasema wamekuwa wakiwekeza na kufanya biashara na nchi za Bara Asia na sasa kupitia ziara ya Rais wamethibirisha kugeukia kufanya biashara kubwa na Tanzania.

### WATENGENEZA FILAMU WAMSHUKURU SAMIA SAFARI YA KOREA

Kuna wale ambao wamekuwa wakihoji kwamba kwa nini msafara wa Rais nje unakuwa na watu wengi. Katika kuwasaidia uelewa ni kwamba ziara hizi zimekuwa ni za kimkakati zaidi na hivyo kila unayemwona kwenye msafara wa Rais ana sababu maalumu na muhimu kwake na kwa taifa. Si safari za kwenda kula bata bali kuleta kitu nchini.

Katika safari ya Korea Rais alikuwa na watu wa startups, yaani kampuni zinazonzishwa kwa lengo la kuleta bidhaa au huduma mpya kwenye soko kwa kutumia teknolojia (Tehama) au ubunifu wa kipekee pamoja na wasanii wa filamu.

Malengo yalikuwa kujifunza kwa wenzao waliopiga hatua kubwa zaidi (best practice) ili na wao wapanue shughuli zao kama si kupanuka kimawazo.

Ni kutokana na hatua hiyo, wasanii, watayarishaji na watengeneza filamu wa Tanzania, wanamshukuru Rais kwa kuwakutanisha na wenzao wa Korea Kusini, hatua ambayo wanasema inakwenda kuboresha filamu za Tanzania.

Mmoja wa watayarishaji wa filamu nchini aliyekuwepo kwenye ziara hiyo, Leah Mwendamseke "Lamata", akizungumza kwa niaa ya wenzake anasema kupitia ziara hiyo wenzao wa Korea wamekubali kushirikiana na watayarishaji wa filamu wa Tanzania katika kutengeneza filamu na tamthilia zenye hadhi ya kimataifa.

"Tumepata connections na wamekubali kushirikiana na sisi. Tuna matumaini makubwa kwamba sanaa yetu inaenda kubadilika. Kwa kweli tunamshukuru sana Rais," anasema

Lamata ambaye aliandamana na msanii Elizabeth Michael "Lulu" kwenye ziara hiyo.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dkt. Saada Mkuya Salum anasema Rais Samia anaona mbali kwani nchini India, tasnia ya filamu (Bollywood), mbali na kutoa ajira kwa vijana inachangia pakubwa katika uchumi wa nchi hiyo.

Anasema hata Nigeria (Norwood) filamu zimekuwa zikitoa mchango mkubwa katika uchumi wa nchi hiyo pamoja na ajira sambamba na nchi ya Afrika Kusini. Kwa hiyo matarajio ni kwamba Wakorea watatusaidia katika kuboresha tasnia ya filamu kwa kulenga Soko la kimataifa.

Nihitumishe kwa kusema kwamba kutokana na manufaa ya ziara za Rais Samia nje, unaweza kutamani awe anatoka kila mara ili kuifungua nchi kuliko kujifungia. Na kwa hakika, kama anavyosema January Makamba, ukijifungia ndani, hata maendeleo yako ya ndani uliofikia, yanadidimia pia.



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na viongozi mbalimbali baada ya kuwasili katika uwanja wa ndege wa Jeshi wa Seoul, kwenye ziara rasmi ya kikazi katika nchi ya Jamhuri ya Korea Mei 31, mwaka huu.**



# Sekta ya bima na ukuaji wa uchumi, uimarishaji afya nchini Tanzania

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na kupelekea mafanikio makubwa ambayo yamepatikana na yanaendelea kupatikana katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi madhubuti wa **Mhe. Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.**

TIRA chini ya Uongozi wa Kamishna wa Bima, Dkt. Baghayo Saqware imeweka mazingira yatakayowawezesha kutekeleza majukumu yake kwa urahisi ikiwa ni pamoja na kuzisogeza huduma kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mamlaka hii ina ofisi tatu ambazo ni **Makao Makuu Dodoma**, **Ofisi ya Zanzibar** pamoja na **Ofisi ya Dar es Salaam**. Aidha kuna ofisi za kanda ambazo zipo 10.

Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inahudumia mikoa ya Songwe, Mbeya na Njombe wakati Kanda ya Kaskazini inahudumia mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga huku Kanda ya Ziwa ikihudumia mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Simiyu na Mara.

Kwa upande wa Kanda ya Mashariki, mikoa inayohudumiwa ni Dar es Salaam, Pwani na Morogoro; Kanda ya Kati inahusisha mikoa ya Dodoma, Iringa na Manyara wakati Kanda ya Magharibi inahudumia mikoa ya Tabora, Shinyanga na Singida.

Lakini pia kuna Kanda ya Kusini yenye mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma; Kanda ya Ziwa Tanganyika inayohudumia mikoa ya Katavi, Kigoma na Rukwa; Kanda ya Unguja inayohudumia mikoa ya Unguja, Kaskazini Unguja pamoja na Mjini Magharibi; na Kanda ya Pemba inahudumia Mkoa wa Pemba.

## UMUHIMU WA BIMA KULINDA UWEKEZAJI, AFYA

Kama tutakavyoona katika makala haya, kuna bima za aina nyingi. Mfano wa bima hizo ni bima ya afya, bima ya vyombo vya moto, bima za biashara, kilimo, elimu, safari pamoja na bima za miradi mbalimbali.

Bima ni njia ya ulinzi wa kiuchumi dhidi ya hasara mbalimbali ambazo kwa namna moja au nyingine huathiri uchumi wa mhusika na pia ni ulinzi mzuri kwa afya kwa kuwa magonjwa huja ghafla wakati mwingine ukiwa huna pesa.

Mtu hulipa kiasi kidogo cha pesa kwa mwaka kwenye Kampuni ya Bima kama ada ya bima (premium) kulingana na mkataba wa bima ili kumwezesha kunufaika na Bima pindi atakapokuwa amepata majanga au ugonjwa.

Bima inaendelea kuwa na mafanikio makubwa ikiwa ni pmoja na kuwa nguzo muhimu katika kuchagiza ukuaji wa uchumi nchini.

## BIMA YA AFYA KWA WOTE

Bima ya afya kama ilivyo bima za vyombo vya moto ni moja ya bima zilizojipatia umaarufu mkubwa nchini. Kwa kutambua umuhimu wa Bima ya Afya, hivi karibuni serikali ilipitisha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote (UHI) namba 13 ya mwaka 2023 ambayo imeanza kutumika rasmi Agosti 16, 2024 ambayo itahakikisha Watanzania wote wanapata huduma bora na kuimarisha afya zao ikiwa ni pamoja na kuwapunguzia mzigo wa gharama za matibabu.

Ni mpango unaolenga kuleta usawa katika upatikanaji wa huduma za afya, kuzuia wananchi kushindwa kumudu gharama za matibabu na kuboresha afya ya umma kwa ujumla.

Kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, sheria inatoa haki ya msingi kwa kila Mtanzania kuwa na bima ya afya na kwamba inahusisha raia wote wa Tanzania na wageni wanaoishi nchini bila kujali wanatoka sekta rasmi au siyo rasmi.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 7(2), TIRA imepewa mamlaka ya kuhakikisha kuwa watoa huduma wa bima ya afya wanatoa huduma bora na za haki kwa wananchi waliopo kwenye skimu zao.

Sheria hii imeambatana na kanuni za bima ya afya kwa wote za mwaka 2024 ambazo zimeelekeza namna skimu za bima zinavyopaswa kutekelezwa, lakini pia kwa mujibu wa kanuni za bima ya afya kwa wote, skimu zote za bima zinatakiwa kufuata utaratibu ili kuhakikisha utekelezaji wake unafanikiwa.

Bima ya afya ina manufaa makubwa baadhi ya hayo ni **kupunguza mzigo wa gharama za matibabu** kwa maana kwamba bima ya afya inalinda watu dhidi ya gharama kubwa za matibabu, hasa kwa magonjwa yasiyotegemewa, inawawezesha watu kupata huduma bora za afya kwa wakati bila kulazimika kulipa papo hapo na pia inasaidia kuepuka kutumia akiba binafsi au mali kwa ajili ya matibabu ghafla.

**Bima ya afya pia inasaidia uboreshaji wa afya ya jamii** kwa maana kwamba inachangia kuboresha afya ya umma kwa kuruhusu upatikanaji wa huduma za kinga, matibabu, na ufuatiliaji wa magonjwa na pia ina**hamasisha** watu kutafuta matibabu mapema kabla hali



**Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), imeshiriki katika uzinduzi wa zoezi la uandikishaji wa Bima za Mufti elfu moja katika wilaya ya Korogwe mkoani Tanga.**

kuwa mbaya.

**MAFANIKIO YALIYOFIKIWA**

Miongoni mwa mafanikio mengi yaliyopatikana ni pamoja na Maendeleo ya Teknolojia, Uelimishaji wa Bima kwa Watanzania, uwekezaji wa kuvutia, mafanikio ya kampuni za Bima pamoja na ulipwaji wa fidia kwa waathirika wa majanga.

**BIMA YA TAKAFUL**

Mwaka 2022 ilizinduliwa bima mpya ya **TAKAFUL** inayofuata misingi ya Dini ya Kiislamu ili kuifikia jamii pana ambayo hapo awali haikuguswa. Takaful inafuata sheria za Kiislamu (Shariah), na hivyo kuepuka mambo yanayokatazwa katika dini hiyo kama vile riba (faida za ziada), gharar (kutokujulikana kwa hali) na kamari. Pia, faida zinazopatikana kutoka kwa uwekezaji wa fedha za Takaful zinagawanywa miongoni mwa washiriki kulingana na mikataba ya awali.

**KUJIWEKEA ULINZI**

Kama ilivyogusiwa hapo awali, kukata bima ni kujiwekea ulinzi ili iwapo janga litatokea kama vile ajali, uharibifu wa mazao, majengo, vyombo vya moto au mradi kukwama na kwenda nje na mpangilio wake, bima italipa fidia ili kupunguza athari za kiuchumi na athari nyingine kadiri ya makubaliano ya kampuni ya bima na mteja wake na hivyo kusaidia kuepuka anguko la kiuchumi.

Katika kuhakikisha wananchi wanaepukana na hasara zinazoweza kutokana na majanga ya ajali au miradi kukwama, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima imekuwa ikitoa elimu ya bima kwa wananchi katika nyanja mbalimbali kulingana na mahitaji ili kuhakikisha wanapata uelewa kuhusu masuala ya bima pamoja na haki zao za kibima.

Hiyo imechangia Uchumi wa Tanzania kuendelea kukua kwa kasi hasa katika kipindi hiki cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ya **Mhe. Rais Dk. Samia Suluhu Hassan**.

Pamoja na sekta nyingine, pia sekta ya Bima imekuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi, na hii imetokana na sera nzuri za bima na usimamizi mzuri wa Mamlaka ya Bima Tanzania (TIRA) chini ya Uongozi wa **Dk. Saqware na Naibu wake, Khadija I. Said** ambaye anasimamia upande wa Zanzibar.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Fedha, ifikapo mwaka 2030 imejiwekea lengo la kufikia asilimia 50% ya watumiaji wa bima nchini huku ikijiwekea lengo la kuhakikisha asilimia 80% ya jamii nzima ya Tanzania inapata elimu ya bima.

Aidha, serikali imeweka mikakati mbalimbali ili kuvutia wawekezaji, kuimarisha mazingira ya biashara na kutoa motisha ambavyo vimesaidia kufungua milango ya fursa mpya za uwekezaji katika sekta ya bima.

Kupitia mikakati hiyo katika kukuza uwekezaji katika sekta ya bima Tanzania, hivi sasa Mamlaka ina wasajiliwa wa bima zaidi ya **1,650** zikiwemo kampuni za bima, mawakala, mabrokers, wakadiria hasara na wengineo wanaotoa huduma za bima nchi nzima huku asilimi 18% ya Watanzania wote wakiwa ni watumiaji wa huduma za bima mbalimbali.

Kulingana na maelekezo ya Serikali, Sekta ya Bima inaendelea kuweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha wigo wa usambazaji wa bidhaa za bima unatanuka na hatimae wananchi waweze kupata huduma za bima kwa urahisi zaidi popote walipo.

Pia serikali imeweka mazingira mazuri ya biashara, maboresho ya Sheria na hatua za kuhamasisha uwekezaji ambazo zimekuwa kichocheo katika kuvutia wawekezaji wa kigeni lakini pia kufuta baadhi ya masharti ya usajili kwa mawakala wa bima kikiwemo kigezo cha mtaji ili kuongeza wigo wa watoa huduma za bima kote nchini.

**UTULIVU WA KIUCHUMI:** Sekta ya bima imekuwa muhimu katika kudumisha utulivu wa uchumi kwa kutoa fidia ya kifedha na suluhisho la usimamizi wa vihatarishi. Hii imewasaidia wafanyabiashara na watu binafsi kupunguza hasara wakati wa kushuka kwa uchumi.

**UKUAJI WA MALIPO YA BIMA:** Katika sekta hii ukuaji wa malipo ya bima uliongezeka kwa asilimia 25% kutoka shilingi bilioni 911.5 mwaka 2021 hadi shilingi bilioni 1,138 mwaka 2022. Ukuaji huu uliendelea hadi mwaka 2023, hii ikionyesha uimara wa sekta na uwezo wake wa kuvutia wateja zaidi.

**MCHANGO WA PATO LA TAIFA (GDP):** Mwaka 2022, sekta ya bima ilichangia shilingi bilioni 5,720.8 kwa pato la taifa la Tanzania, ikiwakilisha asilimia 3.6% ya jumla ya GDP. Hii ilikuwa ni ongezeko la kutoka shilingi bilioni 5,259.8 mwaka 2021.

**UWIANO WA UPENYEZAJI:** Uwiano wa upenyezaji wa soko la bima uliongezeka kutoka asilimia 1.68% mwaka 2021 hadi asilimia 1.99% mwaka 2022. Hii inaonesha ongezeko la uelewa na matumizi ya bidhaa za bima miongoni mwa Watanzania.

**MSAADA KWA MIKAKATI YA KITAIFA:** Ukuaji wa sekta hii umeungwa mkono na mikakati ya kiuchumi ya kitaifa kama vile Dira ya Maendeleo ya 2025 na Mfumo wa Kitaifa wa Ujumuishaji wa Kifedha III. Mipango hii imeunda mazingira mazuri kwa sekta ya bima kustawi.

**UREJESHAJI BAADA YA JANGA LA KORONA**: Sekta ya bima pia iliunga mkono urejeshaji baada ya janga la korona kwa kutoa bima kwa sekta kama vile usafiri, utalii, na malazi, ambazo ziliathirika sana na janga hilo.

**MAENDELEO YA TEKNOLOJIA:** Serikali ya Awamu ya Sita kupitia TIRA imefanikiwa kuleta mabadiliko ya teknolojia ambayo yamelenga kuimarisha usimamizi na usalama wa soko la bima kwa kuboresha mifumo ya kidijitali na halikadhalika Mamlaka imeboresha mfumo wa TIRA-MIS ambao unatumika kuhakiki bima mbalimbali.

Maboresho hayo yameleta mabadiliko kwa kuimarisha uhalali wa bima zinazotolewa na kupunguza kwa kiasi kikubwa vitendo vya udanganyifu kwenye bima.

Vilevile Serikali imerahisisha mifumo ya usajili wa watoa huduma za bima kwa kuanzisha mfumo wa usajili mtandaoni unaopatikana kupitia tovuti ya Mamlaka yenye anuani **ors.tira.go.tz**. Aidha, kupitia mfumo huu Serikali ya Awamu ya Sita imewarahisishia njia ambayo wananchi na wawekezaji wanaweza kufanya usajili wa biashara za bima kwa urahisi zaidi.

Takwimu hizi zinaonesha muamko wa wananchi katika kujilinda na athari za majanga mbalimbali kupitia bima na vilevile mchango wa bima katika kuwanusuru watanzania kuondokana na umasikini na kupelekea mustakabali mzuri wa kifedha.

**HITIMISHO:**

Sekta ya Bima nchini inaendelea kukua. Mafanikio, ukuaji wa uchumi, na mabadiliko chanya yanaendelea kuiweka Tanzania katika ramani ya kimataifa. Fursa za kipekee, mazingira bora ya biashara, na mikakati madhubuti inayoendelea kuwekwa inaonesha jinsi Tanzania inavyoendelea kuwa kitovu cha uwekezaji wa kimataifa ikiwemo uwekezaji katika sekta ya bima.

Pia, mchango wa sekta ya bima umekuwa muhimu katika kupunguza athari za mgogoro wa kifedha na kusaidia urejeshaji wa uchumi nchini. Ukuaji na maendeleo endelevu ya sekta hii ni muhimu kwa utulivu na uimara wa kifedha wa nchi. Ikumbukwe kuwa kama Taifa kupitia Wizara ya fedha imejiwekea malengo ya kutoa na kufikisha elimu ya bima kwa asilimia 80% ya wananchi wa Tanzania na kufikia lengo la watumiaji asilimia 50% wa huduma za bima ifikapo 2030.

# TASAF inavyoinua hali ya maisha ya Watanzania wenye hali duni





**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF), umepiga hatua kubwa kwa kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika kuwainua Watanzania maskini kiuchumi.

Juni, mwaka 1999, serikali ilizindua Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, ikiwa na dhima kuu ya kupunguza walau nusu ya watu wanaoishi kwenye umaskini na kuwafanya waishi katika uchumi wa kati kufikia mwaka 2025.

Katika kufanikisha hilo, serikali ilikuja na mikakati mbalimbali, mojawapo ni Mpango wa TASAF wa mwaka 2000.

Ikiwa umesalia mwaka mmoja pekee wa utekelezaji wa dira hii, Serikali ya Rais Dk. Samia, imepiga hatua kubwa katika kuwaondoa maelfu ya Watanzania kwenye umasikini uliokithiri.

Utekelezaji wa Mpango wa TASAF umefikia awamu kuu ya tatu, awamu ya pili ndogo, maarufu kama TASAF-3 PSSN-II iliyoanza utekelezaji wake Februari, 2020 ikienda hadi Septemba, mwaka huu (2024).

Wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia alipoingia madarakani Machi, 2021, utekelezaji wa awamu hii ya tatu ulikuwa umefikia kaya 877,352 zenye jumla ya wanufaika 3,322,627.

Itakumbukwa kuwa awamu ya kwanza na ya pili za TASAF, zilihusu kujenga miundombinu muhimu ya huduma za jamii kama elimu na afya, ikitekelezwa kati ya mwaka 2000 hadi 2012.

Shughuli kama mpango wa Ruzuku ya Kujikimu Kimaisha (Livelihoods and Productive Grants-LPG) kwa kaya maskini na miradi midogo midogo ya Kazi za Umma (PWP), ilianzishwa katika awamu ya PSSN-I iliyotekelezwa kati ya mwaka 2012 hadi 2019.

Shedrack Mziray, Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF anasema tangu mwaka 2014, Mfuko ulianza rasmi kutoa ruzuku hizo mbili baada ya miaka miwili ya maandalizi na tathmini iliyoanza mwaka 2012.

Hadi kufikia Machi, 2021, jumla ya kaya 877,352 zenye wanufaika 3,322,627, zilikuwa zimefikiwa na Mpango wa Ruzuku ya Kujikimu Kimaisha ambapo jumla ya Shilingi 172,137,398,200 zilikuwa zimetolewa.

Kwa upande mwingine, jumla ya shilingi 264,069,017,000 zilikuwa zimelipwa kwa wanufaika wa miradi midogo midogo ya Kazi za Umma (PWP).

Mziray anasema baada ya kuchukua hatamu, Rais Dk. Samia aliweka mkazo katika kuwainua Watanzania kiuchumi kuanzia ngazi ya kaya. Kwa kuendelea kutekeleza bajeti ya Dola za Marekani milioni 883.3, wadau wa maendeleo pia wameendelea kuchangia katika kuongezeka kwa bajeti hii.

Kuongezeka kwa bajeti hiyo kumechechemua shughuli za mfuko ambapo kati ya Septemba, 2021 na Septemba, 2024, jumla ya kaya 1,371,038 zenye wanufaika 5,202,655, zimefikiwa na Mpango wa TASAF.

Mziray anasema kati ya fedha hizo zilizotolewa, shilingi 984,131,701,084 zimelipwa kupitia Ruzuku ya Kujikimu Kimaisha (LPG) na Shilingi 213,840,759,300, zililipwa kupitia Mpango wa Kazi za Umma (PWP).

Anasema mafanikio haya yanatokana na dhamira ya dhati ya Rais Dk. Samia ya kumwinua kiuchumi Mtanzania wa hali ya chini.

Kufanikisha dhamira hii, chini ya Serikali yake ya Awamu ya Sita, Rais Dk. Samia iliahidi na imeendelea kuwahudumia wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya za walengwa unaotekelezwa na TASAF katika Tanzania Bara na Zanzibar.

Anasema kuwa katika kipindi cha miaka sita kati ya mwaka 2014 hadi 2020 kabla ya Rais Dk. Samia hajaunda serikali yake, ni kaya 158,262 pekee zilikuwa zimefikia hadhi ya kuondolewa katika mpango wa kaya masikini zikiwa na wanufaika 601,396.

Mziray anabainisha kuwa idadi hii inaonesha kuwa kumekuwepo na ongezeko kubwa la kaya ambazo zimefikia hadhi ya kuondoka katika mpango huo ndani ya kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Ongezeko la kaya zinazoondoka kwenye mpango huu katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, ni sawa na asilimia 29 ya jumla ya kaya zote 400,000 ambazo zimeondolewa katika mpango wa kaya masikini hadi kufikia Septemba 2024.

"Haya ni matunda ya uthubutu wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika jitihada za serikali yake kuwainua Watanzania kiuchumi," anasema Mziray.

Akizungumzia mafanikio ya mpango huo tangu kuanza kutolewa ruzuku mwaka 2024, anasema kuwa jumla ya fedha za ruzuku zilizotolewa kwa kaya 83,666 ni Shilingi bilioni 17.1 ambapo kwa awamu ya kwanza ilikuwa na kaya 77,972 zilizonufaika zikipata jumla ya Shilingi bilioni 13.9.

Kiwango cha juu cha ruzuku kwa kila kaya inayonufaika ni shilingi 350,000 ambayo imekuwa msaada kwa wajane, vijana na watu wenye ulemavu kuanzisha shughuli za kujiingizia kipato ikiwemo biashara ndogondogo.

## WANUFAIKA WA RUZUKU WANENA

Shufaa Mfinanga, mfanyabiashara wa duka la reja reja na mkazi wa Mtaa wa Kalemani, Kata ya Kaloleni, Manispaa ya Moshi, ni miongoni mwa wanufaika wa ruzuku.

Amewekeza kwenye biashara ya mgahawa kutokana na kupewa ruzuku ya Shilingi 350,000.

Mama wa watoto wanne ambao wawili kati yao wanafaidika na ruzuku ya TASAF, anaishi maisha ya furaha kwa kujipatia kipato kutokana na biashara aliyoianzisha kwa fedha za ruzuku.

"Nimefanikiwa kupanua uwekezaji wangu wa biashara hadi duka la vinywaji baridi. Ninavyozungumza mtaji wa biashara umekua hadi Shilingi milioni," anasema.

Hamad Masumbuko, mnufaika mwingine na mkazi wa Mtaa wa Kalemani Kata ya Kaloleni Manispaa ya Moshi, anamiliki duka la rejareja la mitungi ya gesi alilolianzisha kutokana na ruzuku ya TASAF.

Alianza biashara hiyo Septemba, mwaka jana akiwa na mitungi minane ambayo imeongezeka na kufikia mitungi 20.

Masumbuko anayeishi na ulemavu, anasema kuwa ruzuku imemsaidia kukuza biashara ambayo anapata wastani wa faida ya





**Bi Christina Kunamila Chumba mkazi wa Kijiji cha Chang'ombe Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, akiwa na mume wake pamoja na baadhi ya mifugo yake aliyoipata baada ya kuingia kwenye mpango wa tasaf na kuanza kuwekeza sehemu ya ruzuku anayopokea ili kuwa na kipato endelevu.**



shilingi 58,000 kwa mwezi.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Mziray, anasema jumla ya vikundi vya akiba vya wanufaika 60,327 vyenye wanachama 838,241, vimeundwa na kupatiwa mafunzo.

Anasema akiba katika vikundi hivi sasa ni shilingi bilioni 7.9.

Kati ya akiba hizo, shilingi bilioni 3.2 zilitolewa kama mikopo kwa wanachama kwa ajili ya kuwekeza kwenye shughuli zao za kuwaingizia kipato tangu mwaka 2019.

"Hadi Juni 2024, jumla ya wanufaika wa moja kwa moja 5,195,605, wamejiandikisha katika mpango huo, ambapo asilimia 55.7 ni wanawake na asilimia 44.3 wanaume," anafafanua Mziray.

## UFADHILI SEKTA YA ELIMU

Wanafunzi wanaotoka kwenye kaya maskini nchini zaidi ya milioni mbili ni miongoni mwa wanufaika wa TASAF.

Wanafunzi hao wanapofika vyuo vikuu, hupata mkopo kwa asilimia 100 ili kuwawezesha kukamilisha masomo yao kutokana na familia zao kutokuwa na uwezo wa kutoa nyongeza.

Mziray anasema kuwa kati ya wanufaika wote milioni 5.19, wanafunzi pekee ni milioni 2.13 ambao ni sawa na asilimia 41.

Mziray anasema kati ya wanafunzi 2,139,500 waliohudumiwa kwa mpango huu, wanafunzi wa kike walikuwa 1,074,445 na wa kiume ni 10,65,055 ambao wote wana umri wa kati ya miaka sita na 18.

Anasema mradi huo umetekelezwa katika halmashauri 186 nchini ambapo pia wanawake ndiyo wanufaikaji wakuu zaidi ya wanaume.

Kati ya idadi hiyo ya wanufaika, wanawake ni 2,892,643 sawa na asilimia 55.7 na wanaume ni 2,302,962 ambao ni sawa na asilimia 44.3.

# Rais Samia anavyosimamia

## Mingi imeanza kutoa matokeo chanya na takwimu hazidanganyi

**Na Hamid Yassin**

MIRADI yote mikubwa ya kimkakati iliyoanzishwa au kuendelezwa kuanzia Serikali za Awamu ya Nne na ya Tano, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan naye pia anaiendeleza kwa kasi nzuri huku wahafidhina wengi wakiwa hawaamini macho yao!

**UJENZI WA SGR**

Hayati Rais Dk. John Pombe Magufuli, aliacha ujenzi wa reli ya kisasa ya mwendo kasi (SGR), ukiwa chini ya asilimia 80, kati ya Dar es Salaam na Morogoro. Lakini sasa kipande hicho, chini ya Rais Dk. Samia, kimekamilika na tayari safari kati ya Dar, Moro hadi Dodoma, zimeanza kwa kishindo na ufanisi mkubwa!

Ile falsafa yake ya 'Kazi iendelee', akimaanisha kuendeleza yote mazuri ya mtangulizi wake na mengine mapya, haikuwa ya kinafiki; kwani sasa vipande vyote vilivyobaki vya mradi huo, vimeshasainiwa na hivi sasa wakandarasi wako maeneo ya kazi wakiwajibika.

Wakati wa utiaji saini wa ujenzi wa kipande cha SGR Tabora-Kigoma, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa anasema ujenzi wa SGR katika vipande vyote unaendelea vizuri.

Mbali ya ujenzi wa Dar es Salaam hadi Dodoma kukamilika, Kadogosa amebainisha kuwa, Serikali ya Rais Dk. Samia imefanikiwa kuendeleza ujenzi huo katika maeneo mengine ya reli hiyo ya mwendokasi.

Ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR kwenye vipande vya Makutupora-Tabora na Tabora-Mwanza unaendelea kwa kasi. Kwa kipande cha Makutupora-Tabora chenye urefu wa kilomita 368, kazi imekamilika kwa asilimia 13.86 kufikia Aprili 2024. Kwa upande wa kipande cha Tabora- Mwanza kupitia Isaka, ujenzi unaendelea na umekamilika kwa takriban asilimia 52.69 (kwa mujibu wa gazeti la Mwananchi).

Kwa mujiu wa gazeti la The Citizen, kipande cha Makutupora hadi Tabora, kinatarajiwa kukamilika Januari, 2026, huku vipande vingine vikitarajiwa kuanza kufanya kazi ndani ya miaka machache ijayo.

Mradi huu wa SGR ni muhimu kwa uchumi wa Tanzania kwani unalenga kuimarisha usafirishaji wa mizigo na abiria kutoka bandari za Dar es Salaam hadi mikoa ya Kati na Magharibi, pamoja na kuunganisha nchi jirani kama Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokraisa na Congo (DRC).

**MRADI WA JNHPP**

Huu ni mradi mwingine wa kimkakati wa ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme Julius Nyerere (JNHPP) kutumia maji ya maji Mto Rufiji. Wakati anazindua ujazaji maji wa bwawa hilo Desemba 22, 2023, Rais Dk. Samia alisema alikuta ujenzi wa mradi huo ukiwa asilimia 37 wakati ainingia madarakani, lakini mpaka siku ile ya ujazaji maji, ujenzi wake ulikuwa umefikia asilimia 78.68.

Hivi niandikapo makala haya, tayari vinu vitatu kati ya tisa, vimeshaanza uzalishaji wa umeme wa megawati 705 ambapo lile jinamizi la kukatika kwa umeme mara kwa mara kutokana na uchache wa umeme unaozalishwa, sasa limepungua kwa zaidi ya asilimia 90 kwa mikoa yote nchini inayotumia umeme wa Gridi ya Taifa.

Mara nyingi umeme unaweza kukatika kwa sababu za kiufundi.

Miradi mingine ya kimkakati inayoendelea kwa kasi ya kimbunga, ni pamoja na ujenzi wa Daraja refu la Magufuli (Kigongo-Busisi) katika Ziwa Victoria ambapo sasa umefika asilimia 98 ya ujenzi.

**ROYAL TOUR**

Royal Tour ilikuwa fursa ya kimkakati ya kuitambulisha Tanzania kimataifa, kuvutia uwekezaji nchini na kutangaza utalii ambapo katika kipindi hiki cha miaka yake mitatu na nusu, Dk. Samia amefanikiwa kushawishi watalii mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kutembelea mbuga zetu na vivutio vingine vya kitalii.

Wawekezaji na mawakala wa utalii zaidi ya 30 kutoka katika nchi za Marekani, Ufaransa na Lithuania, walitembelee Tanzania ili kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii kwa lengo la kuvitangaza katika nchi hizo.

Kutokana na juhudi hizo, hadi kufikia mwaka 2022, idadi ya watalii walioitembelea Tanzania iliongezeka kwa asilimia 57.7 kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 1,454,920 mwaka 2022.

Watalii hao wameongozwa na mataifa ya Marekani, Ufaransa, Ujerumani, Uingereza, Poland, Italia, India, Uholanzi, Hispania na Jamhuri ya Czech.

Kwa upande wa nchi za Afrika, watalii wengi wametoka Kenya, Burundi, Zambia, Malawi, Rwanda, Afrika Kusini, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Zimbabwe na Msumbiji.

Pamoja na ongezeko la idadi ya watalii wa Kimataifa, utalii wa ndani pia umeendelea kuimarika nchini ambapo katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2022, idadi ya watalii wa ndani waliotembelea maeneo ya hifadhi imeongezeka kwa asilimia 199.6 kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 2,363,260 mwaka 2023.

Aidha, sambamba na ongezeko hilo sekta ya utalii nchini imefanikiwa kupata tuzo mbalimbali za kimataifa zikiwemo za Tanzania kuwa kituo bora cha utalii Afrika (Safari Bookings.com), Tanzania kuwa kituo bora cha kutembelea Barani Afrika (New York Times) na Ngorongoro imetajwa kuwa ni eneo bora duniani na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti imetajwa kuwa hifadhi bora katika Afrika.

Aidha, kupitia kazi kubwa iliyofanywa na Dk. Samia, katika kipindi hiki cha miaka mitatu ya uongozi wake, wawekezaji kutoka Taifa la Bulgaria wanakusudia kujenga hoteli nne zenye hadhi ya nyota tano ambazo zitaendeshwa na Kampuni ya Kempinski katika Hifadhi za Taifa za Serengeti, Manyara, Tarangire na Hifadhi ya Ngorongoro.

Katika kipindi hiki Tanzania imekuwa mwenyeji wa mikutano na maonesho makubwa ya Kimataifa ya Utalii yaliyofanyika nchini ukiwemo Mkutano wa 65 wa Shirika la Utalii Duniani Kamisheni ya Afrika (65 th UNWTO-CAF Meeting) uliofanyika Oktoba, mwaka 2022 Jijini Arusha.

Mkutano huo ulifanyika sambamba na Jukwaa la Uwekezaji, Jukwaa la Utangazaji Utalii na Uzinduzi wa Mwongozo wa Uwekezaji wa Tanzania (UNWTO Investment attraction).

Katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Utalii inaendelea kuimarika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dk. Samia imeimarisha miundombinu ya utangazaji utalii kupitia matumizi ya teknolojia ya Habari na mawasiliano (Tehama). Wizara ya Maliasilina Utalii, kupitia Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) imenunua vifaa vya kisasa vya kituo cha kutolea taarifa za utalii kidijitali (Digital Command Center) ili kuwezesha utangazaji wa utalii kwa kutumia mitandao ya kijamii na tovuti.

Aidha, Serikali imejenga na kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 2,383.12 katika maeneo ya hifadhi za Taifa, mapori ya akiba, maeno tengefu na misitu ya hifadhi ya mazingira Asilia; viwanja vya ndege nane (8) katika Hifadhi za Taifa za Nyerere, Tarangire, Mkomazi, Saadani na Mapori ya Akiba ya Maswa na Ziwa Natron; Helipad tano katika Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro na kujenga malango tisa ya kupokelea wageni katika maeneo ya hifadhi za taifa, mapori ya akiba na hifadhi za misitu ya mazingira asilia.

**TANZANIA YA SITA DUNIANI KWA ONGEZEKO LA WATALII**

Chini ya uongozi wa maono wa Rais Dk. Samia, Tanzania inashuhudia ongezeko kubwa la watalii wa kimataifa, jambo ambalo limeongeza kwa kiasi kikubwa uchumi wa taifa.

Kulingana na 'Barometer ya Utalii ya Dunia' ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii Duniani (UNWTO), Tanzania imeibuka kama moja ya mataifa yanayoongoza kwa utalii, sambamba na nchi kama Qatar na Saudi Arabia. Taarifa hii inaonesha mafanikio ya sera za Rais Dk. Samia za kufufua sekta ya utalii.

Katika muda mfupi tu, Rais Dk. Samia ameweka kipaumbele kwenye utalii kama moja ya injini kuu za ukuaji wa uchumi. Serikali yake imeanzisha mipango ya kimkakati ya kuongeza mvuto wa kimataifa wa nchi, ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu, kampeni za uhamasishaji na ushirikiano na mashirika ya kimataifa ya usafiri.

Juhudi hizi zimesababisha ongezeko la watalii wanaovutiwa na mandhari nzuri ya Tanzania, wanyamapori wake wa aina mbalimbali, na urithi wake tajiri wa kitamaduni.

Kuongezeka kwa utalii hakukuongezi tu mapato, bali pia kunazalisha ajira kwa Watanzania, hususan katika maeneo ya vijijini ambako fursa za kiuchumi mara nyingi ni chache. Hii inaendana na dhamira ya Dk. Samia ya kuhakikisha maendeleo ya uchumi jumuishi, ambapo faida za utalii zinawafikia wananchi wote.

Zaidi ya hayo, msisitizo wa Rais Samia kwenye utalii endelevu unaiweka Tanzania mbele kama kivutio kinachowajibika. Kwa kukuza miradi rafiki kwa mazingira, serikali yake inalinda uzuri wa asili wa nchi wakati huohuo ikivutia watalii wanaojali mazingira.

Mbinu hii haihifadhi tu mifumo ya kipekee ya mazingira ya Tanzania, bali pia inaimarisha ustahimilivu wa sekta ya utalii dhidi ya changamoto za siku zijazo.

Tanzania inavyozidi kupanda kwenye ramani ya utalii wa kimataifa, kwa msaada wa mashirika ya kimataifa kama UNWTO, uongozi wa Rais Dk. Samia unathibitisha kuwa maono wazi na hatua za kimkakati zinazoweza kusababisha mabadiliko makubwa ya kiuchumi.

Akiwa kwenye usukani, Tanzania siyo tu ni kivutio; ni taa ya matumaini na fursa kwa watu wake.

**MADINI**

Ikiwa imetimia miaka mitatu na nusu sasa akiwa madarakani, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuisimamia na kuiongoza ipasavyo Sekta ya Madini kama ambavyo Kifungu cha 5 (1) cha Sheria ya Madini kinavyoainisha na hivyo kuifanya sekta hiyo kuendelea kuchangia vyema pato la taifa letu.

Kifungu hicho cha sheria kinaeleza kwamba, mali yote na udhibiti wa madini yote ndani, chini au juu ardhi yoyote, vijito, njia za maji kote Tanzania, eneo ndani ya mipaka ya bahari, rafu ya bara au eneo la pekee la kiuchumi ni mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya udhamini wa Rais kwa niaba ya Watanzania.

Kutokana na usimamizi huo thabiti, katika kipindi hiki akiwa madarakani, mchango wa Sekta ya madini katika pato la taifa umeendelea kuongezeka kutoka asilimia 6.7 mwaka 2020 hadi asilimia 7.3 mwaka 2021.

Kwa vipindi vya robo mwaka vya 2022, mchango wa sekta umekuwa ukiimarika, ambapo katika kipindi cha robo ya kwanza, Januari hadi Machi ulikuwa asilimia 7.8, robo ya Aprili hadi Juni asilimia 8.3 na robo ya tatu ya Julai mpaka Septemba mwaka 2022, mchango wa Sekta



# vyema miradi ya kimkakati

umefikia asilimia 9.7.

Naamini zikitoka takwimu mpya hivi mchango wa sekta ya madini utakuwa umepanda zaidi!

**UUZAJI WA MADINI NJE YA NCHI**

Katika kipindi hiki cha miaka mitatu na nusu ya Rais Dk. Samia madarakani sekta ya madini imeendelea kuongoza kuchangia mapato ya fedha za kigeni kutokana na mauzo nje ya nchi ambapo mwaka 2021 ilichangia asilimia 45.9 ya mauzo yote.

Aidha, mwaka 2022, jumla ya vibali 10,318 vya kuuza madini nje ya nchi vilitolewa vyenye thamani ya dola za Marekani milioni3,240.35 ikilinganishwa na vibali 5,526 vilivyotolewa mwaka 2021 vilivyokuwa na thamani ya Dola za Marekani ni milioni 3,046.23.

**UKUSANYAJI WA MADUHULI**

Makusanyo ya maduhuli kutokana na madini yameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Mwaka 2020/21 zilikusanywa Sh. bilioni 585.2, mwaka 2021/22 Sh. bilioni 624.6. Aidha, katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2022 jumla ya shilingi bilioni 353.4 zimekusanywa.

Katika miaka hii, Serikali imefanya marekebisho mbalimbali katika Sheria ya Madini Sura 123 na kanuni zake kupitia Sheria ya Marekebisho Mbalimbali, Na. 3 ya Mwaka 2022. Marekebisho hayo ni pamoja na kuanzisha leseni mpya ya uchenjuaji mdogo wa madini (Primary Processing Licence).

Hii ni kumpa Waziri mamlaka ya kurejesha serikalini maeneo ya leseni za madini zilizofikia ukomo; kuipa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini (GST) mamlaka ya kisheria ya kufanya utafutaji wa madini wa kimkakati; kuweka muda wa uhuishaji wa leseni za utafutaji wa madini (Prospecting License) wa kipindi cha pili; na kuweka ukomo wa umiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji (Primary Mining License) na kuanza shughuli za uchimbaji baada ya kupewa leseni.

**MCHIMBAJI MDOGO APATA SH. BILIONI 20 CHUNYA**

Dhana ya madini ni maisha na utajiri imejidhihirisha wilayani Chunya mkoani Mbeya hivi karibuni baada ya mchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu, Aidan Msigwa, Septemba 17, 2024 kusajili na kuuza madini ya dhahabu katika Soko la Madini Chunya ya kiasi cha kilo 111.82 zenye thamani ya Sh. bilioni 20.11.

Msigwa ni mchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu katika Wilaya ya Chunya anayemiliki leseni za uchimbaji mdogo (PML) na utafutaji wa madini (PL) katika maeneo tofauti wilayani humo. Aidha, anamiliki mtambo wa uchenjuaji wa madini ya dhahabu wilayani humo.

**UBORESHAJI BANDARI**

Kulikuwa na mizengwe mingi wakati Serikali ya Awamu ya Sita ilipotangaza kutaka kuingia mkataba wa miaka 30 na Kampuni ya DP World wa kuendesha Bandari ya Dar es Salaam, lakini sasa wahafidhina wote wanatafuta pa kuficha sura zao!

Makubaliano yale ya kusaini mikataba mitatu ya uwekezaji na uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam ni pamoja na Mkataba wa Nchi Mwenyeji, Mikataba ya Ukodishaji na Uendeshaji wa Gati namba 4 hadi 7.

Katika mkataba huo gati namba 0 hadi 3 zitatumiwa kwa pamoja baina ya Kampuni ya DP World na Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kwa ajili ya shughuli nyingine za kibiashara na Serikali.

Uwekezaji wa DP World kwenye bandari ya Dar es Salaam unatarajiwa kuongeza ajira na mapato ya serikali kutoka kwenye kodi ya forodha kwa asilimia 244, kutoka Shilingi trilioni 7.76 kwa mwaka 2021/22 hadi kufikia Sh. trilioni 26.7 kwa mwaka ifikapo 2032/33.

Pia Uwekezaji wa DP World unatarajiwa kuongeza shehena inayohudumiwa na bandari ya Dar es Salaam kutoka tani milioni 18.4 kwa mwaka 2021/22 hadi kufikia tani milioni 47.5 kwa mwaka ifikapo 2032/33.

DP World katika uwekezaji wao hapa Tanzania, wataongeza meli zinazotia nanga kwenye bandari ya Dar es Salaam mara dufu kutoka meli 1,569 kwa mwaka kwa sasa, hadi kufikia meli 2,950 kwa mwaka 2032/33.

Uwekezaji huu wa DP World kwenye Bandari ya Dar es Salaam unatarajiwa kuongeza ajira zinazotokana na shughuli za bandari kutoka ajira 28,990 kwa mwaka 2021/22 hadi kufikia ajira 71,907 ifikapo mwaka 2032/33. Hii ni sawa na ongezeko la mara tatu la ajira zilizopo sasa hivi kwenye bandari ya Dar es Salaam!

Ombi langu kwa Watanzania wenzangu, kwa hiki alichotuonesha Rais Dk. Samia, hatuna cha kumlipa zaidi ya kumrudisha madarakani kwenye Uchaguzi Mkuu ujao wa mwakani 2025.

Kumrudisha? Ndiyo; Machi 19 mwaka 2021 aliapishwa kuwa Rais wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

Safari hii ni zamu yetu kumweka madarakani. Mwenyezi Mungu akituweka hai tumrudishe Ikulu kwa njia ya sanduku la kura! Inshallah.

*Kwa maoni: 0768 888787 ama 0784 122020.*



## DENI LA TAIFA

# Bila kukopa mambo m

## ■ Kuna miradi ingemaliza hata miaka 70 kukamilika




**Na Hamisi Kibari**

DENI la Taifa ni kiasi cha fedha ambacho serikali ya nchi ikiwemo taasisi binafsi, zinakopa ili kufidia upungufu wa mapato.

Kwa upande wa serikali, hulazimika kukopa hasa pale ambapo matumizi yanapozidi mapato inayokusanya kutoka vyanzo mbalimbali, hususani kodi.

Serikali inaweza kukopa kutoka kwa wafadhili wa ndani kama benki za ndani au raia wake (mara nyingi kupitia hati fungani au kuchelewa kuwalipa wazabuni), na pia inakopa kutoka kwa wafadhili wa kimataifa kama mashirika ya kifedha (mfano IMF au Benki ya Dunia) au kwa nchi nyingine.

Kuhusu hati fungani (dhamana za serikali), ni kwamba badala ya wananchi kuweka fedha kwenye baadhi ya mabenki kwa akaunti za muda maalumu, kupitia hati fungani, wananchi hupata faida kubwa na hivyo kuboresha zaidi uchumi na maisha yao.

Hati fungani hutumika sana katika kuwekeza kwa sababu zinatoa mapato ya riba ya kawaida na zina hatari ndogo ikilinganishwa na uwekezaji kama wa hisa.

Kwa hiyo ni njia pia ambayo imekuwa ikitunisha mifuko ya wananchi na hivyo kuchangia pia kukuza mitaji na uwekezaji kwa wazawa.

Lingine la kufahamu ni kwamba serikali inapokopa kutoka kwa taasisi binafsi huongeza deni lake la taifa, lakini kwa upande mwingine taasisi hizi hupata riba kama faida ya uwekezaji wao.

Hii ni njia mojawapo ambayo serikali hutumia kupata fedha za kufanyia miradi pasipo kulazimika kukusanya kodi zaidi au kupunguza matumizi.

### MIKOPO YA TAASISI BINAFSI KWENYE DENI LA TAIFA

Ufafanuzi wa hili ni kwamba, sekta binafsi inapokopa nje, deni hilo husajiliwa Benki Kuu (BoT) na hata malipo yake yanafanywa kwa fedha za kigeni zilizopo nchini.

Kuna sababu nyingi za serikali kulitambua deni linalokopwa na sekta binafsi, kubwa ikiwa kwamba mhusika anaweza akahamisha fedha nyingi kwa mkupuo na kuleta athari katika uchumi wa nchi na pia ni lazima ieleweke fedha hizo zinakwenda kufanya nini zisije zikawa zinakwenda kutumika katika mambo yenye athari hasi kama kufadhili ugaidi, ushoga na mengine mfano wa hayo.

Kwa hiyo ukisikia Deni la Taifa, basi ujue kwamba zimo pia fedha zilizokopwa na sekta binafsi.

### DENI LA SASA LA TAIFA

Akiwasilisha Bajeti ya Serikali, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema deni la taifa limefikia Sh. trilioni 111.3, likiwa limeongezeka kwa asilimia 54 kutoka mwaka uliopita.

Ukuaji wa deni hili unatokana na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, huku uchumi wa taifa ukikua kwa asilimia 5.2 mwaka 2023.

Uwiano wa Deni la Serikali kwa Pato la Taifa (GDP) kwa sasa, ni asilimia 35.6, kiwango ambacho bado kiko chini ya ukomo wa asilimia 55 unaokubalika kimataifa.

Deni hili linajumuisha deni la nje na la ndani, ambapo deni la nje ni asilimia kubwa zaidi, likiwa asilimia 71.8 ya deni lote.

### WANAOLALAMIKIA DENI LA TAIFA

Baadhi ya Watanzania wamekuwa wakilalamikia ongezeko la Deni la Taifa kutokana na sababu kadhaa, kubwa ikiwa ni kukosa maarifa ya kutosha kuhusu Deni la Taifa au wanalizungumzia kisiasa zaidi.

Hata hivyo, mambo ambayo wamekuwa wakiyataja kusababisha hofu yao moja wapo ni ukuaji wa haraka wa deni na hivyo wamekuwa wakihofia kuwa litaiongezea nchi mzigo wa kodi au kupunguza huduma za msingi kama afya na elimu.

Pia wamekuwa wakidai kuwa miradi inayofadhiliwa na mikopo, haileti faida ya moja kwa moja kwa wananchi wa kawaida.

Lakini wapo pia ambao wamekuwa na hofu kwamba deni la sasa linaweza kuleta mzigo kwa vizazi vijavyo ambao watalazimika kulilipa.

Wengine wamekuwa wakilalamika kuwa kuna ukosefu wa uwazi kuhusu jinsi mikopo inavyotumiwa na jinsi miradi inavyosimamiwa.

### SABABU ZA KUKOPA

Kimsingi, tangu awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi yetu hadi awamu hii ya sita, serikali imekuwa ikikopa kwa sababu ya uhitaji wa kufanya miradi yenye tija kwa wananchi huku makusanyo ya fedha za ndani yakiwa hayatoshi na pia imekuwa ikifanya hivyo kwa sababu inakopesheka na inaaminika.

Kama tutakavyokuja kuona baadaye, takribani nchi zote duniani zinakopa zikiwemo nchi zinazoonekana kuwa na uchumi mkubwa kama Marekani, Japan na nyinginezo tena nyingine zina asilimia kubwa zaidi ya uwiano wa deni lilikofikia na GDP ya nchi hizo.

Mimi mwandishi wa makala haya, nilibahatika kushiriki semina maridhawa kuhusu deni la taifa na kwa bahati nzuri mmoja wa walimu wetu alikuwa Gavana wa sasa wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba ambaye wakati huo

# engi yasingewezekana



Daraja la Busisi

alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha.

Wanasemina tulijifunza kwamba hatua ya kukopa au kutokopa, inaanza na nakisi inayotokana na bajeti ya taifa.

Kwamba ukishakuwa na nakisi, unalazimika kukopa kwa ajili ya kufidia pengo hilo.

"Na kimsingi tunakopa kwa sababu sisi ni matajiri. Maskini hawezi kukopa. Tunakopa pia kwa sababu tunaaminika. Unaona mashirika makubwa kama Benki ya Dunia yanatukopesha ni kwa sababu tunaaminika," anasema Tutuba.

Anasema pesa hukopwa katika maeneo matatu; kwa ajili ya kuunga mkono bajeti (general budget support), kukopa kwa ajili ya sekta ambayo wadau wanadhani kuna changamoto zinazopaswa kutatuliwa kama vile sekta ya afya na tatu ni mikopo ambayo ni kwa ajili miradi ambayo wafadhili wenyewe huamua kupeleka fedha zao huko.

Kama ilivyo kwa mtu binafsi, mkopo unatakiwa uwe ni kwa ajili ya kuwekeza ama kufanya jambo muhimu la dharura na siyo kukopa kwa ajili ya, mathalan, kuolea mke mwingine au kustarehe. Na ukichunguza, matajiri wengi tunaowaona mitaani kwetu wakifanya vizuri kiuchumi, wamefika hapo walipo kwa sababu ya kukopa.

Na hivyo, Watanzania wanachopaswa kuuliza ni sababu za kukopa ambazo mara nyingi, kama si zote, huwa muhimu na zina majibu sahihi.

Lingine la muhimu kwa Watanzania ni kufuatilia usimamizi thabiti wa matumizi ya mkopo!

Mtu yeyote makini, kama ilivyo nchi, hukopa leo ili afanye mambo ya maendeleo huku akilipa taratibu kwa sababu thamani ya fedha zake leo haiwi sawa na kesho au kadiri muda unavyokwenda.

Gazeti moja liliwahi kumkariri Mchumi Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Profesa Aurelia Kamuzora akifafanua kwamba endapo uwekezaji mzuri unafanyika katika mikopo inayochukuliwa, uchumi wa nchi unaendelea kukua.

"Deni la Taifa linavyozidi kukua, ndiyo uchumi wa nchi unakua na nafasi ya kuongezeka inakuwepo pia kama fedha zinapokopwa zinawekwa vizuri kwa sababu mtaji wa kufanya miradi mbalimbali unakuwepo," ananukuliwa na gazeti hilo akisema.

Profesa anazidi kufafanua kwamba mzunguko wa fedha nchini unaongezeka kama fedha zinazokopwa zinaingia katika miradi.

Kwa wanaokumbuka, fedha zilizobatizwa za korona, Sh. trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) ambazo zilitumika kujenga miradi mingi ikiwemo ya madarasa na vituo vya afya, zilisababisha mzunguko mkubwa wa fedha kwa wananchi.

Wapo ambao walishiriki kutoa huduma mbalimbali kwenye miradi husika ikiwemo mafundi na hivyo mzunguko wa fedha hizo kuleta athari nyingi chanya kwenye jamii.

"Unajua hata nchi zilizoendelea zinakopa kwa ajili ya kufanya miradi mbalimbali na kuongeza mzunguko wa fedha.

Sioni shida ya deni kuongezeka kama zinatumika kwa tija na hazingii mifukoni mwa watu," anasema Profesa.

Nikirudi darasani kwenye semina, tulijifunza kwamba sababu ya kuwepo kwa haja ya kukopa, ni pamoja na ongezeko la watu na mahitaji yao, mapato ya ndani kutokidhi mahitaji ya vipaumbele vilivyopo na haja ya kufungua miundombinu ya mitaji ili kuongeza pato la mtu mmoja mmoja.

Sababu nyingine tukaelezwa kwamba ni kuongeza mapato ya ndani kwa kufungua miradi inayozalisha zaidi na kuzuia mtikisiko wa thamani ya Shilingi.

Sababu nyingine ni tabia za mkopaji kwamba tunakopa kwa mahitaji sahihi, uwezo wa kulipa tunao, dhamana ya mkopo na kuangalia masharti ya mikopo.

**AINA ZA MIKOPO**

Wananchi wanapaswa kujua pia kwamba mikopo mingi ambayo nchi imekopa, iko katika masharti nafuu ambayo riba yake ni chini ya asilimia moja na kipindi cha kuiva mikopo hiyo ni hadi miaka 40.

Kwa mfano, hivi karibuni, Tanzania ilipata mkopo kutoka Korea wa Dola bilioni 2.5 na watu wakavumisha kwamba eti Tanzania imetoa kipande cha bahari kama dhamana ya mkopo huo, kitu ambacho hakikuwa kweli. Kwanza, licha ya kwamba si Tanzania pekee iliyopata mkopo huo, lakini unalipwa kwa miaka 40 na riba yake ni asilimia 0.01.

Ni mkopo utakaotolewa kwa muda wa miaka mitano na utaanza kulipwa baada ya miaka 25.

Hata hivyo, kuna mikopo iliyo katika masharti ya kati ambayo riba yake ni chini ya asilimia tatu na kipindi cha kuiva mkopo ni hadi miaka 15 mpaka 20.

Kadhalika, kuna mikopo michache sana ambayo nchi imekopa ikiwa katika masharti ya kibiashara ambayo riba yake inalingana na hali ya soko na kipindi cha kuiva ni miaka saba.

**NI DENI HIMILIVU**

Kama tutakavyokuja kuona baadaye kulinganisha na nchi nyingine, deni la Tanzania bado ni himilivu (sustainable) kwani kuna nchi ambazo madeni yao si himilivu na hivyo tunaweza kusema 'hazikopesheki.'

*Inaendelea uk. 18*

# Bila kukopa mengi yangesimama



*Inatoka uk. 17*

Maana ya deni kuwa himilivu ni kwamba serikali inapokopa inakuwa pia na uwezo wa kulipa madeni yake ya sasa na madeni yake yatakayoiva baadaye bila kuathiri ukuaji wa uchumi na shughuli nyingine za serikali ikiwemo kutoomba msaada wa kulipiwa madeni kutoka mataifa au taasisi nyingine.

Hata hivyo, taarifa zilizopo ni kwamba Tanzania ni moja ya nchi inayokimbiliwa na wakopeshaji kutokana na uhimilivu wake.

Katika bajeti ya mwaka 2024/2025 , serikali imeeleza kuwa moja ya vipaumbele ilivyo navyo katika mwaka huu wa fedha, ni kulipa Deni la Taifa pamoja na kugharimia mishahara ya watumishi wa umma na maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Serikali pia imesema inaendelea na juhudi za kuimarisha miradi ya maendeleo ya kimkakati na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Cha msingi, elewa ndugu Mtanzania mwenzangu, kama si kukopa, kwa maana ya kutegemea makusanyo ya fedha za ndani, baadhi ya miradi ingechukua hata miaka 70 kukamilika, lakini miradi hiyo zikiwemo barabara, madaraja, hospitali na miradi ya maji, tunandelea kutumia na kunufaika nayo huku tukilipa kidogo kidogo. Wale ambao miaka ya nyuma wakitaka kwenda Musoma kutoka Dar es Salaam, walilazimika kupitia Nairobi, hili wanaweza kulielewa zaidi.

Elewa pia kwamba Deni la Taifa limekuwa likiongezeka kwa miaka ya hivi karibuni kutokana na mikopo ya ndani na nje ambayo serikali imekuwa ikikopa kwa ajili ya kufadhili miradi mikubwa ya maendeleo, kama vile ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere, barabara, madaraja na miundombinu mingine ya kijamii.

Kuna Mtanzania ambaye haoni haja ya kuwa na reli ya kisasa? Kuna ambaye haoni haja ya kuwa na umeme wa uhakikia kupitia ujenzi wa Bwawa la Julius Nyerere? Hii miradi itanyanyua haraka uchumi wetu, lakini kwa kutegemea makusanyo ya ndani pekee, pengine ingechukua miaka mingi sana kukamilika au ikashindikana kabisa.

## USIMAMIZI WA DENI, KUKOPESHEKA

Kama nilivyokwisha dokeza, Deni la Taifa bado ni himilivu na kwenye kila bajeti serikali inatenga fedha za kulipa deni.

Kwa mujibu wa tathmini za taasisi za kimataifa kama IMF na Benki ya Dunia, serikali imekuwa ikilipa madeni yake kwa wakati huku ikiendelea na mikakati ya kupunguza utegemezi wa mikopo kwa kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani, hususan kupitia kodi.

Kwa kifupi, taasisi hizi za kimataifa hususani Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), zimekuwa zikifanya ukaguzi, ambapo huangalia uwezo wa nchi kurejesha mikopo kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi, mapato ya ndani na uwiano wa deni na Pato la Taifa (GDP).

Ripoti ya Benki ya Dunia imeonyesha kwamba ukuaji wa uchumi wa Tanzania ulikuwa asilimia 5.2 mwaka 2023, ambayo ni dalili nzuri kwamba nchi inajiimarisha kiuchumi.

Hata hivyo, Tanzania inachukua mikopo kwa uangalifu, kuhakikisha kuwa mikopo hiyo inatumiwa kwa miradi yenye faida na inayosaidia kuongeza mapato, hivyo kuongeza uwezo wa kulipa mikopo hiyo kwa wakati.

## NCHI ZA AFRIKA ZENYE MADENI MAKUBWA

Nchi nyingi za Afrika zinakabiliwa na changamoto za madeni, ambapo baadhi ya nchi zina viwango vya juu vya deni la taifa kutokana na sababu mbalimbali kama vile kushuka kwa mapato, vita vya ndani, changamoto za kiuchumi au uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu.

Baadhi ya nchi za Afrika zenye deni kubwa ni pamoja na Sudan ambayo deni lake ni takribani asilimia 211 ya GDP.

Nchi nyingine pamoja na uwiano wa deni na Pato la Taifa (GDP) kwenye mabano ni Eritrea (175%), Cape Verde (160%), Msumbiji (120%), Zambia (115%), Angola (100%), Ghana (80-85%), Kenya (70-75%), Afrika Kusini (70%) na Ethiopia (karibu 60-65% ya GDP).

Lakini kama tulivyoangalia hapo awali, uwiano wa deni la Serikali ya Tanzania kwa Pato la Taifa (GDP) kwa sasa, ni asilimia 35.6, kiwango ambacho bado kiko chini ya ukomo wa asilimia 55 unaokubalika kimataifa.

Inaelezwa kwamba nchi nyingi za Afrika zenye madeni ambayo si himilivu, zinakopa kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu na miradi mingine ya kijamii, lakini ukosefu wa usimamizi mzuri wa fedha na changamoto za kiuchumi zinafanya madeni haya kuwa mzigo mkubwa kwa baadhi ya nchi hizi.

## NCHI NYINGINE NJE YA AFRIKA ZENYE DENI KUBWA

Nchi nyingi duniani zina deni la taifa, lakini baadhi ya nchi zina madeni makubwa sana kutokana na ukubwa wa uchumi wao, sera za matumizi ya serikali au hali ya kiuchumi.

Zifuatazo ni nchi ambazo zina madeni makubwa (kwa uwiano wa asilimia ya Pato la Taifa – GDP):

Inayoongoza ni Japan yenye karibu asilimia 260 ya GDP. Nchi nyingine zenye deni kubwa na uwiano wake na pato la taifa (GDP) kwenye mabano ni Ugiriki (180%), Italia (145%), Lebanon (150%), Venezuela (zaidi ya 300%), Marekani (120%) na Argentina (asilimia 100 ya GDP).

Nchi za Ureno, Hispania na Uingereza, pia zina viwango vya juu vya deni, ingawa siyo sawa na nchi hizo tajwa hapo juu.

Lakini ni ukweli pia kwamba deni linapokuwa kubwa, inaweza kuwa hatari kwa uchumi wa nchi ikiwa halidhibitiwi vizuri, kwani linaweza kusababisha kudorora kwa maendeleo au kutegemea zaidi mikopo ya kimataifa.

## NCHI AMBAZO HAZIKOPESHEKI

Nchi ambazo hazikopesheki kwa urahisi mara nyingi zinajulikana kama "nchi zenye hatari kubwa ya kufilisika au zilizoshindwa kulipa madeni (sovereign default) na hivyo zina uwezo mdogo au hazina kabisa uwezo wa kupata mikopo kutoka masoko ya kifedha ya kimataifa.

Hii inatokana na mambo kama vile madeni makubwa, ukosefu wa utulivu wa kisiasa, migogoro ya ndani, au uchumi dhaifu.

Nchi hizi zinaweza pia kuwa na mikopo ya zamani ambayo hawajalipa (default), hali inayozuia uwezo wao wa kukopesheka. Baadhi ya nchi za Afrika na nje ya bara hilo zenye hali hii ni pamoja na Zimbabwe, Sudan, Eritrea, Somalia, Chad, Sudan Kusini na Venezuela.

Athari za kutokopesheka ni pamoja na kukosa fedha muhimu za maendeleo, kama vile kwa ajili ya kujenga miundombinu, huduma za afya na elimu au kunapotokea majanga.

Nchi hizi pia huwa na matatizo ya kijamii na kiuchumi kwa maana ya kwamba hali hii mara nyingi inasababisha kuporomoka kwa huduma za kijamii, kushuka kwa thamani ya sarafu na ugumu wa kuwekeza katika sekta za uzalishaji mali.

Nchi inapokosa sifa za kukopesheka, pia hujikuta ikiongeza utegemezi wa misaada ya kimataifa kutoka kwa mashirika kama Umoja wa Mataifa au nchi wafadhili, badala ya kupata mikopo kwa masharti ya kibiashara.

Kukosa uwezo wa kukopesheka, ni changamoto kubwa kwa nchi zinazoendelea, kwani kunadhoofisha uwezo wao wa kushiriki kikamilifu kwenye uchumi wa kimataifa na kuboresha maisha ya raia wao.

Watanzania tumshukuru sana Mungu hatuko huko. Deni letu bado ni himilivu, tunakopesheka na hivyo tuna uwezo wa kuendelea kubuni miradi ya maendeleo itakayosisimua uchumi na kuongeza uwezo wetu wa kuhudumia madeni.

Tusihoji deni, bali tuhoji sababu ya deni na tujikite kwenye kujiridhisha kwenye usimamizi wa fedha tunazokopa.

## DENI LA TAIFA HALIGAWANYWI KWA KILA MTANZANIA

Ipo dhana kwamba Deni la Taifa linagawanywa kwa kila Mtanzania na hata mtoto anayezaliwa leo au kesho, anakuwa na sehemu yake ya kulipa.

Haya ni maneno ya kwenye vijiwe vya kahawa ambayo hayana maana yoyote kuhusina na Deni la Taifa.

# Rais Samia na kazi pevu ya kujenga Taifa

**Na Hamid Yassin**

SEPTEMBA 19 wiki iliyopita, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alitimiza miaka mitatu na miezi sita tangu aapishwe Machi 19, mwaka 2021 kuongoza taifa hili la Tanzania ikiwa ni Awamu ya Sita tangu tupate uhuru kutoka kwa wakoloni wa Kiingereza.

Ni miaka ya kazi hasa, kama ilivyo kauli mbiu yake aliyoingia nayo madarakani ya 'Kazi iendelee'. Ameendeleza yale yote mazuri ya awamu ya tano ambayo yeye alikuwa Makamu wa Rais na alishiriki kikamilifu kuyaanzisha na kuyasimamia.

Katika miradi yote mikubwa ya kimkakati ameendelea kuidhinisha fedha ili iendelee kama ilivyopangwa. Hii ni kama vile ile ya Reli ya Mwendokasi (SGR), Bwawa la Mwalimu Nyerere, barabara kubwa na ndogo na hata ule mradi wa REA wa umeme vijijini, tumeshuhudia ndege zilizonunuliwa zinaendelea kuwasili nchini ndani ya hii miaka mitatu na miezi sita.

Lakini kama hiyo haitoshi amekuja na mipango yake mingine thabiti ya kufufua uchumi uliyoyumba kwa sababu mbalimbali ikiwemo ile ya gonjwa hatari la UVICO 19.

Ameelekeza ukusanyaji mzuri na wakiungwa wa kodi toka kwenye vyanzo mbalimbali hususani kwa wafanyabiashara ambapo aliagiza ule 'ubabe' dhidi yao ukome.

Rais Dk. Samia kwa kasi kubwa anarudisha uhusiano uliotetelek a na mataifa mbalimbali na hivi niandikapo makala haya Mama ameshatembelea mataifa kadhaa ya nje, makubwa ameshahudhuria mikutano mbalimbali ya kimataifa ambayo haikuhudhuriwa na kiongozi mkuu wa nchi wakati wa Serikali ya Awamu ya Tano.

Katika kipindi hiki kifupi pia Rais Samia ameonyesha kwamba yeye ni msikivu. Amesikiliza vilio na malalamiko kadhaa ya wananchi anawaongoza na kutolea majawabu ya haraka na yenye manufaa kwa raia wake.

Hii ni kama vile toza za miamala ya simu zilizoanzishwa miaka kadhaa iliyopita ambapo baada ya malalamiko toka kwa wananchi haraka aliviagiza vyombo husika kuliangalia hilo na tayari tozo hizo zimepunguzwa kwa asilimia thelathini na hivi sasa mambo ni shwari.

Amekuwa akitembea kukagua miradi mbalimbali na kuwa mkali kwa ile inayosuasua ambapo sasa tumeshuhudia miradi kadhaa ikienda kwa kasi ya 'kimbunga'.

Huwezi kuyataja yote bila kugusia lile jambo la kuunda Kamati Maalumu ya Ugonjwa wa COVID 19 chini ya Mwenyekiti wake, Prof. Said Aboud ambapo ilikuja na majibu mazuri ya kumshauri rais akubali kuidhinisha chanjo ya hiari kwa ugonjwa huo ambapo hivi niandikapo makala haya tayari Watanzania kadhaa wameshachanjwa na wengine wakiendelea kujitokeza kupata chanjo bure, yaani bila malipo yoyote yale.

**MAFUTA**

Toka dunia ianze kufunguka na shughuli za watu kuanza kurudi, kufuatia lile janga la ugonjwa wa Uvico – 19, bei za mafuta ziliendelea kupanda kote duniani kuanzia mafuta ya vyombo vya moto na mafuta ya kula.

Kwa sasa tani ya mafuta ya petroli kwenye soko la dunia inauzwa kati ya Dola 500 mpaka 1000, dizeli, mafuta ya kula na mengine nayo bei ziliendelea kuwa juu sana toka janga lile la Uviko-19.

Bei za mafuta kwenye soko la dunia bado hazijatengemaa (Stable) na zimeendelea kupanda kwa muda mrefu sana toka dunia ianze kurudi taratibu kwenye uhalisia na shughuli zake.

Kupanda kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia moja kwa moja kunapandisha bei ya mafuta sokoni na kwa mlaji wa kawaida na wa mwisho.

Hapa Tanzania licha ya ushuru, tozo na kodi mbalimbali zinazotozwa kwenye mafuta lakini kupanda kwa bei soko la dunia ndiko kumechangia pakubwa sana kupanda kwa bidhaa hii muhimu sana kwa maisha na uchumi wa watu na nchi.

Njia pekee ya Serikali katika jambo hili ilikuwa ni kuingilia kati na kulibeba kwa gharama yoyote ile ili kumsaidia Mtanzania asiumie na kifupi, Serikali ya Dk. Samia iliamua kubeba mzigo huu wa kupanda kwa mafuta kwenye soko la dunia ili kulinda ustawi na maslahi ya Watanzania.

Serikali ya Awamu ya Sita iliondoa tozo 8 zilizokuwa zinatozwa kwenye mafuta kuanzia tozo ya udhibiti iliyokuwa inatozwa na Mamlaka ya Udhibiti wa huduma za Nishati na Maji, tozo ya miundombinu iliyokuwa inatozwa na Mamlaka ya Bandari.

Tozo ya kupima ubora wa mafuta kwenye meli na gharama ya uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta iliyokuwa inatozwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), tozo ya uhakiki wa ujazo wa mafuta melini iliyokuwa inatozwa na Wakala wa vipimo nchini, tozo ya forodha iliyokuwa inatozwa na Wakala wa usimamizi wa meli pamoja na tozo ya ushuru wa huduma iliyokuwa inatozwa na Halmashauri 4 zenye maghala ya kupokea mafuta za Kigamboni, Temeke, Tanga na Mtwara.

Tozo hizi pekee kwenye mafuta zilikuwa zinakusanya Milioni 300 kwa siku na Bilioni 102 kwa mwaka mzima na ni Mtanzania ambaye ndiye mtumiaji wa mwisho aliyekuwa analipa tozo hizi kupitia kupata huduma ya mafuta.

Sasa licha ya dunia kushuhudia mfumuko mkubwa wa bei kubwa ya mafuta kwenye soko la dunia kwa muda mrefu ambayo imeathiri moja kwa moja bei zetu za ndani, Serikali ya Dk. Samia imeamua kubeba mzigo huo kwa kupunguza kodi, ushuru na tozo zake 8 zilizokuwa zinatozwa na Taasisi zake 8 nchini ili bei ya mafuta ishuke sana licha ya bei kwenye soko la dunia kuendelea kuwa juu.

Kwa hiyo ili kumlinda Mtanzania ambaye ndiye mhanga namba moja wa kupanda kwa hizi bei, Serikali ya Rais Dk. Samia iliamua kufuta tozo hizi 8 zilizokuwa zinatozwa kwenye bidhaa za mafuta ili bei ishuke na wananchi wasiumie kwa sababu tu bei ni kubwa soko la dunia.

Hii ni njia ya Serikali sikivu tu, Serikali ya Kidemokrasia na inayojali watu inaweza kuchukua kwa kubeba mzigo wa madhila ya nje kama haya ya kupanda kwa bei za bidhaa ili wananchi wake wabaki na unafuu. Heko Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan katika hili.

**DK. SAMIA AMETOKEA WAPI?**

Bi Samia alizaliwa Januari 27, 1960 visiwani Zanzibar ambapo alipata elimu ya msingi kati ya 1966 na 1972 katika shule tofauti tofati katika visiwa viwili vikubwa vinavyounda Kisiwa cha Zanzibar.

Rais Samia alianza safari yake ya elimu katika shule ya msingi Chawaka iliyopo kisiwani Unguja na baadaye alihamia shule ya msingi Ziwani iliyopo kisiwani Pemba kabla ya kurejea kisiwani Unguja na kumaliza elimu ya msingi katika shule ya msingi ya Mahonda.

Elimu ya Upili ama Sekondari aliisoma kati ya mwaka mwaka 1973 mpaka mwaka 1976 ambapo kama ilivyokuwa kwenye elimu ya msingi,

Samia Suluhu Hassan alisoma shule mbili tofauti ambapo alisoma kidato cha kwanza mpaka cha nne katika shule ya sekondari ya Ngambo iliyopo visiwani Unguja kati ya mwaka 1973-1975 kabla ya kuhamia sekondari ya na Lumumba, iliyopo kisiwani Unguja mnamo mwaka 1976 ambapo alihitimu kidato cha nne.

Baada ya kumaliza elimu ya Sekondari, Bi Samia hakujiunga moja kwa moja na masomo ya Chuo, kwani mwaka 1977 aliajiriwa kama mchapishaji katika serikali ya Zanzibar ambapo alipanda mpaka ngazi ya kuwa Afisa wa Mipango serikalini kati ya 1987 na 1988.

Wakati akiwa mtumishi katika serikali ya mapinduzi ya Zanzibar, Bi Samia alikuwa akijiendeleza kielimu ambapo alisoma kozi fupi mbalimbali ikiwemo ya cheti cha takwimu kabla ya kujiunga na Taasisi ya Maendeleo na Uongozi ya Mzumbe Morogoro ambapo alihitimu stashahada ya juu ya Utawala mnamo mwaka 1986.

*Inaendelea uk. 20*



# Samia na kazi pevu

*Inatoka uk. 20*

Kati ya mwaka 1992 mpaka 1994 Rais Samia alisoma stashahada ya Uzamili ya Uchumi katika Chuo Kikuu cha Manchester kilichopo nchini Uingereza.

Kiu ya Mama Samia kujiendeleza kielimu haijawahi kufikia ukomo kwani mwaka 2015 alihitimu shahada ya uzamili katika Maendeleo ya Uchumi ya Jamii katika programu ya ushirikiano kati ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Chuo kikuu cha Southern New Hampshire cha nchini Uingereza.

Rais Samia aliolewa miaka miwili tu baada ya kuhitimu elimu yake ya sekondari kule visiwani Zanzibar mnamo mwaka wa 1978, ambapo alifunga pingu ya maisha Bw. Hafidh Ameir, ambaye wakati huo alikuwa Afisa wa Kilimo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo wawili hao wamejaliwa watoto wanne; mmoja kati ya wanawe Bi. Wanu Hafidh Ameir aliyezaliwa mwaka 1982 ndiye anayefuata nyayo za mama yake kwani ni Mwakilishi Maalum katika Bunge la Zanzibar.

Rais Samia mbali na kuhudumu Serikalini tangu amalize masomo yake ya sekondari akiwa na miaka 16, alipata kufanya kazi na mashirika ya kimataifa ambapo kati ya Mwaka 1992 mpaka mwaka 1994 alifanya kazi na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula ambapo alihudumu kwa nafasi ya Afisa Miradi.

Pia mbali na kufanya kazi Serikalini na katika Shirika hilo la Umoja wa Mataifa, Bi. Samia alipata kufanya kazi na taasisi zisizo za kiserikali kwa miaka karibu kumi akijikita zaidi katika harakati za usawa wa kijinsia.

Alijiunga rasmi na siasa mwaka wa 2000 wakati alipochaguliwa kwenye Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kama Mjumbe Maalum.

Kuingia kwake kwenye siasa kuliifanya nyota yake kuanza kuchomoza katika medani za kisiasa na uongozi ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya akateuliwa kuwa Waziri wa Afya, Jinsia na Watoto; uteuzi uliofanywa na Rais wa kipindi hicho Aman Abeid Karume.

Mwaka 2005 alichaguliwa tena kuwa mjumbe maalum na kuteuliwa upya kama waziri, wakati huu akipewa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji katika Serikali ya visiwani. Mwaka wa 2010 alitia nia ya kuwania uwakilishi ambapo alichaguliwa kuwa mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi huko Zanzibar.

Nyota ya Bi Samia ilivuka mipaka kwani muda mfupi baada ya uchaguzi mkuu wa 2010 alichomoza kwenye Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kuteuliwa na aliyekuwa Rais wa Tanzania Jakaya Kikwete kuwa waziri wa maswala ya Muungano katika serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akihudumu chini ya Makamu wa Rais Mohamed Gharib Bilal.

Machi mwaka 2014 Tanzania iliingia kwenye vuguvugu la kubadili Katiba yake ambapo huko nyota ya Rais Samia ilichomoza tena baada ya kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba mjini Dodoma.

Bi Samia alichaguliwa kwa kura 390 sawa na asilimia 74.6 na kumshinda mpinzani wake Amina Abdalla Amour ambaye alipata kura 126 sawa na 24%. Atakumbukwa sana wakati wa Bunge la Katiba, kwani ndipo alipoanzwa kutabiriwa kushika nafasi ya juu zaidi ya kiutawala ambapo mmoja wa wajumbe aliwaasa wajumbe wamfikirie Mama Samia kwa nafasi ya juu zaidi kwenye uchaguzi uliokuwa unafuata wa mwaka 2015.

Nyota ya Bi Samia Suluhu haikuwahi kuzimika wala kufifia kwani Julai mwaka 2015, Dkt. John Magufuli mara baada ya mpambano mkali ndani ya CCM uliompa ushindi wa kupeperusha bendera ya CCM kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka huo, mbele ya wajumbe wa mkutano Mkuu alimpendekeza Mama Samia kuwa mgombea mwenza wake.

Hatimaye baada ya uchaguzi Bi Samia aliweka historia nyingine ya kupanda katika siasa za Tanzania kwa chama chake kupata ushindi kwenye uchaguzi mkuu uliomuweka yeye katika historia nyingine ya kuwa msaidizi mkuu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maana ya Makamu wa Rais.

Mwaka 2020, aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati John Magufuli wakati akiomba ridhaa ndani ya Chama chake ili apeperushe tena bendera ya CCM kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huo, kwa mara nyingine alimpendekeza Dk. Samia kuwa mgombea mwenza wake ambapo ushindi wa chama chake uliilinda historia ya Mama Samia.

Baada ya kifo cha aliyekua rais wa awamu ya tano Dk. John Pombe Magufuli katiba ilimlazimu Dk. Samia kuwa Rais wa Tanzania na kuweka historia nyingine ya Rais wa kwanza wa mwanamke Tanzania.


Wengi walimtilia Shaka lakini aliwahakikishia Watanzania baada ya ile kauli aliyoisema Dodoma baada ya kuapishwa; "Huyu aliyesimama hapa ni Rais mwenye maumbile ya kike," alisema Rais Samia.

Hayo ndiyo machache yanayomuhusu Samia Suluhu Hassan toka pale alipozaliwa na maisha yake ya siasa bila kukata tamaa; daima alisonga mbele kutimiza ndoto zake.

*Kwa maoni na ushauri;*
*0768 888 787 ama 0784 122 020.*



Bungeni.



Samia alipokuwa Makamu wa Rais, akiwa na Hayati John Magufuli.



Rais Samia na mume wake, Hafidh Ameir.

# Majeshi yetu na uchumi imara wa viwanda

**Na Hamid Yassin**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, amekuwa akiendeleza mipango ya watangulizi wake kuhakikisha majeshi yetu pia yanashiriki ipasavyo katika kuinua uchumi wa Taifa.

Jeshi la Magereza nchini, limekuwa likizalisha mazao mbalimbali ili kujitosheleza kwa chakula, kuepuka utegemezi kutoka serikalini pia kuzalisha na kutengeneza bidhaa mbalimbali ili kusaidia Serikali katika azma yake ya kufikia Tanzania ya viwanda.

Huko nyuma, ujenzi wa nyumba za maafisa wa Jeshi la Magereza kwenye Gereza Kuu la Ukonga jijini Dar es Salaam, ulikuwa ukifanywa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), lakini hivi sasa kazi hizo zinafanywa na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia SUMA-JKT kukamilisha miradi yote ya jeshi hilo.

Katika kutekeleza agizo la Rais Dk. Samia, idadi ya wafungwa wapatao 1,553 wamehamishiwa kwenye magereza 10 ya kimkakati, ambapo Jeshi la Magereza linatekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo chini ya Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza, Cooperation-Sole, ambapo shirika lina jumla ya miradi 23, kati ya miradi hiyo 15 ni ya kilimo na mifugo na miradi nane ni ya viwanda vidogo vidogo.

Kuhusu kuunga mkono ajenda ya Tanzania ya Viwanda, Jeshi la Magereza limekuwa likiendesha miradi nane ya viwanda vidogovidogo ambayo ni pamoja na ushonaji wa nguo na useremala katika Gereza Kuu la Ukonga Dar es Salaam, utengenezaji wa viatu Gereza la Karanga Kilimanjaro, kiwanda kinachoendeshwa kwa ubia na Shirika la Hifadhi ya Jamii PSSSF.

Viwanda vingine chini ya jeshi hilo ni pamoja na kiwanda cha uchakataji ngozi, samani na mbao kilichopo Gereza la Uyui, Tabora, kiwanda cha samani katika Gereza la Arusha, kiwanda cha sabuni Gereza Ruanda Mbeya, kiwanda cha chumvi katika gereza la Mtwara, pamoja na kiwanda cha uhunzi katika Gereza la Kingolwira mkoani Morogoro.

Hali kadhalika, Shirika la Magereza, lina kikosi cha ujenzi ambacho kimesajiliwa kufanya kazi za ukandarasi wa majengo, ufyatuaji wa matofali, pamoja na ujenzi wa miundombinu ya barabara na mifumo ya umeme.

Kikosi hiki hufanya kazi za ujenzi wa majengo ya aina zote kwa ajili ya matumizi ya ofisi, makazi na shughuli za biashara.

Sambamba na shughuli hizo, vipo vikosi vya kufanya ukarabati wa miundombinu ya magereza kwa kuwashirikisha wafungwa kwa ajili ya kuwapa ujuzi katika stadi mbalimbali za ujenzi zikiwemo uashi, useremala, umeme, rangi pamoja na ufundi bomba.

Kwa upande wa mifugo kuna miradi ya mifugo katika magereza ya Kingolwira yenye mifugo 52,



**Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Dk. Samia Suluhu Hassan, akihutubia viongozi, wageni mbalimbali na wananchi wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam Septemba mosi, mwaka huu.**

Mbigiri Morogoro kuna mifugo 968, Prison Mugumu Mara mifugo 1359, Kitengule Kagera kuna mifugo 742 na Gereza la Isupilo, Iringa kuna mifugo 99.

Aidha, Gereza la Arusha, kuna mifugo 90, Mollo, Rukwa 168, Mang'ola, Arusha 68, Ruanda, Mbeya 14, Songwe 169, Kiberege 119, Idete, Morogoro 15, Kitai, Ruvuma 53 na Mkwaya mifugo 22.

Kwa upande wa kilimo, kuna zao la mahindi katika shamba la Songwe mkoani Mbeya lengo lilikua kulima hekta 400 ambapo eneo lililolimwa ni hekta 300 na matarajio ya mavuno ni tani 1,350, Gereza Kitai mkoani Ruvuma, lengo hekta 400 eneo lililolimwa ni hekta 260 matarajio ya mavuno ni tani 1,170, Ludewa mkoani Njombe, lengo hekta 280 eneo lililolimwa hekta 200 na matarajio ya mavuno tani 900.

Mkoani Kagera, lengo lilikuwa hekta 300, eneo lililolimwa hekta 272 na matarajio ya mavuno ni tani 1,206 na Gereza la Mollo mkoani Rukwa, lengo hekta 400 eneo lililolimwa ni 374 matarajio ya mavuno ni tani 1449. Jumla ya mahindi wanayotarajia kuvuna ni tani 6,075, hivyo kwa upande wa mahindi matarajio ni gereza kujitosheleza kwa asilimia 73.41.

Kwa upande wa zao la mpunga, Gereza la Pawaga lengo ni kulima hekta 150, eneo lililolimwa ni hekta 60 na matarajio ni kuvuna hekta 394; Idete mkoani Morogoro, lengo ni kulima hekta 280 zilizolimwa ni 200 na matarajio yake ni kuvuna hekta 1313, Kiberege mkoani Morogoro lengo hekta 200 eneo lililolimwa 160 matarajio ni kuvuna hekta 1,050 Jumla ya tani za mpunga ni 2,756.

Maharage Gereza la Kidete wilayani Nkasi, wana lengo la kulima hekta 120 eneo lililolimwa ni hekta 72 matarajio kuvuna tani 136, Gereza la Arusha wana lengo la kulima hekta 120 eneo lililolimwa wamevuka lengo kufikia hekta 144 wanatarajia kuvuna tani 247.2 na Kitengule mkoani Kagera, lengo hekta 100 eneo lililolimwa ni hekta 30 matarajio ni kuvuna tani 60.8.

Mkoa wa Dar es Salaam una jumla ya magereza manne ambayo ni Gereza Kuu Ukonga, Keko, Segerea na Gereza la Wazo Hill.

Aidha, zipo kambi mbili ambazo ziko chini ya Gereza la Ukonga ambazo ni kambi ya Kimbiji na Mvuti.



Kazi zinazofanywa na wafungwa katika magereza hayo ni pamoja na kilimo cha michikichi na ukamuaji wa mawese katika Gereza la Ukonga (Kambi ya Kimbiji) na kazi za useremala na ushonaji katika Gereza la Ukonga.

Kazi za vibarua katika mradi wa ujenzi wa nyumba za watumishi pia hufanya na baadhi ya wafungwa katika Gereza Ukonga.

Kazi nyingine wanayofanya ni utengenezaji wa kokoto katika Gereza la Wazo Hill, kazi za usafi kwenye maeneo ya makambi, kilimo cha bustani za mbogamboga na matunda pamoja na ufyatuaji matofali ambazo zinafanyika katika magereza yote hapa nchini.

Kuna mradi usio wa kimkakati wa kuchakata ngozi za mbuzi, kondoo na ng'ombe katika Gereza la Uyui mkoani Tabora, ambao ulianza rasmi Oktoba 15, 2018 kwa mkopo wa shilingi bilioni 5 na bado unaendelea hadi kwenye hii awamu ya sita ya Dk. Samia.

Kazi zinazofanyika ni uchakataji wa ngozi pamoja na kutengeneza bidhaa zinazotokana na ngozi vikiwemo viatu vya shule, mabegi na makobazi (sandals) za aina mbalimbali kwa ajili ya jinsia zote na rika zote.

Mradi huo umelenga kuipunguzia serikali mzigo na gharama za uendeshaji wa magereza, kwa kuzalisha bidhaa zilizo bora kwa gharama nafuu.

Hii itasaidia kuongeza ujuzi kwa watumishi na kutoa ajira ndogondogo kwa jamii inayozunguka magereza hayo kwa kununua ngozi ambazo awali walikuwa wakizitupa. Lakini pia unatoa ujuzi kwa wafungwa.

Inaendelea uk. 11

# Majeshi yetu na uchumi imara wa viwanda



**Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, akikagua shamba la SUMA JKT Mngeta Plantation lililoko katika Wilaya Kilombero mkoani Morogoro.**

Inatoka uk. 10

### SUMA JKT NA TANZANIA YA VIWANDA

Rais Samia ambaye pia ni Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, amesema moja ya mkakati wa Serikali iliyojiwekea katika kuzingatia diplomasia ya ulinzi na usalama ni kujenga Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) lenye sekta maalumu ya uchumi na hivyo serikali, mbali na kuboresha vilivyopo, inakwenda kufufua viwanda vya kijeshi.

Rais Samia alisema hayo hivi karibuni wakati akizungumza na taifa kuhusu maadhimisho ya miaka 60 ya JWTZ na kuongeza kwamba mkakati huo umeshaanza na kwamba baada ya miaka mitatu hadi minne jeshi litakuwa limeshaanza uzalishaji wa bidhaa kwa kutumia viwanda vyake.

Kuna Kituo cha uwekezaji cha JWTZ kilichoko katika kikosi cha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Mgulani Jijini Dar es Salaam, ikiwa ni miradi mahsusi ya jeshi yenye azma ya kuunga mkono jitihada ya kuifikia Tanzania ya viwanda na yenye uchumi wa kati. Kumbuka, JKT ni sehemu ya Jeshi la Wananchi.

Kituo hicho cha uwekezaji kina viwanda vya kushona nguo, kiwanda cha kutengeneza maji ya kunywa, kiwanda cha kukereza vyuma pamoja chuo cha ufundi stadi (VETA), Shule ya Sekondari Jitegemee na kumbi mbili za mikutano za (Muhuga na Isamuhyo), uwekezaji ambao umegharimu Sh. bilioni 5.793.

Miradi hii mikubwa inayomilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) sio tu ni mfano wa kuigwa katika kuelekea Tanzania ya viwanda bali ni mkombozi wa suala la ajira kwa vijana hasa wale waliomaliza vyuo vikuu, pia ni shule tosha kwa vijana hasa wale wanaotaka kujiajiri katika sekta mbalimbali za ufundi na hata ujasiriamali.

Inafahamika kuwa uwekezaji unatumia fedha nyingi na ili mradi husika uendelee kukua na kuleta tija ni lazima ujiendeshe kwa faida ili kumudu gharama za uendeshaji ikiwemo kulipa wafanyakazi, kulipia huduma za umeme na maji pamoja na ukarabati na ununuzi wa mashine na vipuri, kadhalika malighafi zinazotumika kiwandani ama kwenye mradi husika.

Pamoja na SUMA JKT kushiriki katika miradi mingi ya kiuchumi, kumekuwa na tatizo sugu la wadau kuchelewesha malipo ama kutolipa kabisa kazi zinazofanywa na kitengo hicho cha uzalishaji cha jeshi.

Kwa Watanzania na wapenda maendeleo sio jambo la kiuungwana wala sio sifa kupewa huduma na kutoilipia, hali hii inaonyesha kiwango kikubwa cha ukosefu wa uzalendo kwa baadhi ya taasisi za serikali, taasisi binafsi pamoja na watu binafsi walioshindwa kulipia huduma walizopewa na SUMA JKT.

Kwa kuwa uzalendo unaanza kwa watu binafsi ni vyema wadaiwa hao wakalipa madeni yao haraka, tena haikutakiwa hadi Mhe. Rais Dk. Samia aje awakaripie ndipo walipe, kiuungwana walitakiwa wawe wamelipia huduma walizopewa ili kuiwezesha SUMA JKT kujiendesha.

Aidha, JWTZ kwa kushirikiana na wahisani pamoja na washirika wa maendeleo linatarajia kujenga kiwanda cha chumvi huko Kilwa mkoani Lindi, na pia wanatarajia kuanzisha kiwanda cha maji tiba kwa kushirikiana na mfuko wa bima ya Taifa (NHIF).

Mwelekeo huu wa Jeshi kwa hakika utasaidia kukimbiza maendeleo ya Watanzania kama Rais Dk. Samia anavyotaka. Rai ni kwa wapenda maendeleo wote nchini kuhakikisha wanasapoti miradi mikubwa na ya mfano inayoanzishwa na kuendeshwa na majeshi yetu ili yaweze kutupatia matokeo chanya.

Majeshi mengine pia yanapaswa kuiga mfano wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na lile la magereza katika kuunga mkono Tanzania ya viwanda kwani wana rasilimali watu ya kutosha, lakini pia wana weledi na nidhamu ambavyo ni silaha kuu ya kukuza maendeleo ya kiuchumi duniani kote.

### RAIS SAMIA MWELEKEO MZURI

Hatua ya Rais Samia kueleza kwamba sasa wanafufua viwanda vya jeshi na kuboresha vilivyopo ni njia sahihi ambayo hata baadhi ya nchi zinafanya. Kwa mfano, nchini ya Vietnam inatumia sana jeshi lake kuanzish

Kwa mfano kampuni ya Halotel ambayo ina takribani miaka minane nchini, inamilikiwa na kampuni ya Viettel Group ambayo ni Shirika la Mawasiliano la Kijeshi la Vietnam iliyo chini ya Wizara ya Ulinzi ya nchi hiyo.

### NCHI ZILIZOWEKEZA SANA UZALISHAJI JESHINI

Baadhi ya nchi zinazotegemea sana majeshi katika uwekezaji na viwanda zimefanikiwa kupunguza gharama nyingi za ulinzi na usalama. Baadhi ya nchi hizo ni:

1. Marekani - Ni nchi inayoongoza duniani kwa matumizi ya kijeshi. Sekta ya ulinzi na viwanda vya kijeshi kama vile Lockheed Martin, Boeing, na Northrop Grumman vinachangia sana uchumi na uwekezaji. Kwa hiyo wasiojua ni kwamba Boeng kimsingi ni kampuni ya kijeshi ingawa pia inatengeneza ndege za kiraia.
2. Urusi - Ina viwanda vya kutengeneza silaha kama vile Kalashnikov na Sukhoi na kuuza nje na hivyo vinachangia sana kwenye pato la taifa.
3. China - Ina sekta kubwa ya viwanda vya kijeshi na hutegemea kwa kiasi kikubwa teknolojia ya ulinzi kwa ajili ya kukua kwa uchumi wake. Kampuni kama AVIC (Aviation Industry Corporation of China) zinajihusisha na utengenezaji wa vifaa vya kijeshi lakini zipo kibao zinazotengeneza bidhaa za kiraia.
4. Israeli - Inajulikana kwa sekta yake ya teknolojia ya ulinzi na uvumbuzi wa kijeshi, ambayo inavutia wawekezaji wa ndani na nje. Kampuni kama Israel Aerospace Industries (IAI) zina mchango mkubwa.
5. Saudi Arabia - Inatumia sehemu kubwa ya pato lake kwa ununuzi wa silaha lakini sasa imeanza kuwekeza kwenye viwanda vya kijeshi kwa lengo la kujitegemea zaidi.
6. Korea Kusini - Kampuni kama Samsung Techwin na Hyundai Rotem zinahusika katika utengenezaji wa vifaa vya kiraia na kijeshi.

**Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 au 0784 122 020.**





# NHC inavyosaidia Watanzania makazi bora

**Na John Ngunge**

HAYATI Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere enzi za uhai wake alithamini vitu vitatu katika maisha ya Watanzania na hivyo moja ya falsafa ya utawala wake ilikuwa ni kuhakikisha mwananchi anapata vitu hivyo vitatu.

Vitu hivyo ni chakula, mavazi na malazi kama mambo ya msingi sana kwa maisha ya binadamu.

Katika makala hii, ningependa tuzungumzie suala la makazi, ambalo kwa mujibu wa aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba Nchini (NHC), Nehemiah Mchechu katika ukurasa wake wa mtandao wa X alipata kuandika kuwa wanamuenzi Mwalimu Nyerere kwa kujenga makazi bora. Mchechu sasa hivi ni Msajili wa Hazina.

Miongoni mwa huduma zinazotolewa na NHC ni kupangisha nyumba, kuuza nyumba za kipato cha chini ambazo ni rahisi na zenye ubora wa hali ya juu, ambazo zipo mikoa yote nchini.

Kwa mujibu wa mwongozo wa uhamasishaji ujenzi wa nyumba bora ngazi ya jamii uliotolewa na iliyokuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Desemba 2019, nyumba bora ni ile iliyojengwa kwa mpangilio mzuri na kutumia vifaa vya ujenzi vyenye ubora.




Mkurugenzi Mkuu NHC, Hamad Abdallah.

Mwongozo unaeleza nyumba hiyo inatakiwa kuwa na madirisha yanayopitisha mwanga na hewa ya kutosha, iliyoezekwa vizuri na yenye choo bora.

Kwa mantiki hiyo, NHC inatakiwa kuendelea na jitihada zake za kukuza maendeleo ya makazi nchini kwa lengo la kuhakikisha kuwa wakazi wa mikoa yote wanapata fursa ya kipekee ya kumiliki nyumba bora hivyo kuwafanya washiriki katika ukuaji wa uchumi.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu, Hamad Abdallah, NHC lina jukumu la kuhakikisha wananchi wanapata makazi bora na hilo lilibainika katika mazungumzo yake na Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu mwezi uliopita.

Ni ukweli usiopinda kwamba haki ya msingi ya malazi ni kubwa na ya lazima nchini na hii inatokana na Ripoti ya Sensa ya Watu na Makazi ya 2022, kuonesha kuwa Tanzania imefikisha idadi ya watu milioni 61.7.

Idadi ya watu inaongezeka kila uchao na ongezeko hilo linalichagiza shirika kufanyakazi kibiashara huku likiekeleza mipango endelevu ya malengo yake.

Wote wenye mavazi na chakula wanahitaji malazi na siyo malazi tu, bali malazi bora.

Malazi yanaweza kuwa kwenye nyumba wanazozimiliki wenyewe au za kupanga.

Takwimu katika sensa hiyo inaonesha kaya zinazomiliki nyumba Tanzania Bara ni 8,865,242 sawa na asilimia 64.3.

Inaonesha kaya zinazomiliki nyumba kwa upande wa vijijini ni 6,328,170 sawa na asilimia 75.7 wakati kaya zinazomiliki nyumba maeneo ya mijini ni 2,537,072 sawa na asilimia 46.8.

Pia zinaonesha asilimia 64.8 ya kaya zilizopo Tanzania Bara zinaishi katika nyumba wanazozimiliki wenyewe na asilimia 20.2 ya kaya zinaishi katika nyumba binafsi za kupanga.

Asilimia ya kaya zinazoishi katika nyumba wanazomiliki katika maeneo ya vijijini ni kubwa (75.8%) ikilinganishwa na maeneo ya mijini (47.9%).

Wamiliki wengi wa nyumba wamezijenga wenyewe, wengine wamezinunua kwa njia ya mikopo au kununua kwa fedha taslimu. Wapo ambao kutokana ukosefu wa fedha za kutosha na kukosekana kwa viwanja katika maeneo wanayoishi wanashindwa kujenga nyumba, hivyo, wakajikuta wakilazimika kupanga nyumba za watu binafsi au za mashirika, hususan NHC.

Ili kutekeleza azma ya shirika ya kuuza nyumba kwa gharama nafuu, linaweza kufanya mambo matatu; Moja kujenga lenyewe, mbili kutafuta watu watakaoingia nao ubia, na tatu matumizi ya teknolojia ya kisasa katika ujenzi.

Mwaka jana, Chuo Kikuu Ardhi (ARU), kupitia taasisi yake ya Utafiti ya Nyumba walibuni teknolojia ya ujenzi wa gharama nafuu kwa kutumia matofali ambayo ni rafiki kwa mazingira.

Tofali hizi hutengenezwa kwa kutumia udongo wa mfinyanzi, saruji na maji kidogo na huwa imara kwa matumizi mbalimbali ya shughuli za ujenzi.

Ni vyema utaalamu huu ukasambazwa na kuchukuliwa na wadau ikiwemo NHC ili kuwapatia Watanzania makazi bora kwa gharama nafuu zaidi.

# TCRA na kampeni muhimu ya usalama mtandaoni




**Na Mwandishi Wetu**

MATUMIZI ya mitandao ni muhimu sana katika zama za sasa kwa sababu yanawezesha mawasiliano ya haraka, upatikanaji wa taarifa na pia ni rahisi kufanya biashara kwa njia ya mitandao.

Mitandao inasaidia kuunganisha watu duniani kote, kukuza elimu kwa kutoa fursa za kujifunza kwa njia ya mtandao (mfano elimu mtandaoni), kuboresha huduma za afya kupitia telemedicine, na kuimarisha biashara kupitia biashara za mtandao (e-commerce). Pia, mitandao imerahisisha ushirikiano wa kijamii kupitia majukwaa kama vile mitandao ya kijamii kama WhatsApp, Facebook, Jamii Forum, Instagram na kadhalika. Kwa hiyo mitandao ni elimu, maarifa lakini pia mitandao ni uchumi.

**USALAMA KWENYE MITANDAO**

Hata hivyo, usalama wa mitandao ni suala nyeti kutokana na hatari nyingi zinazowakumba watumiaji. Baadhi ya hatari hizo ni kama vile udukuzi, wizi wa taarifa binafsi, utapeli, upotoshaji, na usambazaji wa virusi vya kompyuta.



**Mkurugenzi Mkuu TCRA, Dk. Jabiri Bakari**

Hatua za usalama ambazo watumiaji wanapaswa kuchukua ni pamoja na kutumia nywila (password) ngumu, kuhifadhi taarifa kwa kutumia mbinu za usimbaji wa data (encryption), matumizi ya programu za kinga kama firewalls na antivirusi, na elimu kwa watumiaji juu ya kutofungua viunganishi visivyoaminika au kushiriki taarifa binafsi bila tahadhari.

Athari za kutokuwepo kwa usalama mtandaoni kunaweza kusababisha athari mbaya kama wizi wa fedha kupitia akaunti za kibenki, upotevu wa data muhimu kwa biashara au watu binafsi, utapeli wa mtandaoni na pia uharibifu wa sifa za watu au taasisi. Athari hizi zinaweza pia kudhoofisha maendeleo ya kidijitali na kuharibu uaminifu wa matumizi ya mitandao.

**TCR YACHUKUA HATUA**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imezindua kampeni ya "Ni Rahisi Sana" ili kuhamasisha mambo mbalimbali kwa ajili ya usalama wa matumizi ya mitandao.

Baadhi ya vitu vinavyohamasishwa na kampeni hii ni usajili wa laini za simu kwa njia sahihi na salama. Kampeni hii pia inalenga kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa usajili wa namba za simu kwa kutumia

>>>Inaendelea Uk. 26



# TASAC: Ni shirika lenye majukumu muhimu kwa Taifa

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (Tanzania Shipping Agencies Corporation -TASAC) ambalo ni mdau muhimu katika usafiri wa majini, lina majukumu kadhaa nyeti na ndio maana limeendelea kutoa elimu kwa Watanzania ili kushirikiana nalo katika kuunga mkono juhudi mbalimbali zinazofanywa na shirika hilo.

Hata makala hii inavyoadikwa sasa, Tasac inaendelea kutoa elimu katika Maonesho ya 7 ya Kitaifa ya Madini yanayoendelea pale Viwanja vya Bombambili, Geita, yaliyoanza Oktoba 2 na kilele ni kesho Oktoba 13, 2024, ambapo Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Kwa wale ambao watafika kwenye maonesho hayo leo na kesho wasikose kutembelea Banda la Tasac kwani kuna mengi ya kujifunza.

Moja ya majukumu ya Tasc ni kudhibiti shughuli za usafiri na usafirishaji wa majini. Ikumbukwe kwamba usafiri wa maji ni sekta muhimu kabisa katika kukuza uchumi wa Taifa. Bidhaa nyingi zimekuwa zikisafirishwa kupitia njia ya maji; baharini, mitoni na kwenye maziwa, hususani mizigo mikubwa kama magari na mashine mbalimbali.

Ikumbukwe pia kwamba Tanzania ni nchi ambayo imezungukwa na maji kwa sehemu kubwa, jambo ambalo linafanya watu wengi kutumia usafiri wa vyombo vya majini ili kwenda sehemu moja hadi nyingine na kusafirisha bidhaa zao. Mbali na Bahari, Tanzania imezungukwa na maziwa makubwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa.

Kupitia usafiri wa majini, inaelezwa kwamba Tanzania ni nchi pekee Afrika ambayo inazungukwa na nchi nyingi ambazo hazipakani na Bandari (Land locked countries) kama Uganda, Malawi, Zambia, Rwanda na Burundi. Pia inategemewa na baadhi ya maeno ya nchi zenye bahari kama Msumbiji, Comoro na Kenya.

Pamoja na kutumia maji kama sehemu ya usafiri lakini maji yametumika kama sehemu ya kupata ajira kupitia uvuvi na ulimaji wa mazao kama mwani. Hivyo serikali ikaona umuhimu wa kuwa na chombo hiki cha kudhibiti shughuli hizo za usafiri na usafirishaji kwa njia ya maji ili kuwa na tija kubwa zaidi.

Tasac pia ina jukumu la kusimamia ulinzi na kuzuia uchafuzi wa mazingira kutokana na shughuli za vyombo vinavyotumika majini.

Kwa kifupi sana tunaweza kusama kazi kuu tatu za msingi za shirika hili kisheria ni kuboresha huduma za usafirishaji wa majini; kuboresha usalama wa usafiri wa majini, usalama na ulinzi na utunzaji wa mazingira ya bahari na maziwa pamoja na huduma za biashara za meli.

Kwa hiyo utaona Tasac ni 'dude' lenye mambo mengi sana ya kujadili, lakini kwa leo katika makala haya tutazungumzia suala la usalama majini tena kwa kifupi tu.



**Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), Bw. Mohamed Malick Salum**

### USALAMA WA MAJINI

Katika miezi ya karibuni, katika mikoa ya Mwanza na Mara kumetokea ajali majini ambapo watu kadhaa wamepoteza maisha pamoja na mali kupotea. Pengine maafa yasingekuwa makubwa kama vyombo hivyo na wahusika waliokuwemo wangekuwa wakifuata vilivyo sheria na hasa kufanyia kazi elimu inayotolewa mara kwa mara na Tasac.

Shirika limekuwa likiwataka wananchi kusajili vyombo hivyo na kutopanda vyombo ambavyo havijasajiliwa na pia kuhakikisha kila chombo cha majini ikiwemio mitumbwi inakuwa na vifaa vya kujiokolea (life jackets) endapo kukitokea ajali.

Shirika katika maeneo mbalimbali linakoshiriki yakiwemo maonesho limekuwa likitoa rai kwa wananchi, kuzingatia masuala ya usalama wanapokuwa wanatumia vyombo vya majini. Hii ni pamoja na waendesha usafiri na wanaomiliki vyombo hivyo kuhakikisha vinakuwa katika hali nzuri lakini pia, kama ilivyoelezwa hapo awali, vinakuwa na vifaa vya kwa ajili kuokoa maisha ya watu endapo itatokea ajali.

Ni kutokana na hilo, ndio maana Tasac iko kwenye maonesho ya madini Geita ikiendelea kutoa elimu hii muhimu ili wakati wote watumiaji wa usafiri wa majini wajue jinsi ya kujiandaa na dharura na changamoto zozote zinazoweza kujitokeza wanapokuwa kwenye maji.

Hii si kuwa tu na vifaa husika bali pia kujua matumizi sahihi ya vifaa vya kujiokoa ambavyo vinatakiwa viwepo kwenye meli, boti na mitumbwi lakini pia idadi ya abiria ambao wanapaswa kuchukuliwa na boti, meli na hata mitumbwi.

Mwishoni mwa mwezi uliopita (Septemba) Tasac pia ilikuwa mkoani Mara kushiriki kikamilifu katika maadhimisho ya Wiki ya Usafiri wa Majini, na hasa kwa kuzingatia kwamba mkoa huo una eneo kubwa ambalo linazungukwa na Ziwa Victoria.

Bila shaka wananchi wengi wa mkoa huo, hususani pale Musoma Mjini walipata elimu

>>>Inaendelea Uk. 26



# TCRA na kampeni muhimu ya usalama mtandaoni

>>>Inatoka Uk. 24

alama za vidole ili kuepuka utapeli, udukuzi na matumizi mabaya ya huduma za mawasiliano.

Pia, TCRA inasisitiza umuhimu wa usalama wa data binafsi na kuhakikisha kuwa watu wanajua namna ya kutumia huduma za mawasiliano kwa usahihi na kwa faida bila kuathiri usalama wao au wa wengine.

Katika kampeni hiyo, TCR inahimiza Watanzania kuzingatia mambo yafuatayo kila wakati: Kutumia nywila imara ambayo si rahisi mtu kuiiga (strong password), kuepuka kumshirikisha mtu yeyote nywila yako, kupakua program rununu (apps) kutoka vyanzo vinavyoaminika, kuhakikisha kifaa chako cha mawasiliano kinahuishwa mara kwa mara (updated) na kuepuka kutuma taarifa zako bunafsi kwenda kwa mtu usiyemfahamu.

### TANZANIA MFANO WA KUIGWA

Tanzania imepiga hatua kubwa katika usalama mtandaoni, ikiorodheshwa kati ya nchi bora barani Afrika kwenye Global Cybersecurity Index (GCI) ya mwaka 2024 iliyoandaliwa na International Telecommunication Union (ITU).


Tanzania ipo katika Tier 1, ambayo ni kundi la nchi zinazoonekana kama "mfano wa kuigwa" katika usalama wa mtandao. Nafasi hii inatokana na utendaji mzuri wa Tanzania katika maeneo matano muhimu: mifumo ya kisheria, hatua za kiufundi, miundo ya kiutawala, maendeleo ya uwezo, na ushirikiano.

1. Mifumo ya Kisheria: Uwepo wa sheria na sera za kitaifa zinazohusu usalama mitandaoni, kama vile sheria za makosa ya mtandaoni, kulinda taarifa za mtumiaji, na vitendo vya uhalifu wa kidijitali.

2.Hatua za kiufundi: Kinachoangaliwa kingine ni uwepo wa taasisi na miundombinu ya kiufundi inayohakikisha usalama wa mtandao, kama vile Computer Emergency Response Teams (CERTs) na mifumo ya kudhibiti na kupambana na uhalifu wa mtandaoni.

3.Miundo ya kiutawala: Uwezo wa nchi katika kupanga, kuongoza, na kuratibu sera za usalama wa mtandao kupitia mipango ya kitaifa au kamati maalum zinazohusika na usalama wa mitandao ni jambo lingine linaloangaliwa na Tanzania iko vyema.

4.Mzaendeleo ya Uwezo (Capacity Building): Namna ya kuimarisha uwezo wa rasilimali watu kupitia elimu, mafunzo, na kuongeza ujuzi wa watu wanaohusika na usalama mitandaoni ni jambo lengine ambalo Tanzania kupitia TCRA imekuwa ikifanya.




5. Ushiriakiano (Cooperation): Ushirikiano wa kitaifa na kimataifa katika kushirikisha taarifa na uzoefu wa kiusalama wa mitandao, pamoja na kushiriki katika mipango ya ushirikiano na mashirika mengine duniani ni jambo lingine ambalo limeibeba Tanzania.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imekuwa na mchango mkubwa katika jitihada hizi, hasa kupitia kuanzishwa kwa Kikosi cha Dharura cha Usalama Mtandaoni cha Tanzania (TZ-CERT), ambacho kinashughulikia matukio ya usalama wa mtandao katika ngazi ya kitaifa. Mafanikio haya yanaonekana kuwa msingi muhimu kwa ukuaji wa kidijitali wa Tanzania, huku lengo likiwa ni kujenga mifumo ya ICT iliyo salama na ya kuaminika.

### NCHI ZILIZO CHINI KIUSALAMA

Wakati Tanania inapiga hatua katika suala la usalama mtandaoni, nchi zinazokabiliwa na changamoto kubwa za usalama mtandaoni zinajumuisha Honduras, Haiti, na Bolivia, ambazo zimepata alama za chini sana katika Global Cybersecurity Index ya 2024.

Nchi hizi zina upungufu mkubwa katika utekelezaji wa sera za usalama wa mtandaoni, rasilimali za kiufundi, na uimarishaji wa uwezo, hali inayoathiri usalama wa miundombinu yao ya kidijitali.

Kwa upande mwingine, Nigeria pia imeorodheshwa kuwa na usalama wa chini mtandaoni kutokana na changamoto kama utekelezaji duni wa sera za usalama wa mtandaoni, ukosefu wa ufadhili wa kutosha, na miundo ya kisheria ambayo haijaboreshwa kushughulikia vitisho vya kisasa kama udukuzi wa akili unde (AI).

# TASAC: Ni shirika lenye majukumu muhimu kwa Taifa

>>>Inatoka Uk. 25

nzuri kuhusu usalama wa vyombo vya usafiri katika maji, usalama katika mialo na hata usalama katika visiwa.

Mbali na kutoa elimu, Tasac imekuwa ikifanya ukaguzi wa mara kwa mara na hiyo ni sehemu ya kazi ya msingi, lengo likiwa ni kuhakikisha usalama wa raia wa na mali.

Maeneo ambayo Tasac imekuwa ikifanya udhibiti masuala ya usalama ni kwenye bandari mbalimbali nchini. Mbali na bandari za kwenye maziwa na bahari, Tasac pia inafanya udhibiti kwenye bandari kavu.

Kwa maana hiyo waendesha bandari kavu ni kundi lingine ambalo Tasac imekuwa ikidhibiti shughuli zao katika kutoa huduma za bandari kavu hasa kwenye mizigo ambayo inaingia

### HISTORIA FUPI

Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania Sura ya 415 na kuanza kutekeleza majukumu yake rasmi kuanzia tarehe 23 Februari, 2018 kufuatia Tangazo la Serikali Na. 53 la tarehe 16 Februari, 2018.

Kama ilivyodokezwa hapo awali majukumu ya Shirika ni pamojka na kusimamia na kudhibiti sekta ya usafiri wa majini, kuwezesha biashara ya usafirishaji majini na kufanya biashara ya uwakala wa meli.

Misingi Mikuu ya kuanzishwa kwa Shirika ni kuwajibika kwa Taifa na kwa wadau katika kutekeleza mamlaka na makujumu yaliyo chini ya dhamana ya Shirika; Kuwa mfano wa kuigwa katika mwenendo wa kufanya kazi kwa uaminifu na uadilifu kwenye shughuli zote; Kutumia mkabala unaodhihirisha utaalamu katika weledi, mwenendo, mtazamo na tabia; Kutokuwa na upendeleo katika kuhudumia wateja, watoa huduma na wadau wengine kwa kutoa huduma bila ya upendeleo wala ubaguzi; Kuwa wazi katika shughuli zote na kuwa tayari kupokea maoni ya wananchi.

Makao makuu ya TASAC yapo Dar es Salaam na ofisi nyingine zipo katika mikoa ya Mwanza, Tanga, Kigoma, Rukwa, Mtwara, Geita, Kagera, Mara, Lindi, Mbeya-Kyela na Mwanza-Ukerewe. Tasac pia ina ofisi za Mipakani zipo mikoa ya Kilimanjaro (Holili), Kahama, Tunduma na Sirari (Mara).



# Ukombozi wa Afrika na Mwalimu Nyerere

**Na Hamid Yassin**

JUNI 22 mwaka huu 2024, Rais wa Guinea-Bissau, Umaro Sissoco Embaló alikuwa hapa nchini kwa ziara ya kikazi na hakusita kusema kuwa, wakati wakiwa watoto wadogo shuleni kwao walifundishwa kumjua Rais wa kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye aliongoza harakati za ukombozi wa nchi za Afrika.

Embalo alikiri kuwa, miongoni mwa mataifa yaliyonufaika na juhudi za Mwalimu Nyerere ambaye tunaadhimisha maka 25 tangu afariki dunia, ni lao la Guinea-Bissau ambapo alisema Mwalimu alimsaidia kiongozi wao aliyeongoza mapambano ya kudai uhuru wa taifa lao, Amilcar Cabral.


Akiongea mbele ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassani Ikulu Dar es Salaam hiyo Juni 22, Rais Umaro alisema kuwa Guinea-Bissau na Tanzania walishirikiana pamoja katika kuondoa ukoloni na ubaguzi wa rangi na ilikuwa ni hapa Dar es Salaam ambapo Kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Afrika ilipokuwa na Makao Makuu na kwa mchango mkubwa wa Serikali ya Tanzania Kamati hiyo iliweza kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha nchi zote za Afrika zinajipatia uhuru wake kamili ikiwemo Guinea-Bissau.

“Niko hapa kutoa heshima kwa Mwalimu Julius Nyerere ambaye mwaka 1976 alitembelea nchi yetu na akapewa medali ya heshima na alikuwa Rais wa kwanza kutoka nje ya nchi yetu kupewa medali hiyo kutokana na mchango wake wa kuleta haki, heshima na maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa nchi za Afrika,” alinena Rais Umaro.

Rais Umaro aliongeza kuwa, mataifa ya Afrika yakifanya kazi pamoja yana jukumu muhimu la kuandaa mustakabali wa Dunia; na kusisitiza kwamba Bara hili kuna rasilimali nzuri, kuna uongozi sahihi ambao unaweza kuleta ustaarabu mpya wa dunia, na kwamba inatakiwa dunia yenye usawa zaidi, heshima zaidi, yenye jukumu la pamoja kati ya mataifa makubwa na madogo.

“Tuko hapa leo tuna furaha kubwa na dada yangu (Rais Samia), kwa sababu tukiwa hapa tunajiona tuko nyumbani, tupo nchi ya kwanza ya Ukombozi wa Afrika, viongozi wote waliopigania uhuru walikuwa hapa, ni muhimu sana,” alinena Rais Umaro na kuongeza.

“Kubadilisha mahusiano yetu yawe imara zaidi, kule Guinea-Bissau kamwe hatutosahau kuhusu Tanzania wakati tukiwa watoto wadogo shuleni walitufundisha kumjua Rais wa kwanza aliyemchukua Cabral ambaye alikuwa Mwalimu Julius Nyerere, yeye ataendelea kukumbukwa daima hatutomsahau, sisi tupo tayari kuwasaidia mkituhitaji ndio maana leo nipo hapa.”



Naam, kama hata mataifa ya kigeni ndani ya Bara hili la Afrika wanatambua mchango wa Tanzania katika ukombozi wa bara letu kupitia Rais wetu wa kwanza, hayati Mwalimu Nyerere, kwa nini tusiwapuuze wanasiasa uchwara na wanaharakati wa nchi hii wasiochoka kumsema vibaya Baba wa Taifa letu ambaye mwezi huu anatimiza miaka 25 tangua atutoke Oktoba 14, 1999.

Hakuna siri kuwa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania tangu wakati wa Mwalimu Nyerere ilijitoa mhanga kuwapokea, kuwahudumia, kuwahifadhi na kuwasaidia kwa hali na mali Wapigania Uhuru wa nchi nyingi duniani hasa wa ukanda wa Kusini mwa Afrika.

Mwalimu Nyerere katika moja na nukuu zake aliwahi kusema kuwa; “Uhuru wa Tanzania hautakuwa na maana yeyote kama nchi zinazotuzunguka na binadamu wenzetu popote pale duniani hawako huru”.

Katika muktadha huo juhudi za Tanzania ya Mwalimu Nyerere, ziliwezesha kufanyika kwa Mkutano Mkubwa wa PAN African Frontline Movement of East Central and Southern Africa (PAFMECA), katika Jiji la Mbeya, ambapo aliyekuwa Rais wa Zimbabwe, hayati Robert Mugabe alifanya mikutano yake ya harakati.

Mwalimu Nyerere alipopata fursa katika Mkutano wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (enzi hizo OAU) alipokua madarakani, aliwasilisha ajenda ya ukombozi, ambapo kwa pamoja nchi zilizokuwa huru za Afrika, wakaazimia Tanzania kuwa kitovu cha ukombozi wa Mashariki na Kusini mwa Bara la Afrika.

Tangu wakati huo nchi ambazo hazikuwa huru, hapa Tanzania pakawa nyumbani kwao na waliwezeshwa kupata misaada mbalimbali kutoka nchi wanachama wa OAU, pamoja na nchi za Scandinavia, China, Cuba na Urusi. Nchi hizo ambazo zilikuwa hazijapata uhuru miaka ya sabini hadi tisini mwanzoni, ni pamoja na Afrika ya Kusini, Angola, Comoro, Msumbiji, Namibia na Zimbabwe.

Aidha, baadhi ya nchi zilikua huru lakini ziliandamwa na migogoro ya hapa na pale, na kuzalisha makundi makubwa ya wakimbizi waliokimbilia na kuishi Tanzania ni pamoja na Malawi, Burundi, Rwanda, Kongo DRC na Uganda.

Pia, Tanzania ilishiriki kuunga mkono wapigani uhuru wa Polisario wa Morocco na Palestine Liberation Organization (PLO) wa Palestina.

Kutokana na historia ya Ukombozi, Tanzania inalazimika kutambua na kuweka kumbukumbu, kuhifadhi na kuutangaza ili isifutike kwa wale wote waliopata uhuru na ambao ili historia ya uhuru wao ikamilike ni lazima kuitaja Tanzania kama rafiki aliyesaidia wao kujikomboa.

Kutokana na umuhimu wa Tanzania katika ukombozi wa Bara la Afrika hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara, ni vyema sasa urithi wa utalii wa ukombozi wa bara hili ukaenziwa na kuhifadhiwa ili kwa manufaa ya wanufaika yaani nchi zilizopigania uhuru wao wakiwa uhamishoni Tanzania, na hata Watanzania wenyewe.

Yapo majina makubwa nje ya Tanzania ambayo wahusika katika kupigania uhuru wakiyasikia wanakumbuka enzi za harakati, mfano Waziri Mkuu Mstaafu Dk. Salim Ahmed Salim, Hayati Brigedia Hashim Mbita na wengineo wengi ambao walizikwa katika makaburi ya mashujaa ya Nachingwea, Mtwara, Kongwa, Mgagao Iringa, Mazimbu, Dakawa Morogoro, Bagamoyo.

Mwalimu Nyerere alianzisha Kambi za wapigania uhuru maeneo ya Kongwa Dodoma, Kihesa Mgagao na Chuo cha Mkwawa Iringa, Kingoluwira, Kituo cha Maendeleo cha Solomon Mahalangu Mazimbu na Dakawa Morogoro. Kaole Bagamoyo, Makongorosi Chunya na eneo la Mwanjelwa Mbeya.

Tanzania pia ilikua kitovu cha vyama vikuu vya ukombozi barani Afrika ambapo kulikuwa na ngome za African National Congress -ANC, Pan African Congress-PAC, Movement for People Liberation of Angola - MPLA cha Augustino Neto wa Angola, Zimbabwe African National Union – ZANU cha Robert Mugabe na Ndambaningi Sithole, pamoja na wapiganaji wao wa Zimbabwe National Liberation Army –ZANLA.

Aidha, Tanzania pia ilikuwa ngome ya Chama cha Ukombozi cha Msumbiji cha FLERIMO, cha Edward Mondlane na baadaye hayati Samora Machel na chama cha Namibia cha Southern West Africa People’s Organization (SWAPO) cha hayati Sam Nujoma.

Vyama vya wapambanaji vilivyokuwa chini ya vyama vya siasa kama vile Zimbabwe People Revolutionary Army (ZIPA), Zimbabwe African National Liberation Army (ZANLA), Front for Liberation of Zimbabwe (FLORIZ) cha hayati Herbert Chitepo na Shamuyarira nao waliishi katika makambi nchini Tanzania.

Umuhimu wa historia ya ukombozi wa Afrika pia unadhihirika kwa Tanzania, kutokana na viongozi Wakuu wa vyama vya ukombozi kama hayati Samora, hayati Edward Mondlane, hayati Augustine Neto, hayati Robert Mugabe, Thabo Mbeki, Jacob Zuma, hayati Nujoma na wengineo kuishi hapa nchini. Aidha, wengine kama Rais wa sasa wa Zimbabwe Emmerson Mnangwaga aliishi eneo la Kaole Bagamoyo.

Uwepo wa makambi ya wapigania uhuru hapa nchini, kuliwaunganisha wao na Watanzania kuwa kama ndugu na ukarimu wao uliwafanya kuchanganyika kiasi kwamba haikuwa rahisi kutofautisha yupi ni Mtanzania na yupi mpigania uhuru.

Tanzania pia ina historia ya Ukombozi wa Afrika ambapo katikati ya Jiji la Dar es Salaam kuna Ofisi ya Kamati ya Ukombozi Barani Afrika iliyopo barabara ya Garden Avenue pembeni ya Ubalozi wa Msumbiji. Pia, katika mitaa ya Kaluta na Samora kulikua na Ofisi za Chama cha Ukombozi cha Namibia (South West Africa People Organization - SWAPO).

Aidha, katika barabara ya Nkurumah mkabala na Co - Cabs kulikuwa na ofisi za Makao Makuu ya FRELIMO na baadaye zikawa ofisi za urafiki wa Tanzania na Msumbiji, TAMOFA, ambapo ofisi hizo zilitumika sana na Rais Samora wa Msumbiji.

Pia Barabara ya Nkurumah eneo la Gerezani katika majengo ya Shirika la Nyumba la Taifa kulikuwa na ofisi za African National Congress (ANC). Hata hivyo, kituo kikubwa cha kupakulia na kupakia silaha kilikuwa eneo la kituo cha mwendo kasi cha mabasi cha Jiji.

Eneo la Posta ya zamani kitalu namba 331/36 mtaa wa Mkwepu ilikuwa ofisi ya PAC na ANC, eneo la Kariakoo Mtaa wa Chagga zilikuwa Ofisi za chama cha wapigania uhuru wa Comoro, MOLINACO. Eneo la Kisutu kulikuwa na Hoteli aliyokuwa anakula Edward Mondlane na Samora Machel.

Kituo cha Polisi Ikaka, mtaa wa Pangani na Shaurimoyo kulikuwa na majengo ya wapigania uhuru wa FLERIMO. Pia, Mahakama ya Kisutu jengo la zamani mbele walikaa wapigania uhuru wa ANC, ambapo Barabara ya Mandela eneo la Buguruni mtaa wa Madenge eneo la Mahakama kulikuwa na Kambi ya wapigania Uhuru wa Afrika ya Kusini wa chama cha ANC.

Kufanikiwa kwa baadhi ya nchi Kusini mwa Afrika kuwa huru, ikapelekea kuzaliwa kwa Taasisi ya Kuratibu Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADCC) ambayo ilibuniwa Jijini Arusha nchini Tanzania mwaka 1979 na mwasisi wake ni hayati Mwalimu Nyerere ambapo alishirikiana na Marais Kenneth Kaunda wa Zambia, Samora Machel wa Msumbiji, Sir Seretse Khama wa Botswana na Augustino Neto wa Angola (wote hao wametangulia mbele ya haki hivi sasa).

Tanzania pamoja na nchi nyingine nane, zilitia saini tamko kuanzishwa rasmi SADCC ambapo jukumu kubwa lilikuwa kuhamasisha umoja wa kisiasa ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi husika. Mnamo mwaka 1992 ambapo Mwalimu Nyerere alikuwa mwenyekiti wa Tume ya Kusini iliyohamasisha SADCC kuwa Jumuia ya Maendeleo ya Uchumi Kusini mwa Afrika ‘Southern Africa Development Cooperation’, SADC.

Urithi huo mkubwa wa ukombozi wa Kusini mwa Afrika ambao upo Tanzania, ukihifadhiwa na kuimarishwa vizuri utachochea ukuaji wa utalii wa kihistoria na utaiwezesha Tanzania sio tu kupaa kimapato bali kuwa sehemu muhimu ya kihistoria hasa ya ukombozi wa nchi za Kusini.

*Kwa maoni na ushauri;*
*0768 888 787 ama 0784 122 020.*

# Ziara za Rais Dk. Samia zinavyowanufaisha wasanii

## ● Wamepata fursa Korea na Uturuki, kazi kwao kujikwamua kiuchumi

**Na Hamid Yassin**







TANZANIA ilichaguliwa kuwa nchi ya kwanza Afrika kufanya filamu na Korea Kusini. Wasanii wetu kadhaa wa tasnia ya maigizo walikwenda Korea na Uturuki Julai mwaka huu kupata mafunzo na kujionea jinsi wenzao walivyopiga hatua kubwa kwenye fani hiyo.

Tanzania kuwa nchi ya kwanza Afrika kufanya filamu na waigizaji nguli wa Korea Kusini yalibainishwa na Rais wa Filamu wa taifa hilo, Yang Jongkon wakati akizungumza na waigizaji hao wakubwa kutoka Tanzania katika mji unaoongoza kwa filamu duniani ujulikanao kama Busan.

Hiyo fursa ilikuja baada ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuwaunganisha wasanii wa Tanzania na wale wa Korea Kusini kufutia ziara yake aliyoifanya nchini humo kuanzia Mei 30, 2024 hadi Juni 06, mwaka huu 2024.

“Rais Dk. Samia amefanya kazi kubwa ya kuunganisha soko la filamu la Tanzania na Korea Kusini, basi nami sina budi kusema wazi kuwa Tanzania ndio itakuwa nchi ya kwanza tutakayoshirikiana nayo tutakapoingia Afrika. Kwa sasa tunamalizia kuimarisha bara la Asia kwenye tasnia hii ya filamu,” alizungumza Jongkon katika siku ya tatu katika ziara ya kujifunza kwa waigizaji wetu huko Korea Kusini.

Rais Jongkon aliahidi kuja Tanzania kuonana na wasanii wa Tanzania akiongozana na baadhi ya watengeneza filamu wa Korea Kusini.

Nao wasanii kutoka Tanzania walifanikiwa kutembelea Studio kubwa za Busan na kuona jinsi filamu za Kikorea ambazo zimetokea kupendwa sana na Watanzania zinavyotengenezwa.

Filamu hizi maarufu zinazotambulika kama Kdrama (Korean drama) zimetokea kuiteka dunia na kuiweka Korea Kusini juu kabisa katika masoko ya filamu kimataifa.

Wakati Rais huyo wa waigizaji, Jongkon akizungumza hayo mjini Busan, alikazia kuwa, atahakikisha anaendelea kuudumisha na kuimarisha uhusiano mzuri sana uliopo kati ya Tanzania na Korea Kusini.

Pia ameshukuru sana kwa zawadi kutoka kwa Rais Dk. Samia ambayo ilikabidhiwa na kiongozi wa msafara huo wa wasanii Steve Nyerere.

Wasanii hawa wa Tanzania pia walipata fursa ya kukutana na nyota mkubwa sana wa Korean drama, Son Ye-jin.

Balozi wa Tanzania Korea Kusini, Togolani Edriss Mavura ndiye aliyewaunganisha na Son Ye-jini wasanii hao aliowaalika kufanya ziara Korea Kusini kwa ajili ya kuimarisha mahusiano na kubadilishana ujuzi katika soko la filamu.

Wasanii hao walikutana na Son Ye-jin kubadilishana mawazo na kisha kukaa na watengeneza filamu wakubwa Cheol-ha Lee na Yohwan Kim.

Bahati iliyoje kwa waigizaji hawa, kwani Muongoza filamu mkubwa (Director) Cheol-ha Lee alisema yupo katika maandalizi ya filamu itakayohusisha waigizaji wa kimataifa na angependa kupata mwigizaji kutoka Tanzania kwa Afrika.

Katika kikao hicho walitoa mawazo mbalimbali ikiwemo serikali kuweka nguvu katika kuinua wasanii wadogo kwa makusudi kabisa.

Bahati nyingine nzuri kwa waigizaji wetu ni kwamba, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ametoa mwaliko kwa waigizaji hao wa Korea Kusini kuja Tanzania kuchagua maeneo mbalimbali ya kufanyia filamu zao na kisha kutembelea vivutio vyetu vya kitalii.

Nao waigizaji wa Korea Kusini walishukuru sana kwa zawadi za shuka za Kimasai walizovalishwa na kiongozi wa msafara huo, Steve Nyerere, msanii Irene Uwoya na Blandina Chagula (Johari).

Naam; hii ilikuwa fursa nyingine hadimu kwa wasani wetu, huko nyuma haijapata kutokea kwa waigizaji wetu kutembelea nje ya nchi mfululizo namna hii katika kipindi kifupi tu cha mwezi mmoja.

Kumbuka walikuwa huko mwezi Juni pale walipoambatana na Rais Dk. Samia na fursa kama hii ya kukutana na wasanii wenzao nguli katika tasnia hii ya maigizo ya filamu.

Naamini walitumia fursa hizi kujifunza masuala mbalimbali yanayohusiana na uigizaji wa filamu kuliko kugeuza kama mtoko tu wa kutalii huko ughaibuni!

Katika ziara ile ya Korea Kusini waigizaji wetu walipata fursa ya kukutana na mwigizaji gwiji wa kike, Son Ye-jin ambaye analipwa shilingi bilioni moja kwa kila filamu anayoshiriki kule Korea Kusini achilia mbali kwenye nchi nyingine kubwa anazoalikwa kucheza filamu duniani!

Shilingi za Kitanzania bilioni moja kwa filamu! Hapa Wasanii wetu wana kitu kikubwa sana cha kujifunza kutoka kwa dada huyu wa Kikorea na naamini walitumia nafasi ile ya kukutana naye kumuuliza maswali mengi kwa nia ya kujua alifikaje hapo.

Tumezoea kusikia wasanii wetu wakilia kudhulumiwa na waandaaji wao wa filamu ama kulipwa mapato kidogo, hapa ndiyo mahali sasa pa kujifunza kutoka kwa akina Son Ye-jin, wanafanyaje kuepuka vikwazo hivyo.

Moja kubwa ni kuwa na menejimenti na wasimamizi wazuri sambamba na kuwaongoza vema katika kufuatilia haki za kazi zao, kuwasimamia katika kuingia mikataba stahiki na waandaaji wa filamu ili kuepuka malalamiko ya kudhulumiana ya mara kwa mara.

Lakini pia mafanikio kamwe hayawezi kuja kwa kazi za kulipua ama za kuiga kutoka mataifa mengine. Lazima wasanii wetu wajikite kwenye kuandaa kazi za maana zitakazojiuza kirahisi sokoni.

Kubwa kuliko yote ni kujisajili kwa mamlaka husika ili wawe na hatimiliki za kazi zao, kwani hii itawafanya watambulike na kupata vipato vya ziada za kazi zao kama vile mirabaha inayotolewa na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na Bodi ya Filamu nchini.

Na mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, ni kumshukuru Rais Dk. Samia kwa kuwaunganisha wasanii hawa wa Tanzania na wenzao wa nchi zilizoendelea katika utengenezaji wa filamu za kimtaifa.

**Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 au 0784 122 020.**

# Dk. Samia; Mwamba wa kupigania tamaduni, mila na maadili yetu

**Mwandishi Maalumu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan amewataka Watanzania wote, kila mmoja kwa nafasi yake, kukagua hali ya maadili katika nyumba yake kutokana na kuwepo kwa mmomonyoko mkubwa wa maadili katika jamii.

Rais ametoa mwito huo katika Uwanja wa CCM Majimaji, Songea mkoani Ruvuma, wakati akifunga Tamasha la Tatu la Taifa la Utamaduni lililoanza Septemba 20, 2024.

"Kutokana na mwingiliano wa utamaduni kutoka nje na maendeleo ya teknolojia, inaelezwa jamii ya Kitanzania imeanza kushuhudia mmonyoko wa maadili miongoni mwetu na vitendo visivyofanana na Utanzania. Jambo hili la mmonyoko wa maadili linaanzia nyumbani katika ngazi ya familia," amesema Rais.

Akaongeza, "Nitoe rai kwa kila Mtanzania kubeba jukumu la kukagua maadili katika boma lake na ninafurahi kuona viongozi wa kimila mahali hapa kwa sababu ninaamini kwa kushirikiana nao na taasisi zetu za kidini tutafanikiwa kushughulikia suala hili la mmonyoko wa maadili katika jamii yetu."

Naye Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro akizungumza kabla ya Rais Dk. Samia kwenye Tamasha hilo la Utamaduni, ameeleza kuwa, Tamasha la tatu la Utamaduni la Kitaifa Songea litatoa fursa lukuki kwa wakazi wa mkoa wa Ruvuma na mikoa ya jirani katika nyanja za kibiashara, bidhaa za asili, vyakula, malazi, usafiri na litaambatana na mafunzo, semina na midahalo mbalimbali kuhusu Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Amesema Tamasha hilo linahusisha maonesho ya ngoma na vyakula vya asili vya mikoa yote Tanzania Bara na Zanzibar kuanzia ambapo pia kulikuwa na mashindano ya ngoma na vyakula hivyo na washindi walipata zawadi.

Pia kulikuwa na onesho maalum la matumizi ya Kanga katika utamaduni wa Mtanzania ikiwemo kanga inavyotumika kubeba watoto, kata kichwani, kujifunga pamoja na kutoa ujumbe, akielekeza pia kulikuwa na mbio fupi (Jogging) ambapo vyama vya Jogging kutoka mikoa yote pamoja na mkutano wa vyama hivyo katika kukuza maendeleo yao.

**TUENZI UTAMADUNI WETU**

Waziri wa Sanaa na Michezo, Dk. Ndumbaro amesema serikali kupitia Wizara yake imetoa mikopo ya shilingi bilioni 4.2 kwa wasanii kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa.

"Mabadiliko kupitia mfuko wa Utamaduni na Sanaa yamenufaisha wasanii 214 ambapo wamenufaika na mikopo ya shilingi bilioni 4.2 na mwaka huu (Mheshimiwa Rais) umetuongezea shilingi bilioni 3 ili kuweza kufanya mabadiliko zaidi katika sekta ya Utamaduni na Sanaa."

**SAFARI YA KUIMARISHA UTAMADUNI**

Safari kubwa ya mageuzi ya kuimarisha utamaduni unaweza kusema imepamba moto, hii ikiwa ni baada ya kuanzisha Tamasha hili kubwa la Kitaifa la Utamaduni.

Tamasha hili linaleta mwamko mpya wa kiutamaduni ambao unajenga umoja kwa kuwaleta Watanzania pamoja kwa wakati mmoja.

Safari hii kubwa ya mageuzi ya kuimarisha utamaduni imepamba moto nchini na kuwa darasa kwa vijana wanaokua. Tamasha hili limewezesha wananchi wote kukutana nchi nzima na kuwa wa moja.

Wasiojua utamaduni wao wanapata fursa ya kujifunza, ikiwa ni ukurasa mpya kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Serikali itaendelea kuthamini, kulinda na kuendeleza utamaduni wa Mtanzania wakati wote.

Huu ni mwanzo mzuri wa safari kubwa ya kuimarisha utamaduni kwa kuwa matamasha yatainua na kuibua hazina kubwa ya kiutamaduni miongoni mwa jamii nchi nzima na yana tija kwa kuleta taifa.

Tamasha la Kitaifa la Utamaduni ni Tamasha lililozinduliwa kwa mara ya kwanza na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa kule mkoani Mtwara mwaka juzi na kukutanisha mikoa yote nchini.

Katika Tamasha hili shughuli mbalimbali za utamaduni hufanyika ikiwemo ngoma na maonesho ya vyakula na historia mbalimbali za makabila ya Tanzania.

Tamasha hilo ni maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa mkoani Mwanza mwaka 2021 wakati wa kuvikwa Uchifu Hangaya. Kimsingi tamasha hili limejumuisha vitu vikubwa vitatu, shughuli za utamaduni ambazo ni maonesho ya ngoma na vyakula vya asili, matembezi ya kiutamaduni, usiku wa taarabu na maadhimisho ya siku ya Kiswahili.

Vitu hivyo vyote vitatu vikubwa kwa pamoja ni ubunifu ambao umefanya wananchi kufurahia kuona tamaduni zao kwa wakati mmoja katika matukio ya kijamii.

Matukio haya yamefungua historia mpya ya nchi yetu ya kuyatumia ili kutangaza nchi yetu. Hakika huu ni mwanzo mzuri wa kutumia utamaduni katika kuitangaza nchi yetu.

**UTAMADUNI NI HAZINA YA NCHI**

Serikali inaendelea kushirikiana na kufanya kazi na makabila yote nchini ili kuendeleza mila njema kwa vizazi vijavyo. Utamaduni ni hazina ambayo kila kabila na taifa wanapaswa kuulinda na kuendeleza kwa kizazi hadi vizazi vijavyo.



Utamaduni ni tunu kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo hivyo machifu hawana budi kusimamia mila na desturi njema kwa watoto.

Serikali inaonyesha kuthamini utamaduni wa taifa letu kwa kuzingatia kauli ya Baba wa Taifa Mwal. Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema "Utamaduni ni kiini ama roho ya taifa lolote, taifa lisilo na utamaduni ni sawa na mkusanyiko wa watu usio na roho".

Kila mmoja wetu anawajibu wa kulinda Utamaduni, kuendeleza na kuuhifadhi ndiyo maana tunasema "Utamaduni wetu; Fahari yetu.

**KISWAHILI LUGHA YETU**

Katika kuendelea kuikuza na kuienzi Lugha adhimu ya Kiswahili kama sehemu ya utamaduni wa Mtanzania, Serikali kupitia Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na Watanzania walioko nje ya nchi (Diaspora) wanatarajia kufungua vituo 100 vya Kiswahili kote duniani.

Hayo yamesemwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika Uwanja wa CCM Majimaji, Songea mkoani Ruvuma, wakati akifunga Tamasha la Tatu la Taifa la Utamaduni lililoanza Septemba 20, 2024.

"Utamaduni una masuala mengi maana unahusu namna tunavyoishi. Kwetu sisi hatuwezi kuongea utamaduni wetu bila kugusa lugha yetu pendwa ya Kiswahili maana ndio lugha inayotuunganisha na kuwa na utamaduni mmoja, na lugha hii imefungua fursa za kiuchumi kwa Watanzania," alinena Dk. Samia na kuongeza.

"Kwa kulizingatia hili, Wizara (ya Sanaa, Utamaduni na Michezo) imenijulisha kwamba mwaka huu wamejipanga kufungua vituo 100 vya Lugha ya Kiswahili kote duniani kwa kushirikiana na Watanzania walioko nje ya nchi."

Rais Dk. Samia amesema Tanzania inatarajia kufungua vituo 100 vya kufundisha lugha ya Kiswahili duniani, hivyo amewataka Watanzania kutumia fursa hiyo kujiingizia kipato kama inavyofanyika katika nchi nyingine.

"Utamaduni una masuala mengi, maana inahusu jinsi tunavyoishi, kwetu sisi hatuwezi kuongelea utamaduni wetu bila kugusia lugha yetu pendwa ya Kiswahili, ndiyo lugha inayotuunganisha na kuwa na utamaduni mmoja. Lugha hii imefungua fursa za kiuchumi kwa Watanzania.

Dk. Samia amewataka vijana kuchangamkia fursa hii ikiwa pamoja na wale wabunifu kupitia mitandao mbalimbali kwani wana fursa pia ya kueneza na kutangaza lugha ya Kiswahili sambamba na kujiingizia kipato.

"Mitandao ile mnaweza mkafanya mambo tele, ukifungua mitandao mingine unawakuta watu wanafundisha Kiingereza mnaweza nanyi mkaingia mkafungua na mkafundisha Kiswahili," Dk. Samia amewasihi vijana.

Kiswahili ni miongoni mwa lugha za Kiafrika zenye wazungumzaji wengi barani hapa ambapo takribani watu milioni mia moja wanakitumia Kiswahili pamoja na wazungumzaji kutoka nje ya Bara la Afrika.

Muasisi wa taifa la Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipigania kuingiza lugha ya Kiswahili kutumika kama lugha ya taifa kupitia Chama cha Siasa cha TANU mwaka 1954 na Rais wa awamu ya Tano hayati John Pombe Magufuli alipigania Kiswahili iwe lugha ya kimataifa na sasa Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa msitari wa mbele kukibidhaisha Kiswahili duniani.

**Kwa maoni, ushauri; 0713 315966 au 0618 179 727.**

# 'Goli la Mama' linavyomotisha wanasoka

**Na Hamid Yassin**

TANGU Rais wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan aanze kutoa motisha ya fedha taslimu maarufu kama 'Goli la Mama' kwa timu za klabu na zile za taifa tumeshuhudia mafanikio makubwa kwenye soka letu.

Ingawa kuna wadau wa soka walikuwa na shaka na mpango huu wa Dk. Samia kutoa motisha kwa timu zetu wakidai anazidekeza, lakini sasa wapo kimya baada ya kushuhudia timu pinzani toka nje ya nchi zikipata vipigo vya 'shalubela'.

Motisha ya 'goli la Mama' ilianzia kwa klabu za Tanzania zilizokuwa zinaiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa tangu msimu wa 2022/ 2023 ambapo wanufaika kwa kwanza zilikuwa klabu za Simba na Yanga.

Wakongwe wa Simba na Yanga hawakupa fedha zile kwa upendeleo bali ilikuwa baada ya kuanza kufanya vema ndipo Dk. Samia akaamua kuwaongezea chachu ya kusaka ushindi zaidi.

Itakumbukwa msimu ule wa 2022/23 Yanga ilifika hadi hatua ya fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika huku watani zao Simba wakiishia hatua ya robo fainali ya mashindano ya Klabu Bingwa Afrika.

Hatua za awali 'Goli la Mama' kwa msimu huo zilianza kwa dau la Sh. 500,000 katika hatua za awali, lakini kadiri miamba hiyo ilivyosonga mbele ndipo Mama Samia naye alivyoongeza 'mzigo'!

Klabu ya Yanga ilipofika fainali na kucheza dhidi ya USM Alger ya Algeria, Rais Dk. Samia alipandisha dau la ushindi kutoka Sh. 10 milioni alilotoa hatua ya nusu fainali hadi Sh. 20 milioni.

Ingawa bahati haikuwa kwa upande wa Yanga kufuatia kulikosa kombe lile kwa kanuni ya goli la ugenini baada ya matokeo ya jumla kuwa bao 2-2, lakini motisha ya 'Goli la Mama' ilionekana dhahiri shahiri na 'Wananchi' waliambulia shilingi milioni 40 za Mama!

Nakumbuka Rais Dk. Samia alitoa ahadi ile wakati alipozungumza katika uzinduzi wa minara ya kurushia matangazo ya Kampuni ya Azam Media na kuwaambia wahudhuriaji kuwa, anaipongeza Yanga kwa kufuzu hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho na anaongeza dau ili kuwatia hamasa.

"Nitumie jukwaa hili kuipongeza timu yetu ya Yanga, wamecheza kwenye mashindano yetu vizuri na niliwapa msukumo kidogo, sasa Yanga inakwenda kwenye fainali, tunapokwenda kwenye fainali ni milioni 20 kwa kila goli la ushindi zaidi ya hapo Serikali itatoa ndege kuwapeleka katika mchezo wa fainali," amesema Rais jijini Dar es Salaam.

Aidha, Rais Dk. Samia aliwaomba viongozi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini Tanzania (TFF) kushirikiana na klabu hiyo kwa ukaribu ili kuwatia hamasa ya kupata ushindi kwani walikua wanaiwakilisha nchi ya Tanzania kimataifa.

Awali Rais Samia alitangaza kutoa kiasi cha Sh. 5 milioni kwa kila goli la ushindi kwa klabu za Simba na Yanga ambavyo vilikuwa vinashiriki katika michuano ya kimataifa ambayo ni Ligi ya Mabingwa Barani Afrika (CAFCL) pamoja na Kombe la Shirikisho Barani Afrika (CAFCF).

Klabu ya Simba iliondoshwa katika hatua ya robo fainali ya michuano ya CAFCL ikiwa imevuna kiasi cha Sh. 45 milioni ya 'goli la mama' kutokana na magoli ya ushindi iliyopata.

Siyo Simba na Yanga tu zinazoambulia fedha za 'goli la Mama' kwa msimu huu Azam FC nayo ilikabidhiwa Sh. Milioni 5 ya Goli la Mama kutoka kwa Rais Samia.

Azam FC ya jijini Dar es Salaam, ilikabidhiwa Sh. Milioni 5 ya Goli la Mama kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia kutokana na ushindi wake bao 1-0 dhidi ya APR ya Rwanda, katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza katika makabidhiano hayo, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Damas Dumbaro, alimshukuru Rais Samia kwa kuamua kujitosa kusaidia ukuaji wa michezo ukiwemo mpira wa miguu kwa kutoa zawadi za magoli ya ushindi kwa timu za Tanzania zinazocheza mashindano ya kimataifa.

Msimu huu tu wa 2024/25 Yanga imejipatia shilingi milioni 85 kama zawadi ya 'Goli la Mama' baada ya kuzifunga FC Vitalo'O ya Burundi jumla ya bao 10 na kuichapa AS CBE ya Ethiopia jumla ya bao 7!

Kwa mahasimu wao Simba ambao hawakucheza hatua za awali, wameshachota jumla ya shilingi milioni 15 baada ya kuitoa nje ya mashindano timu ngumu ya Libya ya Al Ahly Tripoli kwa bao 3-1.



> **Hatua za awali 'Goli la Mama' kwa msimu huo zilianza kwa dau la Sh. 500,000 katika hatua za awali, lakini kadiri miamba hiyo ilivyosonga mbele ndipo Mama Samia naye alivyoongeza 'mzigo'**



Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa hivi karibuni aliikabidhi timu ya Twiga Stars kitita cha shilingi milioni 10 zilizotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dk. Samia kufuatia ushindi waliopata dhidi ya timu ya Ivory Coast.

Akikabidhi kiasi hicho cha fedha, Katibu Mkuu, Msigwa alisema kuwa, wachezaji hao wanafanya kazi kubwa ya kuiwakilisha nchi kimataifa na Serikali ipo pamoja nao kwa kuwa wanaitangaza na kuipigania nchi yao.

"Mnapokuwa uwanjani katika mechi za kimataifa mnakuwa mmebeba matumaini ya Watanzania, katika mechi zote mlizocheza tumeona dhamira mliyonayo kwa nchi yenu, Mhe. Rais Dk. Samia anawapongeza sana, anafurahi sana anapowaona mnacheza uwanjani, anafurahi sana mnapopata matokeo mazuri katika mechi zetu," alinena Msigwa.

Pia timu ya Simba Queen ilijipatia jumla ya shilingi milioni 20 ikiwa ni zawadi ya 'Goli la Mama' kufuatia kufunga goli nne kwenye michuano ya Wanawake kwa timu za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati iliyofanyika nchini Ethiopia na kuambulia kushika nafasi ya nne.

Timu ya Taifa, Taifa Stars, nayo wachezaji wake wamekula sana fedha za 'Goli la Mama' kupitia michuano mbalimbali wanayoshiriki na kufunga magoli ikiwemo zile mechi za kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika zilizofanyika nchini Ivory Coast Februari mwaka huu.

**Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 au 0784 122 020.**



# Kona ya Urembo



Na Hidaya Machupa

# Shanga Katika urembo na mitindo





### HISTORIA NA ASILI YA SHANGA

SHANGA zimekuwa na umuhimu mkubwa katika tamaduni nyingi za Kiafrika, ikiwemo Tanzania, Kenya, Afrika Kusini, na maeneo mengine ya dunia.

Zimekuwa zikitumika kwa maelfu ya miaka, si tu kama mapambo, bali pia kama alama za kitamaduni, kifahari, na kisayansi. Shanga hutengenezwa kwa vifaa mbalimbali kama vile kioo, mbao, chuma, plastiki, na madini, na hutumiwa kutengeneza mikufu, vikuku, pete, na vipuli.

### SHANGA KATIKA UREMBO NA MITINDO

Katika ulimwengu wa urembo na mitindo, shanga zimekuwa zikipewa kipaumbele kwa muda mrefu kutokana na mvuto wake wa kipekee na utofauti wake.

Wanamitindo wengi wamekuwa wakitumia shanga kuongeza thamani ya mavazi yao, hasa kwenye mitindo ya kipekee kama ya kitamaduni au ya kisasa yenye mchanganyiko wa asili na mitindo ya kisasa.

Shanga huvaliwa sehemu mbalimbali za mwili kama shingoni (mikufu), miguuni (vikuku), kiunoni (mikanda ya kiuno), na kwenye masikio (vipuli).

Aina na rangi ya shanga huweza kubeba maana tofauti katika jamii mbalimbali, huku zingine zikiwa na alama za kifahari, heshima, au hata mahusiano ya kijamii.

### UMITINDO WA KIKE NA WA KIUME

Wakati shanga mara nyingi zinahusishwa na wanawake, baadhi ya makabila na mitindo ya kisasa hutoa nafasi kwa wanaume pia kuvaa shanga kama sehemu ya mtindo wao wa maisha.

Kwa mfano, katika tamaduni fulani za Afrika Mashariki kama vile Wamasai, shanga ni sehemu muhimu ya mavazi kwa wanaume na wanawake, zikitumika kama alama za umri, ndoa, na hali ya kifahari.

Shanga zimekuwa sehemu ya urembo kwa makabila kadhaa katika bara la Afrika, hususan makabila kama Wamasai

### WAMASAI NA SHANGA

Wamasai ni mojawapo ya makabila yanayojulikana zaidi kwa kutumia shanga katika mavazi yao ya kitamaduni. Wanawake wa Kimasai hupamba miili yao na mikufu mirefu ya shanga, na rangi ya shanga huwa na maana maalum kama vile; Nyekundu kuwa na maana ya ujasiri na nguvu, nyeupe ni amani na afya, bluu Maji, uhai na mbingu njano ni wingi na rutuba.



Wadigo; ni kabila dogo linaloishi pwani ya Tanzania, karibu na mkoa wa Tanga. Shanga hutumiwa na wanawake wa Kigiriki kama mapambo kichwa, shingoni, na kiunoni. Maana ya shanga kwa Wadigo ni pamoja na urembo wa mwanamke, lakini pia kuonyesha umri, hali ya ndoa, na heshima katika jamii.

Wamakonde; wanapatikana kusini mwa Tanzania, maarufu kwa sanaa yao ya uchongaji, pia hutumia shanga kama mapambo. Wanawake wa Kimakonde huvaa shanga wakati wa sherehe za kitamaduni, hususan katika ngoma za jadi kama vile Sindimba.

Shanga za Wamakonde zinaweza kuwa alama ya utambulisho wa kitamaduni na pia kuonyesha umri na hadhi ya mtu katika jamii.

Wakamba; nao hutumia shanga, hasa wanawake, katika mapambo ya kichwani na shingoni. Shanga hizi mara nyingi huvaliwa wakati wa sherehe maalum kama vile za kitamaduni na harusi.

Wanyakyusa; Hawa ni kutoka mkoa wa Mbeya pia wanajulikana kwa kutumia shanga kama sehemu ya urembo na mavazi ya kitamaduni. Wanawake wa Kinyakyusa huvaa shanga wakati wa sherehe za harusi na ngoma za kitamaduni kama vile Makwaju.

Shanga zinavaliwa kuonyesha hali ya ndoa na uzuri wa wanawake, huku rangi tofauti zikionyesha maana maalum kama furaha au huzuni.

Wahehe; Ni kabila kutoka mkoani Iringa, maarufu kwa historia yao ya kijeshi na ujasiri. Wanawake wa Kihehe hutumia shanga kwa ajili ya mapambo ya mwili, hasa wakati wa sherehe za kijamii kama harusi na sherehe za mpito.

Shanga hizi zinaweza kuonyesha uzuri, ubikira wa binti, na pia heshima kwa familia.

Wanyamwezi; Ni kabila kutoka mkoa wa Tabora ambalo pia hutumia shanga kama sehemu ya mapambo na urembo. Wanawake wa Kinyamwezi huvaa shanga wakati wa sherehe za harusi, tohara, na matukio ya kijamii. Shanga hizi mara nyingi huwa za rangi tofauti, na zinaweza kuonyesha hali ya ndoa, uzazi, na nafasi ya mtu katika jamii.



### WATAALAMU WA UREMBO NA MITINDO NA MATUMIZI YA SHANGA

### UCHAGUZI WA RANGI NA VIFAA

Unapochagua shanga, ni vyema kuzingatia rangi inayolingana na mavazi yako au tukio unalohudhuria. Rangi ya shanga inaweza kubeba ujumbe au kuonyesha hisia maalum, hivyo ni vyema kuchagua rangi zinazofaa.

### MITINDO MCHANGANYIKO

Wataalamu wanapendekeza kutumia shanga za kitamaduni kwenye mavazi ya kisasa ili kutoa mchanganyiko wa mitindo (fusion fashion). Hii inafanya mtindo wako kuwa wa kipekee na wa kuvutia zaidi.

### UBORA WA SHANGA

Ni muhimu kutumia shanga zilizotengenezwa kwa vifaa bora ili kuepuka kuvaa bidhaa ambazo zinaweza kusababisha athari za kiafya kama vile aleji. Vifaa kama vile shanga za kioo au madini ni maarufu zaidi kwa sababu ya ubora wake na uimara.

### MATUMIZI YA KIMAADILI

Baadhi ya wataalamu wa mitindo wanashauri matumizi ya shanga ambazo hazikugharimu mazingira au jamii. Kwa mfano, ununuzi wa shanga kutoka kwa wasanii wa ndani au vikundi vya kijamii huimarisha uchumi wa ndani na pia kuhakikisha kuwa unatumia bidhaa zenye thamani ya kiuchumi na kijamii.

Shanga zimebeba maana kubwa katika ulimwengu wa mitindo na urembo. Kutoka kwa mapambo ya kawaida hadi sherehe maalum, shanga zina uwezo wa kuwasilisha ujumbe, hali ya mtu, na utambulisho wa kitamaduni.

Kupitia ushauri wa wataalamu wa mitindo na urembo, tunaweza kuelewa jinsi ya kutumia shanga kwa njia bora zaidi ili kuimarisha mtindo wa kipekee na wa kuvutia.



Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti



Uwanja wa Arusha utakavyokuwa ukikamilika

# Dk. Samia: Michezo ni ajira, vijana changamkieni fursa

**Na Hamid Yassin**



WAKATI Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dkt. Damas Ndumbaro akimwahidi Rais Samia Suluhu Hassan kuleta medali 5 kwenye michezo ya kimataifa ya Olimpiki itakayofanyika mwaka 2028 nchini Marekani, mwenyewe amepasha kuwa, michezo ni ajira na kuwataka vijana kuchangamkia fursa hiyo.

Dkt. Samia alisema hayo wakati wa ufungaji wa Tamasha la Utamaduni la Taifa lililoanza Septemba 20, 2024 mkoani Ruvuma ambapo alibainisha hivi sasa michezo ni ajira tosha na Serikali yake ipo tayari kuweka mazingira rafiki ya kufanikisha hilo.

Moja ya ahadi yake kwenye Tamasha hilo la Songea ni ujenzi wa miundombinu ya kisasa ikiwemo ujenzi ulioanza kule mkoani Arusha wa Uwanja mkubwa wa kisasa.

Naye Waziri Ndumbaro aliweka wazi kwamba, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amefanya uwekezaji mkubwa kwenye michezo ikiwemo kukubali kuwa mwenyeji wa michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) ya mwaka 2027 hivyo sekta hiyo inatakiwa kufanya maendeleo makubwa kulingana na uwekezaji huo.

### MICHEZO NI SOKO LA AJIRA

Tanzania ina wachezaji 54 wa kulipwa nje ya nchi wengi wao wamepitia michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA, na sasa wamepata ajira, na kuliletea heshima kubwa taifa. Mashindano haya yameleta mafanikio makubwa kiuchumi na kijamii kwa wananchi.

Mashindano ya Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi na Sekondari (UMITASHUMTA) na Sekondari (UMISSETA) ni mashindano ya michezo yanajumuisha mikoa yote kutoka Tanzania Bara na Visiwani ambapo michezo mbalimbali hushindanishwa ili kuleta uhai katika timu za Taifa ambao unatokana na kuwepo kwa vipaji vinavyozalishwa kuanzia shule za msingi na sekondari.

Katika UMITASHUMTA michezo inayoshindaniwa ni pamoja na mpira wa miguu kwa wasichana na wavulana, mpira wa miguu maalum kwa wavulana (wenye ulemavu wa kusikia) mpira wa pete, mpira wa goli kwa wasichana na wavulana wasioona na wenye uoni hafifu, mpira wa wavu kwa wasichana na wavulana, mpira wa mikono kwa wasichana na wavulana, mpira wa meza kwa wasichana na wavulana, riadha jumuishi, kwaya na ngoma.

Kwa upande wa UMISSETA michezo inayochezwa ni yote ya UMITASHUMTA pamoja na mchezo wa mpira wa kikapu kwa wasichana na wavulana isipokuwa mchezo wa mpira wa goli, pamoja na mashindano ya usafi katika mazingira. Mashindano haya hupambwa na wasanii ili kutoa hamasa na burudani. Pia vyama vya michezo, mashirikisho na vilabu vya michezo mbalimbali hushiriki kuangalia vipaji mbalimbali.

Serikali inaangalia uwezekano wa kuwa na kanda za UMISSETA na UMISHUMTA kwa maana ya kuwa na kanda au mikoa itakayochaguliwa maalum na shule maalum zenye miundombinu ya michezo ili miundombinu ya kisasa iongezewe kwenye shule hizo.

Hii itawafanya vijana waweze kucheza katika mazingira ya kiwango cha kimataifa ili wakienda kwenye mashindano ya kimataifa waone mazingira yanafanana na nyumbani hatimaye waendelee kufanya vizuri zaidi.

Mashindano haya huandaliwa na Wizara tatu zinazohusika na Elimu, Habari na TAMISEMI chini ya Kamati ya Uratibu ya Kitaifa ya Makatibu Wakuu wa Wizara hizo. Kupitia mashindano haya, wanafunzi wanapata fursa adhimu ya kujifunza uzalendo.

Vilevile vijana wanapata nafasi ya kuonesha na kujifunza tamaduni za Makabila ya mikoa mbalimbali kupitia ngoma ya ndani ya Mkoa na ngoma za nje ya mikoa yao na vipaji binafsi huibuliwa.

Wizara ina jukumu kubwa kama wasimamizi wa sekta wa kuweka mfumo mzuri wa kuvuna vipaji na kuviingiza katika soko la ajira katika sekta za michezo na sanaa.

### MIUNDOMBINU

Rais Dk. Samia ameidhinisha ujenzi wa viwanja viwili vikubwa vya kiwango cha Olimpiki kwenye mikoa ya Arusha na kule Makao Makuu ya nchi Dodoma.

Ujenzi wa Uwanja mpya wa kisasa wa mpira wa miguu na michezo mingine jijini Arusha utakaoitwa Dk. Samia Suluhu Hassan, tayari umeanza baada ya serikali kutoa Sh. bilioni 286 kwa shughuli hiyo.

Uwanja huo unaojengwa na Kampuni ya CRCEG kutoka nchini China ambayo ilijenga reli ya Tazara, ni sehemu ya maandalizi ya fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2027, zitakazofanyika Tanzania, Kenya na Uganda.

Akizungumza Dar es Salaam, wakati wa hafla ya utiaji saini ya ujenzi wa uwanja huo, Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, amesema uwanja huo utaingiza watu 30,000 na utakuwa miongoni mwa viwanja vya kisasa hapa nchini.

Amesema serikali inahakikisha ujenzi huo unafanywa kwa haraka kwa kuwa Tanzania itakuwa mwenyeji wa AFCON 2027, ikiwa ni juhudi zinazofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia.

Dk. Ndumbaro amesema uwanja huo pia utachagiza kwa kiasi kikubwa utalii wa Tanzania kwani zitafanyika shughuli mbalimbali tofauti na mpira wa miguu kama vile mchezo wa riadha, pamoja na biashara zitakazokuwa zinafanyika uwanjani hapo.

"Uwanja huo utakuwa na ubora wa hali ya juu kwani utakuwa na vyumba vya watu mashuhuri pande zote mbili za uwanja zoezi hili limefanyika wakati huu rais wetu akiwa anatimiza miaka mitatu ya uongozi wake," alisema Dk. Ndumbaro siku mkataba wa ujenzi wa uwanja huo uliposainiwa.

Siyo uwanja huo wa Arusha tu, Dk. Samia pia ameidhinisha kujengwa kwa uwanja mpya wa kisasa Jijini Dodoma sambamba na kukarabatiwa kwa viwanja vyote nchini vikiwemo vile vinavyomilikiwa na Chama cha Mapinduzi na vya Serikali.